



GIRLS NOT BRIDES

The Global Partnership
to End Child Marriage



SIMAMA, SIKIKA!

Mafunzo kwa vijana wanaharakati – kukuwezesha
kukomesha kuoza kwa watoto

Mwongozo wa mkufunzi

Shukrani

Tungependa kushukuru mashirika yote yanayounga mkono *Girls Not Brides*, waajiriwa na washauri wetu wanaofanya kazi kwenye sekta hii, ambao walichangia kuandaa mwongozo huu.

Picha ya jalada: © Jessica Lea/ Department for International Development (DFID)

Usanifu www.alikecreative.com


Vielelezo: Ariadna Vásquez

SIMAMA, SIKIKA!

**Mafunzo kwa vijana wanaharakati –
kukuwezesha kukomesha kuoza kwa watoto**

Mwongozo wa mkufunzi





“Kila hatua tunayochukua italetu mabadiliko na maendeleo ambayo yatatuwezesha kukaribia lengo letu la kukomesha kuoza kwa watoto.”

Mara nyingi, tunasikia watu wakisema “vijana ndio viongozi wa kesho,” na kwamba, “vijana wanafaa kupewa nafasi za uongozi.” Lakini, ninatambua kuwa vijana tayari wanaongoza. Moja kati ya mashirika matatu yanayounga mkono *Girls Not Brides* yanaongozwa na vijana, na habari hii kwa hakika ni ya kufurahisha mno. Vijana hawa wanaendesha mikakati ya kila siku katika mashirika hayo, wanafanya maamuzi, pamoja na kuongoza shughuli nyinginezo ambazo zinaahidi ufanisi katika uendeshaji wa mashirika hayo ya kiraia. Idadi ya vijana wanaowakilishwa katika mashirika yanayounga mkono *Girls Not Brides* inathibitisha kwamba vijana kwa ujumla wanaongoza katika harakati za kuleta mabadiliko katika jamii zao. Lakini, licha ya hayo, mara nyingi michango yao haitambuliwi au kupewa sifa inayostahili, au hata zaidi, wanakosa kusikizwa.

Masuala hayo ndiyo yananisababisha kulisimka kuhusu mwongozo huu wa uanaharakati. Kwa kuwa umeandaliwa kwa na ushirikiano wa vijana wanaharakati, mwongozo huu utawasaidia kushupaza na kuimarisha majukumu ambayo vijana wanaweza, au tayari wanatimiza kukabiliana na kuoza kwa watoto kote ulimwenguni. Ndani yake, utapata mbinu na mikakati anuwai na yenye burudani pia, ambayo yatakusaidia kuwaongoza vijana ili wawe mabalozi wa mabadiliko katika jamii zao.



Pamoja na kuwa mabingwa katika jamii zao, kazi za kuvutia ambazo vijana wanafanya zinafaa kuwahakikishia nafasi na jukumu maalum kwenye mikakati zinazoendelezwa katika viwango vya kitaifa. Wanahitaji viti kwenye meza wakati maamuzi muhimu yanatolewa kuhusu sera ambazo zinaathiri lengo la kukomesha kuozwa kwa watoto. Bila vijana kwenye nafasi hizi, mbinu za kufanya maamuzi zitakosa ufanisi na hatutaona mabadiliko ambayo tunahitaji.

Ninaelewa moja kwa moja hali ambapo watu wengine wanataka kufanya maamuzi kuhusu maisha yako ya usoni bila kukuhusisha; watu ambao wanafikiria kwamba kuozwa ukiwa bado mtoto ndiyo njia pekee ambayo maisha yako yanaweza au yanafaa kuchukua.

Nilikuwa mkimbizi jijini Terhan ambapo ndugu yangu alirudi nyumbani Afghanistan na kuamua angetenda kuoa. Wazazi wangu walihitaji kutafuta pesa ili aweze kununua mke. Hivyo basi, wazazi wangu wakaamua kuniuza mimi nirolewe ili wapate hela walizohitaji. Nilijawa na huzuni. Hayo si maisha ambayo nilitaka. Nilitarajia kwenda shuleni. Sikuwa mali ya kuuzwa na kununuliwa.. Sikufikiri hata siku moja ningetarajiwa kurudi nyumbani na kuishi maisha ya utumwa. Kwa hivyo nikaamua kuandika wimbo wa kupinga hayo. Niliuita

wimbo huu Binti wa Kuuzwa (Daughters for Sale) na kwa usaidizi wa rafiki yangu, tukaunda video ya wimbo huu kisha tukaiweka kwenye mtandao wa YouTube. Ilitazamwa na watu wengi mno! Watu kutoka sehemu zote duniani walifanya hima kutufikia na kutokana na msaada wa baadhi ya watu hao wema, nikaja kuishi nchini Marekani. Leo, kwa mara ya kwanza, niko katika shule halisi na ninatarajia kuishi maisha ambayo nitajichagulia mwenyewe. Ingawa maisha yangu yamebadilika kwa njia nyingi, jambo moja halitabadilika kamwe: jukumu langu la uanaharakati la kukomesha kuozwa kwa watoto.

Hivyo basi, ninakuhimiza – kama kijana, mwanaharakati na balozi wa kimataifa wa *Girls Not Brides* – utumie mwongozo huu kueneza matumaini na nguvu. Kila hatua ambayo kila mmoja wetu anachukua katika kazi hii italeta mabadiliko na itatuwezesha kukaribia lengo letu la kukomesha kuozwa kwa watoto. Tafadhali shirikiana na, na uwahimize vijana wa asili, jinsia na usuli mbalimbali wahusike, kwa sababu ni kwa kushirikiana pamoja tu ndivyo tutaweza kukomesha kuozwa kwa watoto. Asante.

Sonita Alizadeh

Kijana Mwanaharakati na Balozi wa Kimataifa wa *Girls Not Brides*



Picha © Lucia / Unsplash

Yaliyomo

Utangulizi	8
Jitayarishe kuanza!	12
Moduli 1 - Kuozwa kwa watoto ni nini? Mambo ya Msingi	19
Moduli 1 - Kikao 1: Tushirikiane pamoja!	20
1.1 Mwongozo wako wa ukufunzi	21
Moduli 1 - Kikao 2: Kuozwa kwa watoto ni nini? Utangulizi	26
1.2 Mwongozo wako wa ukufunzi	27
Moduli 1 - Kikao 3: Kuozwa kwa watoto Athari na ukingaji	36
1.3 Mwongozo wako wa ukufunzi	37
Moduli 2 - Kufanya utafiti kuhusukuoza kwa watoto kwenye jamii yako	44
Moduli 2 - Kikao 1: Kuchunguza jinsia	46
2.1 Mwongozo wako wa ukufunzi	47
Moduli 3 - Chukua hatua - Imarisha mkakati wa uanaharakati	60
Moduli 3 - Kikao 1: Malengo na madhumuni	62
3.1 Mwongozo wako wa ukufunzi	63
Moduli 3 - Kikao 2: Kuunda rasimu ya mikakati ya uanaharakati	68
3.2 Mwongozo wako wa ukufunzi	69
Moduli 4 - Pamoja, tuna nguvu zaidi!	84
Moduli 4 - Kikao 1: Nguvu ya ushirikiano	86
4.1 Mwongozo wako wa ukufunzi	87
Moduli 5 - Mwongozo wako wa ukufunzi	96
Ufuatiliaji wa maendeleo, hatua za ushirikiano na mafunzo	98
5.1 Mwongozo wako wa ukufunzi	99

Utangulizi

Girls Not Brides ni ushirikiano wa kimataifa wenye zaidi ya mashirika 1000 ya kiraia kutoka zaidi ya nchi 95 katika sehemu zote duniani, ambazo zimejitolea kukomesha kuozwa kwa watoto na kuwawezesha wasichana wafikie uwezo wao kamili. Sote tunaamini kwamba kila msichana ana haki ya kuishi maisha ambayo amechagua mwenyewe na kwamba, tukikomesha kuozwa kwa watoto, tunaweza kufikia mustakabali salama, wenye afya na mafanikio kwa wote.

Maana tunatambua tuna nguvu zaidi pamoja, mashirika ya **Girls Not Brides** hufanya kazi katika nyanja mbalimbali ili kufikia tumaini na lengo letu la kukomesha kuozwa kwa watoto. Wanasaidia kuhamasisha kuhusu suala la kuozwa kwa watoto duniani kote, kukuza uelewa kuhusu kitakachohitajika ili kukomesha kuozwa kwa watoto, na kuanzisha mabadiliko endelevu katika sheria, sera na ratiba katika ngazi za kitaifa na kijamii; hatua zote zitakazoleta mabadiliko kwenye maisha ya mamilioni ya wasichana.

Kukuza Ubalizi wa Vijana

Hapa **Girls Not Brides**: Ushirikiano wa Kimataifa Dhidi ya Kuozwa kwa Watoto, tuna fahari kuwa sasa hivi, theluthi moja ya mashirika yanayotuunga mkono yanaongozwa na vijana, au yanafanya kazi pamoja na vijana. Pamoja na hayo, mashirika hata zaidi wanafanya kazi na vijana kupitia ratiba na miradi, kuwasaidia na kuwaimarisha ili waweze kujiandalia maisha yao ya usoni. Tunaamini kwamba hatutaweza kufikia lengo letu la kukomesha kuozwa kwa watoto bila ushirikiano thabiti na amilifu na vijana. Hizi ndizo sababu zetu za kuamini haya.

- **Vijana ni mawakala shupavu wa mabadiliko.** Vijana ndio waathirika wa kwanza wa kuozwa kwa watoto na sauti zao lazima zisikike. Wana uwezo wa kuongeza ufahamu wa suala hili muhimu ili kusaidia jamii zao kuelewa athari mbaya kwa wasichana, familia na jamii.
- **Kukosa kushirikisha vijana kwenye juhudi za kukomesha kuozwa kwa watoto ni kupitwa na nafasi ya kufikia matokeo kwa**

kiwango kinachokithiri. Katika nchi nyingi mno ambapo idadi ya watoto wanaooswa inaongezeka, vijana wanawakilisha idadi kubwa ya wananchi. Kwa mfano, nchini Uganda, takriban nusu ya wananchi wako chini ya umri wa miaka 24, na nchini India, kuna zaidi ya vijana milioni 200.

- **Kushirikisha vijana ni njia bora na muhimu ya kukabiliana na kuozwa kwa watoto kwenye nyanja za kijamii.** Kutokana na tajiriba yetu, tumetambua kwamba vijana wakiwa mawakala wa mabadiliko, wamefikia matokeo mazuri kwenye jamii zao. Kwa mfano, wanasaidia kuongeza ufikiaji na viwango vya miradi, na kushirikisha vikundi mbalimbali, hasa vikundi vinavyobaguliwa.
- **Kushirikisha vijana kunaweza kusababisha miito ya kuchukua hatua na miito ya kubadilisha sera iwe jasiri na bunifu zaidi.** Kufanya kazi pamoja na vijana kunaweza kufungua nafasi za kujadili sera ambazo zinafikiriwa kuwa “zimedhibitiwa” pamoja na watu wenye ushawishi mkubwa katika nafasi hizo.

Kwa nini tumetengeneza mwongozo huu wa ukufunzi kuhusu uanaharakati na lengo lake ni lipi?

Mashirika mengi yanayounga mkono *Girls Not Brides* hupeana mafunzo na hufanya kazi na vijana kukabiliana na masuala yanayohusu kuozwa kwa watoto katika jamii zao na pia kupitia ratiba zao. Lakini mashirika haya yalitueleza kwamba wanahitaji mwongozo wa ukufunzi ambao ni rahisi, wenye ufanisi, kitakachowavutia vijana, pamoja na kuwapa mashirika haya ushauri kuhusu njia bora za kuwafunza vijana uanaharakati dhidi ya kuozwa kwa watoto katika jamii zao. Ili kutimiza mahitaji yao, tuliunda ratiba na mwongozo huu kwa ajili yako - na tulishirikiana na vijana wetu watetezi na wanaharakati. Mwongozo huu una lengo la:

1. Kuwezesha wakufunzi (vijana na pia watu wazima) kuelekeza na kuwasaidia vijana kwa ufanisi kuwa wanaharakati kwenye masuala yanayohusu kuozwa kwa watoto kwenye jamii zao. Kawaida tunapozungumzia vijana, huwa tunazungumzia wenye umri wa kati ya miaka 15 na 24. Hii inajumuisha masafa mbalimbali ya vikundi: vijana wa kike na wa kiume ambao waliepuka kuozwa kwa watoto, wale walio hatarini kuozwa wakiwa watoto na wale ambao wamewahi kuolewa au wameolewa. Vijana ambao wanatekeleza mwongozo huu wanapaswa kuwa na uzoefu wa ukufunzi au wa kufunza vijana wa rika zao.

2. Kuwapa vijana wanaharakati rasilimali za kuisisimua na mwongozo bunifu kuhusu jinsi ya kukabiliana na suala la kuozwa kwa watoto katika mataifa yao na jamii zao.
3. Kuwa na mizizi katika mitazamo ya vijana. Mwongozo huu ulitengenezwa na watu anuwai, ikiwemo mashirika yanayounga mkono *Girls Not Brides*, vijana wanaharakati, washauri wa nje, na waajiriwa wa *Girls Not Brides*. Ni muhimu kabisa kuhakikisha kwamba nyenzo yoyote ambayo itatumika na vijana imeandaliwa na wao wenyewe.
4. Kuhamasisha! Kwa kusambaza uchambuzi wa visa kutumia mbinu tofauti za utafiti kutoka sehemu mbalimbali duniani, tunatumai tutakuonesha mifano jinsi wengine wanakabiliana na kuozwa kwa watoto katika jamii zao.

Mwongozo huu unafaa kutumiwa na nani?

Muhtasari na ushauri kwenye mwongozo huu umekusudiwa kutumika na vijana wenye umri kati ya miaka 15 na 24. Tumewalenga wale ambao hufanya kazi na vijana wengineo kuhusu masuala ya kuozwa kwa watoto katika jamii zao. Tunatumai pia kuwa mwongozo huu utakuwa wa msaada kwa mashirika mengine ya *Girls Not Brides* ambayo hufanya kazi na vijana ili wawe mawakala wa mabadiliko. Wafadhili, watunga sera na mashirika ya kiraia pia watasaidika kwa maana kitabu hiki kina ushauri na mapendekezo kuhusu jinsi ya kushirikisha vijana katika kukomesha kuozwa kwa watoto.



KUMBUKA

Baada ya kutumia mipangilio ya vikao ambayo imeainishwa kwenye mwongozo huu na kukamilisha mafunzo na vijana, tunatumai ratiba hii itasaidia kuwawezesha vijana ambao unafanya kazi nao ili waweze kutimiza yafuatayo:

- Waweze kueleza kuozwa kwa watoto ni nini, kunasababishwa na nini, athari zake ni zipi, na jinsi kunaweza kuzuiwa.
- Waweze kufanya utafiti kuarifu uanaharakati wao wa kukomesha kuozwa kwa watoto.
- Waweze kuunda mkakati rahisi na safi, unaoonyesha mipango yao ya kazi ya uanaharakati, na kuhamasisha ufahamu, na jinsi watakavyowasilisha kazi ambayo wanafanya na suala la kuozwa kwa watoto.
- Waweze kuelewa jinsi ya kujenga mfumo wa kusaidiana na vijana wenzao, na jinsi ya kushawishi wanaharakati muhimu ambao wana uwezo wa kusaidia kazi yao.
- Waweze kuelewa hatari zinazoambatana na kazi ya uanaharakati na kampeni na jinsi ya kukwepa na hatari hizo.
- Wajifunze jinsi ya kutathmini kazi ambayo wanafanya, wawe na uwezo wa kutambua na kuonesha mabadiliko ambayo wanasaidia kufikia.
- Wawe wamejifunza kuhusu njia tofauti za kukabiliana na kuozwa kwa watoto, na wawe na uwezo wa kutumia mafunzo na mifano ya uanaharakati wenye mafanikio kutoka mashirika mengine au nchi nyinginezo.

Jinsi ya kutumia mwongozo huu wa mkufunzi

Kuna moduli tano katika mwongozo wa mkufunzi, Simama, Sikika! ambazo utatumia kufanyia mafunzo pamoja na kikundi chako. Kila moduli ina:

- Muhtasari wa kila kikao cha mafunzo.
- Vitu ambavyo utahitaji kutayarisha kabla ya mafunzo - ikiwemo michezo, mawasilisho na hata vifaa vya maandishi (kama vitabu na karatasi) vya kila kikao.
- Wakati uliopendekezwa kwa kila shughuli na idadi ya washiriki iliyopendekezwa kwa kila kikao.
- Maelezo zaidi ya mpangilio ambayo utatumia kuongoza kila kikao: ikiwa ni pamoja na mpango, wakati uliopendekezwa na jinsi ya kusimamia kila kikao.
- Maelezo zaidi ya kuongoza masomo yote katika kila kikao: ikiwemo shughuli za kulisimua, maelezo na mapendekezo kuhusu mambo ambayo utazungumzia kwa kikundi.

Kila kikao cha mafunzo ndani ya moduli kimegawanyishwa katika sehemu tatu:

- Ya kwanza ni muhtasari wa kikao: malengo, wakati uliotengwa na matayarisho yatakayohitajika kabla ya kikao.
- Ya pili inaonyesha hatua-kwa-hatua jinsi mafunzo yamepangwa ikiwemo shughuli ambazo utakamilisha kwa kikao.
- La mwisho ni mwongozo kwa mkufunzi: ikiwemo mambo yote ambayo utahitaji kujua kuhusu mada ya mjadala, mapendekezo ya mafunzo, na baadhi ya shughuli za kulisimua au michezo ya kucheza na kikundi chako. Kama mkufunzi, hakikisha umesoma kwa makini na umelewa sehemu hii vyema kwa sababu itaunda vikao vyako na mafunzo ambayo utawapa wenzako.

Tunapendekeza ufuatilie kila moduli kwa mpangilio tuliokupa hapa ili kikundi chako kipate kuelewa masuala yote na jinsi masuala yanavyohusiana - lakini unaweza kuchagua mpangilio utakaokufaa.

Maelezo ya ziada

Mawasilisho yako katika kikundi

Tunafahamu kwamba unaweza kuwa na au kukosa ufikiaji wa mtandao, projekta au kompyuta ndogo, ama hata pahala rasmi pa kufanyia vikao - usijali! Unaweza kusaidia kufunza vijana pahala popote na hutahitaji vifaa rasmi kwenye vikao hivi. Tumeangazia baadhi ya sehemu kuu ambazo zinaweza kuwasilishwa kutumia kompyuta ama kuandikwa kwenye chati. Haya mawasilisho “ya mfano” ni mapendekezo kuhusu mafunzo ambayo unastahili kuwapa kikundi chako, na sehemu hizi zimeangaziwa kote ndani ya mwongozo wa mkufunzi ili kukusaidia kufanya matayarisho ukiendeleza vikao hivyo. Jisikie huru kuzitumia, kuzibadilisha au kuongeza maelezo zaidi ambayo unahisi yatahusika au kuwa muhimu zaidi kwa kikundi chako. Ukiendeleza mafunzo, itakusaidia kuwa na baadhi ya hoja muhimu na maelezo ya hoja hizo zikiwa zimeainishwa kwenye mifano kwa mawasilisho, na zikiwa zinaonekana na wote katika vikao - kama vile kwa kuzipachika ukutani kwenye chati - ili watu waendeleo kuzisoma na kuzikumbuka.





Picha © Abdullah al Kaf / Girls Not Brides



Mwongozo wa washirikiki

Tumetengeneza mwongozo wa washirikiki utakaotumika na kikundi chako. Mwongozo huu una mafunzo yote ambayo mtazungumzia katika kila kikao, yakiwa yameainishwa vizuri ili yaeleweke vyema na kikundi.

Mwongozo umeundwa ili kuwasaidia washirikiki waweze kufuata vikao vyako, na pia ili utumike kama nyenzo ya kuwawezesha kusoma baadaye mafunzo yoyote ambayo walipokea, kujikumbusha hoja ulizozungumzia katika vikao na kuwasaidia katika siku za usoni wanapokuza uanaharakati wao na kuimarisha sauti zao za kutetea walioathiriwa na kuozwa kwa watoto. Kifurushi hiki pia kina violezo na majedwali ambayo hayajajazwa ambayo yatumika kufanyia mazoezi na kwa shughuli za kikundi. Utazipitia pamoja na kikundi chako katika vikao mbalimbali.

Tunapendekeza uzichapishe ukihakikisha kila mshiriki kwenye kikundi ana nakala yake ili waweze kujihifadhia kila nakala kutumika baadaye, aidha watakapoanza kazi yao ya uanaharakati, ama watakapotaka kujikumbusha waliyosoma katika vikao. Mwongozo wa washirikiki pia una viungo vya tovuti na mapendekezo kuhusu nyenzo nyinginezo ambapo washirikiki wanaweza kupata mafunzo zaidi kuhusu mada tofauti. Tunapendekeza utumie hadithi na chambuzi za visa kutoka kwa jamii yako au taifa lako kuwasaidia washirikiki kupata mifano kuhusu jinsi wengine walivyofanya uanaharakati na kuibuka wanaharakati shupavu wanaodai kukomeshwa kwa kuozwa kwa watoto. Tunatumai mifano hii itahamasisha kikundi chako kufanikisha mabadiliko makubwa.

La mwisho la muhimu kukumbuka

Unaelewa kikundi chako, jamii yako na taifa lako vyema zaidi, kwa hivyo unajua mkakati bora wa kutumia pamoja na vijana ambao unashirikiana nao. Jisikie huru kubadili mapendekezo ya vikao ili kukuwezesha kupitia kitabu pamoja na mafunzo yaliyomo kwa mwendo ambao utafaa kikundi chako na wewe binafsi pia na ukufunzi ufae mahitaji yenu.

Jitayarisha Kuanza!

Masomo muhimu kwa wakufunzi

Mkufunzi ni nani na kazi yako ni ipi?

Mkufunzi ni mshauri au kiongozi wa majadiliano kwenye kikundi. Kuna majina mengi ambayo hutumika kufafanua wajibu huu, kama vile “msimamizi” - lakini tutatumia jina “mkufunzi”. Mchakato wa kuendesha kikao au vikao vya ukufunzi ni njia ya kuwa kiongozi bila kudhibiti washiriki kikamilifu, na kuwasaidia washiriki kusoma ili wajiundie uelewa wa masuala. Mkufunzi anapaswa kutayarisha

vikao mapema na kuongoza mafunzo na mchakato katika warsha au kikao cha ukufunzi. Mafunzo ambayo utapitia yatajumuisha shughuli, mada na masuala ambayo ungependa kujadili. “Mchakato” ni jinsi ambavyo mafunzo yanatolewa na kujadiliwa katika kikao, ikiwa ni pamoja na mbinu, ufuatiliaji, muundo, zana, mtindo wa mwingiliano na masuala mbalimbali ya kikundi.

VIDOKEZO VIKUU

Vidokezo kumi vya jinsi ya kuwa mkufunzi bora

1. Jiandae mapema: Jifahamishe kuhusu mwongozo wa mkufunzi ili upate ujasiri katika mafunzo, muda na mchakato utakaotumia. Jiweke katika hali ya washiriki wako na uunde maswali ambayo wanaweza kuuliza, au wasiwasi ambao wanaweza kukujulisha. Kama huelewi baadhi ya mambo kwenye kitabu au mada, uliza watu ambao wana ujuzi.
2. Panga wakati wako: Kama itakubidi, mwombe mshirika mmoja akusaidie kufuatilia wakati uliopangiwa kutumika katika kila sehemu ya kikao, na akuarifu wakati wowote umetumia muda zaidi kuliko uliopangiwa au pale ambapo utahitajika kukamilisha sehemu fulani haraka.
3. Chati na kalamu za alama: Hakikisha umezitayarisha na uwe na mtu wa kukusaidia kuainisha hoja utakazozungumzia. Kufanya hivyo kutakusaidia kuwa na muhtasari wa mjadala na kurudia hoja fulani baadaye.
4. Ainisha kusudi la ukufunzi: kubaliana na washiriki kutoka mwanzo wa mafunzo kuhusu kusudi la mikutano yenu na malengo yenu.
5. Jifahamishe na washiriki wako nao pia wapate kukujua: Kujitambulisha kwao na kuwapa fursa ya kujitambulisha mwanzoni mwa mafunzo kutasaidia kuandaa mazingira yaliyo tulivu na salama. pahala Kuruhusu majadiliano ya pamoja ni hatua muhimu ya kuwezesha washiriki kujifunza na kuwa na mfumo wa kusaidiana.
6. Usiegemeo upande fulani, sikiliza: Ni sawa kuzungumzia mitazamo yako binafsi pamoja na uliyoyapitia mwenyewe maishani, lakini usiwalazimishe washiriki kufuata mitazamo hii. Hakikisha kila mmoja anashiriki kwa mijadala na anajisikia huru kuzungumza. Ikiwa mshirika anazungumzia mambo ambayo hayako kwenye mada au mambo nyeti, mjulishe kwamba umewasikiza na mtajadili mambo hayo baada ya kikao.
7. Andaa mazingira salama ambayo yanasimua na kuelimisha: Sote tunashiriki katika mchakato wa mafunzo. Wasaidie vijana kuelewa shughuli mbalimbali mtakayochambua kwa njia rahisi, ya kujali na ya kusisimua.
8. Himiza majadiliano: Ni wajibu wako kuendeleza mjadala. Tayarisha maswali na majibu kabla ya vikao ili kuhimiza mazungumzo na maoni pamoja na washiriki.
9. Kama hujui jibu la swali fulani, litafute kwenye nyenzo zilizo: Kuwa mkweli na wazi maana nyote mko hapo kujifunza pamoja. Waulize wengine kwenye kikundi, au urudie hoja hilo baada ya kutafti jibu sahihi.
10. Fanya muhtasari na uainishe hatua zitakazofuata: Hakikisha umeainisha mambo yote mliyojifunza na kukamilisha katika kikao, na upitie shughuli zozote ambazo zitahitaji kukamilishwa na kikundi pamoja na wale waliowajibika kuhakikisha kwamba shughuli hizi zimekamilishwa. Mfumo huu utakusaidia kufikia matokeo mazuri.



Ni jukumu na wajibu wako kama mkufunzi kuwasilisha mafunzo na shughuli katika kikao kwa njia rahisi iwezekanavyo, ili wote waelewe na waweze kufuata shughuli kwa urahisi.

Ninawezaje kuwa mkufunzi bora?

Ni jukumu na wajibu wako kama mkufunzi kuwasilisha mafunzo na shughuli katika kikao kwa njia rahisi iwezekanavyo, ili wote waelewe na waweze kufuata shughuli kwa urahisi. Mkufunzi pia ana wajibu wa pahalakuandaa mazingira yaliyo huru na salama ya kufanyia mafunzo kwa wote kwenye kikundi.

Ungependa kufanya kazi na nani?

Vijana ambao utashirikisha kwenye vikao vyako wanafaa kuwa wale ambao wameonesha hamu au walio na uzoefu wa kufanya kampeni zinazohusu kuozwa kwa watoto katika jamii zao. Tunapendekeza

kwamba katika kila kikao, ushirikishe vijana wenye umri wa kati ya 10 na 24 ili kuwezesha usimamizi bora. Kikundi kikubwa zaidi kinaweza kuwa changamoto kusimamia vyema na pia kinaweza kukosa muda wa kujadili hoja kwa kina. Baadhi ya washiriki wanaweza kupendelea kuwa kwenye vikundi na wengine wa umri au jinsia yao, ili wajisikie huru wanapozungumzia masuala nyeti au magumu. Tunapendekeza ufikirie kwa uangalifu kuhusu jinsi utawagawanya washiriki katika vikundi wanapoendeleza shughuli kwenye vikundi vidogo, kulingana na misingi yao, ili wajiamini na wajihisi huru kushiriki.

VIDOKEZO VIKUU

Kufanya kazi na vikundi vyenye mchanganyiko wa vijana wa kike na wa kiume

Unapofanya kazi na kikundi kilichochanganywa, fikiria kuhusu masuala kadhaa hapo awali.

- Fikiria kuhusu mienendo ya kijinsia katika kikundi chako. Kulingana na mada, inaweza kuwa bora kugawanya kikundi cha jumla ili kiwe vikundi vidogo tofauti vya washiriki wa kiume na wa kike ikiwa watajisikia huru zaidi wakati wanafanya shughuli za kikundi zinazohusu mada zenye changamoto zaidi.
- Kumbuka kwamba watu hujifunza kwa njia tofauti. Mipango ya vikao hutumia njia nyingi tofauti kuzungumzia masuala kuu na tumejumuisha shughuli na majukumu anuwai za watu kufanya. Unapoendelea kuwafahamu washiriki wa kikundi chako, endesha vikao kulingana na kile kinachowafaa zaidi na kinachowafanya washiriki na wachangamke.
- Kila mara, fuatilia kikundi chako! Njia moja ya kusaidia washiriki kujifunza katika vikao vyako na kuwafuatilia ili kuhakikisha kuwa wanaelewa ni kurudia na kufupisha hoja muhimu ili zibaki kwenye akili zao. Uliza maswali ya kawaida, kama vile "nikumbushe sababu za kiini za kuozwa kwa watoto" na kisha usaidie kikundi kipitie hoja tena pamoja.
- Kumbuka kwamba washiriki hawatakubaliana katika hoja zote mtakazozungumzia na hiyo ni sawa. Usijali - kuzungumza kuhusu mambo, ikiwa ni pamoja na majadiliano magumu ambapo watu hawakubaliani, huboresha mazungumzo kwani inasaidia washiriki kuelewa maoni magumu na kuwezesha mitazamo na maoni mbalimbali. Mwanzoni mwa mafunzo yako, saidia washiriki kukubaliana na sheria kadhaa za msingi ambazo kila mtu atawajibika kuzingatia. Hizi zinaweza kujumuisha vidokezo kama "kila mtu atawasikiliza wenzake na kushiriki, kwa hivyo heshimianeni. "Wakumbushe sheria ikiwa hawazitii na wanapoanza kusababisha mivutano katika kikundi.
- Jenga mienendo dhabiti kwenye kikundi ili washiriki wahisi wapo ndani ya timu na ili watake kushiriki na kufanya kazi pamoja. Unaweza kuhamasisha wengine kusaidia kuongoza baadhi ya vifungu vya vikao pamoja na wewe, inapofaa, kwani hii inaweza kuimarisha umiliki na maelewano katika kikundi.

Kufanya kazi na wasichana walioathiriwa na kuozwa kwa watoto

Ikiwa unapanga kufanya kazi na wasichana walioolewa au vijana wa kike ambao wamepitia kuozwa wakiwa watoto, basi mchakato nyeti ni muhimu. Fikiria kwa umakini kuhusu haya na uunde pahala salama kwa wanawake na wasichana hawa. Haya ni baadhi ya mambo ya kufikiria.

- Mshiriki yeyote aliye chini ya umri wa miaka 18 anahitaji kupata idhini ya kujiunga na masomo ili kuhakikisha ulinzi wa watoto, kwa hivyo utahitaji kuthibitisha kutoka kwa wazazi wao kwamba kujiunga na kikundi chako ni sawa. Thibitisha ikiwa wanawake au wasichana walioolewa wanahitaji ruhusa kutoka kwa mtu mzima ili kujiunga na shughuli zako; wengine wanaweza kuhitaji ruhusa kutoka kwa mume au mama mkwe kujiunga. Hakikisha wanawake na wasichana wote wanajua kuwa kushiriki ni kwa hiari na kwamba hawatalazimishwa kujadili waliyopitia kibinafsi ikiwa hawataki.
- Hakikisha unatambua mitazamo kuhusu wasichana walioolewa katika jamii ambapo unafanyia kazi na mitazamo kuhusu ushiriki wao katika shughuli kama hizi. Ikiwa wataamua kujadili mambo ya kibinafsi katika kikundi, basi ni muhimu uwahakikishie pahala salama pa kushiriki.
- Tafuta nyakati zinazowafaa zaidi. Wasichana walioolewa wanaweza kuwa na watoto na wanahitaji kuwa nyumbani kwa nyakati maalum za siku, kwa hivyo zingatia haya unapopanga vikao vyako.
- Hakikisha kuwa mkufunzi wa kike anafanya kazi na kikundi chochote cha wasichana walioolewa. Utahitaji kujua utawaelekeza kwa nani katika jamii ikiwa washiriki wangetaka kuzungumzia masuala ya unyanyasaji, au wanapokasirishwa na masuala yoyote yanayozungumziwa. Mtu

huyu anaweza kuwa mfanyakazi katika nyanja za ulinzi wa watoto kwenye jamii au mfanyakazi wa kijamii, mtaalamu wa huduma za afya au mtu kutoka shirika la wanawake la eneo hilo, lakini ni muhimu kuhakikisha watapatikana kusaidia wakati wowote utakapowahitaji.

Nifanye nini kabla ya kuanza mafunzo?

1. Kabla ya kuanza mafunzo yoyote unapaswa kuzungumza na watu wanaofaa kutambulishwa katika jamii yako au wale ambao ni waamuzi ili wafahamu mipango yako. Hawa ni pamoja na watu muhimu, kama viongozi wa eneo au walimu ambao wana uwezo na ushawishi katika jamii na ambao wanaweza kusimamisha au kudhibiti mafunzo yako, au vinginevyo kuunga mkono kazi yako. Eleza kwa heshima kile unachotaka kufanya, na ikiwa kuna pingamizi zozote tafuta pahala au wakati mbadala, lakini fanya bidii kupata usaidizi wao.
2. Hakikisha una angalau saa kadhaa kabla ya kikao chako kuandaa vizuri jinsi utakavyoendeleza na kuongoza masomo. Unaweza kutaka usaidizi katika jukumu lako la mkufunzi kwenye vikao vingine kutoka kwa wengine unaofanya kazi pamoja nao katika shirika lako, ili uweze kushiriki uongozi wa shughuli. Ikiwa utashiriki jukumu hili, utahitaji kujiandaa kwa pamoja na mkufunzi mwenzako.
3. Fikiria kuhusu masuala halisi kama vile pahala pa kuandaa vikao na wakati utakapoandaa mafunzo yako: ni muhimu kwamba mahitaji haya yawe rahisi kupatikana, salama na yapendelewe na washiriki wako ili kukidhi mahitaji yao. Ikiwa pahala hapo ni wazi au pa umma, basi hakikisha kupunguza usumbufu (kama vile kelele, hali ya hewa isiyofaa au mambo yanayopotosha). Fikiria ikiwa utahitaji eneo lisilo rasmi - kama vile kwenye mbuga au bustani au kwenye kilabu cha vijana - au eneo rasmi, kama vile shule. Hakikisha ni pahala salama kwa vijana (ikiwa ni pamoja na wasichana) kufikia, na kwamba watajisikia salama na huru kuwa hapo.

Fikiria kuhusu mahitaji ya lugha. Huenda ukahitaji kumwalika mtafsiri, au kutafsiri nyenzo unazotumia katika lugha ambayo inayoeleweka vyema kwa jamii hiyo ili kuhakikisha washiriki wana starehe wakijieleza.

Nijibu masuala vipi?

Kuozwa kwa watoto ni mada nyeti na ambayo inaweza kuwa ngumu kuzungumzia kwa baadhi ya watu. Wakati mwingine, tofauti za maoni zinaweza kutokea, na kunaweza kuwa na hali ngumu au maoni yenye changamoto ambayo hujitokeza kwenye mazungumzo. Tazama majibu haya ambayo unaweza kutumia katika vikundi vyako ikiwa hali hizi ngumu zitatokea.

- *Asante kwa kushiriki maoni yako nasi. Je, unaweza kutueleza ni kwa nini unahisi hivi? Tafadhali jaribu pia kuelewa kuwa sio kila mtu ana maoni sawa na yako.*
- *Ikiwa ungependa kujadili hili zaidi, itakuwa furaha yangu kuketi na wewe baada ya kikao kuzungumza kuhusu suala hili, au kukutambulisha kwa watu ambao wana ujuzi zaidi kuhusu suala hili.*

Kumbuka, usiruhusu maoni yoyote yanayoweza kudhuru yaachwe yapite bila kupingwa au kufafanuliwa. Kwa mfano, baadhi ya washiriki wakisema kuwa ni sawa kwa wasichana kuozwa wakiwa na umri mdogo kuliko wavulana. Unaweza kupinga kwa kujibu:

- *Asante kwa kueleza maoni yako. Je, nyinyi wengine mnafikiria vipi? Nani hapa ana maoni tofauti?.*

Ikiwa maoni mbadala hayatatolewa, basi hakikisha unatoa maoni hayo. Ukiweza, tumia maarifa na ushahidi kwenye nyenzo hii kujadili hoja yako. Kwa mfano unaweza jibu:

- *Ninajua watu wengi ambao hawatakubaliana na maoni haya. Ukweli ni kwamba sheria ya kimataifa inasema kwamba wasichana hawapaswi kuolewa wakiwa chini ya umri wa miaka 18 kwa sababu ya athari nyingi mbaya ambazo zinaweza kutokea. Hii ni haki ya kibinadamu ya kila mtu.*

Kuongoza kikao chako:

1. Soma mwongozo wako wa ukufunzi kwanza

Katika mwongozo wa mkufunzi Simama, Sikika!, katika sehemu inayoitwa Mwongozo wako wa ukufunzi ndipo tutapitia hatua kwa hatua kila shughuli katika kikao na kuelezea ni nini hasa unahitaji kukamilisha na kikundi chako. Tunatoa muhtasari na kuelezea shughuli zote, haswa mambo kama shughuli za kustarehesha ambazo tunashauri utumie katika vikao vyako vya mafunzo. Pia tunapitia kwa undani mafunzo na maelezo yaliyomo ambayo utahitaji kujua ili kuwasilisha kwa vikundi vyako. Soma haya kwa uangalifu na ujiozeze kila shughuli ili ujisikie jasiri katika jukumu lako kama mkufunzi wa kikundi chako.

2. Tahadhari ya masuala nyeti na ulinzi

Peana onyo hili mwanzoni mwa kila kikao. Ni muhimu kuanza kila kikao kwa kupeana tahadhari ya masuala nyeti na onyo la umuhimu wa ulinzi. Unahitaji kufanya hivyo hata ikiwa washiriki wana umri wa zaidi ya miaka 18. Ni muhimu kuelezea hoja hizi tatu zinazofuata.

- Wajulishe washiriki kuwa kuoza kwa watoto ni mada nyeti inayoweza kuwakasirisha baadhi ya washiriki. Eleza kwamba ikiwa yeyote hukasirika na anataka kuondoka, basi anaweza kufanya hivyo wakati wowote. Hakikisha pia washiriki wanajua ni nani wanaweza kuenda ili kupata msaada zaidi.
- Hakikishia kila mshirika kuwa chochote kitakachosemwa kwenye kikundi ni cha siri na kwamba pahala hapo ni salama kuzungumza na kujadiliana. Eleza kwamba hakuna mtu atalazimishwa kueleza mambo ya kibinafsi wakati wowote na kwamba kushiriki kwa majadiliano ni kwa hiari.
- Eleza kuwa kudumisha tahadhari unapozungumzia masuala nyeti na unapolinda watoto ni jukumu la kila mtu

katika kikundi. Sisi sote tunaheshimu michango ya wengine na hatuhukumu watu wanapozungumzia masuala yoyote ya kibinafsi.

Ni muhimu pia kutambua mtu anayeaminika katika jamii yako ambaye ana ujuzi wa kutoa msaada wa kihemko na kiutendaji kwa vijana wowote ambao wanaweza kukasirika au wanaofichua dhuluma walizopitia unapoendeleza vikao. Mtu huyo anaweza kuwa mfanyakazi wa afya, mwanachama wa kikundi cha wanawake, mfanyakazi katika nyanja za ulinzi wa watoto au mwalimu anayeaminika. Sio lazima mtu huyo awe kwenye mafunzo unayoendeleza, lakini anapaswa kupatikana baada ya vikao ili kufuatilia na kuwasaidia washiriki.

Ni muhimu kuanza kila kikao kwa kutahadharisha washiriki kuhusu unyeti wa mazungumzo na kwa kuwapa onyo la kulinda washiriki wote - hata ikiwa washiriki wamezidi umri wa miaka 18. Tunapendekeza utumie *Sera ya Kulinda Watoto ya Girls Not Brides* kama msingi wa kanuni zako za ulinzi katika vikao vyako. Andika onyo la ulinzi kwenye kipande cha chati, uwe nayo kama slaidi ya uwasilishaji ambayo unaweza kuwakumbusha washiriki katika kila kikao, au uibandike kwenye ukuta ili kila mmoja aweze kuirejelea.

Ni muhimu kuanza kila kikao kwa kupeana tahadhari ya masuala nyeti na ulinzi. Unahitaji kufanya hivyo hata ikiwa washiriki wana umri wa zaidi ya miaka 18.

3. Kuweka kanuni za msingi na kikundi chako

Fanya hivi mwanzoni mwa Moduli ya 1, Kikao 1 na ukumbushe kikundi kila wakati mnapokutana. Ni muhimu kila mshiriki katika vikao vyako vya mafunzo ahisi kuwa ni sehemu muhimu ya kikundi, na kwamba anaweza kusaidia kudumisha mienendo ya kikundi na utaratibu. Kila mtu anahitaji kuwa na jukumu la kusaidia ikiwa yeyote atasababisha vurugu yoyote na wote wanahitaji kuwajibika kila mmoja kwa mwingine ili kukamilisha mafunzo kwa umoja. Kuweka sheria rahisi ambazo wanachagua wenyewe ni njia muhimu ya kuwawezesha kutunza mienendo ya kikundi na kuhakikisha kila mtu anafikia malengo yake.

Ni muhimu kila mtu katika vikao vyako vya mafunzo ajihisi kuwa sehemu muhimu ya kikundi, na kuwa anaweza kusaidia kudumisha mienendo na utaratibu wa kikundi.

Kwa mfano, ‘simu haziruhusiwi’ ni kanuni nzuri, ili watu wasipoteze umakini kwa sababu ya jumbe za maandishi au kupigiwa simu, ambazo huleta kelele kwa watu wengine katika kikao. Kuzingatia wakati ni muhimu pia. Kumpatia mtu mmoja katika kikundi jukumu la kuwa mtunza-muda ni njia nzuri ya washiriki kuwajibika kutumia wakati uliotengewa shughuli, na kuhakikisha kuwa mtu hazungumzi zaidi ya wengine. Kanuni moja muhimu ni kwamba sauti ya kila mtu ni sawa na kwamba pahala pa mafunzo ni pahala salama na kwa hivyo lazima waheshimiane, hata ikiwa tofauti za maoni zitatokea. Kuheshimiana ni jambo muhimu sana la kuzingatia ili kila mtu aweze kuelewa.

Amueni kuhusu sheria pamoja kama kikundi na uziandike kwenye karatasi ambayo utabandika ukutani kama ukumbusho wa kila wakati. Zirejeele mwanzoni mwa kila kikao ili washirika wakumbuke jinsi wanataka kufanya kazi pamoja kama kikundi. Ikiwa mtu atavunja sheria, au hajafuata kanuni hizi, kuwa nazo kwenye ukuta ni muhimu ili uzirejeele tena na kumuuliza aheshimu sheria ambazo watu wote waliweka pamoja.

4. Kuendesha kikao chako: jukumu lako la kujenga ujasiri

Vijana wengine wanaweza kuchukua muda kuchangamana na wengine na kushiriki kikamilifu, kwani wanaweza kuhisi haya au labda hawajazoea warsha kama hizi. Unaweza kuunda shughuli za kusisimua ambazo zinalenga ‘kuvunja barafu’ kati ya watu ili kuwasaidia kujuana na kushikamana. Shughuli hizi ni njia fupi na za kufurahisha zinazojenga ujasiri, kusaidia kazi ya timu na kuongeza viwango vya nguvu kwenye kikundi. Hazipaswi kuwa zaidi ya dakika 5 hadi 10. Tumependekeza shughuli tofauti katika sehemu mbalimbali za mwongozo wa mafunzo.

5. Kuendesha kikao chako... hadi mwisho

Nafasi ya maegesho

Eleza haya mwanzoni mwa kila kikao, na ufanye hivyo hadi mwishoni.

Unapomaliza kila kikao, ni vyema kuwauliza washiriki waeleze yale waliyofunza katika kikao, au vidokezo vyovyote au majadiliano ambayo yameibua mawazo fulani au kufungua akili zao. Ikiwa washiriki wanaibua hoja au maswali ambayo huwezi au huna wakati wa kuyashughulikia moja kwa moja, unaweza kuyaandika kwenye karatasi ya chati ambayo kila mtu anaweza kuona, ili uweze kuirejeele mwishoni mwa kikao au warsha. Unaweza kuiita ‘nafasi ya maegesho’, ‘friji’ au ‘ghala’. Haya ni mazoea mazuri ya kuhakikisha kuwa hakuna mtu aliye na maswali ambayo hayajajibiwa au masuala ambayo wanatamani kushiriki.



Picha © Jessica Podraza/ Unsplash



Moduli 1: **Kuozwa kwa** **watoto ni nini?** **Mambo ya Msingi**

Muhtasari wa moduli

- • Kufahamiana na kutambua jinsi ya kufanya kazi pamoja.
- • Kuozwa kwa watoto ni nini na inasababishwa na nini?
- • Je, athari za kuozwa kwa watoto ni zipi?
- • Tunawezaje kuizuia?

Moduli 1 - Kikao 1

Tufanye kazi pamoja



Lengo

Kufahamiana na kujenga uhusiano wenye furaha, salama na wa kuaminika.



Idadi ya washiriki:
Chini ya 24



Wakati unaohitajika:
Saa 1



Muhtasari wa kikao

- Kutambulisha washiriki
- Muhtasari wa Moduli: Masuala makuu yatakayokamilishwa katika vikao vijavyo vya mafunzo
- Madhumuni: matumaini yako na wasiwasi kuhusu mafunzo
- Tahadhari ya Ulinzi wa watoto
- Weka kanuni za msingi



Vitu vya kuandaa mapema

- Shughuli za vikundi: andaa picha
- Slaidi za uwasilishaji (za kielektroniki au kwenye karatasi ya chati)



Vifaa vinavyohitajika

- Picha za rangi kutoka kwa majarida
- Makasi
- Karatasi za chati
- Kalamu za alama au kalamu nene
- Bakuli au kikapu cha kutumia kwa shughuli ya picha

Shughuli	Wakati uliotengwa	Muhtasari
1	Dakika 10	Utangulizi
2	Dakika 15	Kazi ya vikundi: Kutambulisha washiriki na kwa nini mafunzo haya
3	Dakika 10	Uwasilishaji wa mkufunzi: Utangulizi wa masuala ambayo utashughulikia
4	Dakika 10	Kazi ya vikundi: Matarajio na madhumuni
5	Dakika 10	Kazi ya vikundi: Kuunda kanuni za kufanya kazi pamoja
6	Dakika 5	Kufunga kikao: Makumbusho ya hatua zitakazofuata

1.1 Mwongozo wako wa ukufunzi

Katika mwongozo huu, sehemu inayoitwa ‘Mwongozo wako wa ukufunzi’ ni mahali ambapo tunapitia kila shughuli katika kikao hatua kwa hatua na kueleza ni nini haswa unahitaji kukamilisha na kikundi chako. Tunatoa muhtasari na kueleza shughuli zote, haswa shughuli kama vile “kuvunja barafu” ambazo tunashauri uweze kutumia katika vikao vyako vya mafunzo. Pia tunapitia kwa undani habari na mafunzo unayohitaji kujua ili kuwasilisha kwa vikundi vyako. Soma sehemu hizi kwa uangalifu na ujioze kila shughuli ili ujisikie jasiri wakati uko katika jukumu lako kama mkufunzi wa kikundi chako.

Shughuli 1: Utangulizi

Anza kwa kutembea kati ya kikundi na kuuliza kila mtu ajitambulishe: waeleze waseme majina yao na jambo moja la kuchekesha kuwahusu ambalo watu wengine hawajui. Hakikisha kila mtu ana lebo ya majina yake ili wote waweze kufahamiana na kujua majina ya wengine.

Kuweka washiriki wako katika vikundi

Jiandae mapema

- Chagua picha nne za kupendeza kutoka kwenye jarida: kata kila picha kwa vipande sita na uvikunje kabla ya kikao. Weka vipande hivi vilivyokunjwa kwenye bakuli.
- Gawanya jumla ya washiriki wa kikao katika vikundi sawa: ikiwa idadi yao ni 24, wagawanye katika vikundi vinne vya watu sita. Au unaweza kutaka vikundi vidogo, kama vile vikundi sita vya watu wanne.
- Utahitaji picha nyingi kadiri ya vikundi, kila moja ikikatwa kwa idadi sawa ya vipande kama idadi katika kila kikundi. Vikundi vitano = picha tano, watu watatu katika kila kikundi = vipande vitatu kwa kila picha, ili waweze kukutana na kurudisha picha yao pamoja.

Katika kikao

- Waombe washiriki wachukue kipande cha karatasi kilichokunjwa kutoka kwenye bakuli.
- Waambie washiriki wafungue kipande cha karatasi kilichokunjwa na wajaribu kutafuta washiriki wengine tano (au idadi yoyote ya kikundi) ambao wana vipande vitakavyofaa kutengeneza picha nzima.
- Mara tu wanapopata wenzao wanapaswa kuunda kikundi. Baada ya kuunda kikundi chao, waulize wakusanye karatasi ya chati na kalamu ya alama.

Zoezi la utangulizi linaweza kufupishwa, au kuachwa ikiwa huna wakati wa kutosha. Ili kuharakisha mambo, washiriki wanaweza kujitambulisha kwa kusema majina yao na jambo moja wanalopenda kuhusu jamii yao.



Shughuli 2: Kazi ya vikundi - Kufahamiana zaidi

Elezea kikundi maagizo yafuatayo kuhusu kazi ya kikundi ifuatayo.

Katika vikundi vyao vipya, washiriki wote watakusanyika mezani pamoja, watajitambulisha na kuandika majina yao kwenye karatasi ya chati. Wanapaswa kuchagua mtu mmoja kuwa mwandishi wa hoja ambaye atashirikisha mazungumzo kwa kikundi cha jumla mwishoni. Kila mshiriki anapaswa kueleza wenzake:

- a) Sababu moja amekuja kwenye mafunzo, au sababu moja anataka kufanya kazi kushughulikia kuozwa kwa watoto.
- b) Jambo moja anapenda kuhusu jamii au shule yake.

Anayeandika hoja anapaswa kuandika majibu aliyopewa na kila mtu chini ya jina lake kwenye chati na kuiweka ukutani. Wana dakika 10 kupitia majibu haya pamoja na kisha watashirikisha tena kwa kikundi cha jumla. Baada ya kumaliza, yule anayeandika hoja kutoka kwa kila kikundi atawatambulisha wenzake wa kikundi kwa kusoma chati ambazo zimewekwa ukutani ili waweze kujifunza kuhusu kila mmoja na kutambua masilahi ambayo inafanana kati yao. Wana dakika 5 tu za wote kuwasilisha, kwa hivyo waeleze wanahitaji kuwasilisha kwa ufupi. Fuatilia muda shughuli hii inapoendelea.

Shukuru kila mtu kwa kushiriki, na uwaambie jinsi unavyofurahia kufanya kazi pamoja na kikundi hiki chenye bidii na shauku.



Shughuli 3: Uwasilishaji wa mkufunzi - Utangulizi wa masuala utakayoshughulikia

Kile utakachohitaji kuandaa mapema:

- Kipande kimoja cha karatasi ya chati lenye onyo la unyeti na ulinzi wa watoto - ambacho unaweza kubandika kwenye ukuta.
- Ukurasa mmoja ukutani ambao unaitwa 'nafasi ya maegesho' kwa maoni au masuala kuandikwa unapoendelea na mafunzo.

Malengo makuu ya mafunzo kwa ujumla

Katika kikao hiki, mkufunzi anaeleza washiriki lengo kuu na madhumuni ya mafunzo - kwamba sisi sote tuko pamoja kuzungumzia jinsi ya kukomesha kuozwa kwa watoto na jinsi ya kuwezesha uanaharakati katika kuikomesha. Waeleze kuwa mafunzo haya yatawasaidia kuwa wanaharakati hodari, wenye ujuzi kuhusu sababu za kuozwa kwa watoto na jinsi ya kufanya kazi ili kuizuia. Mafunzo haya yatawasaidia kuimarisha ujuzi wao kuhusu kufanya kazi kukomesha kuozwa kwa watoto, kwa kuelezea jinsi ya kupanga uanaharakati wao, jinsi ya kuunda mikakati, na jinsi ya kufuatilia athari na ushahidi wa kuimarisha kazi zao. Elezea kikundi mada kuu ambazo utakuwa ukichunguza pamoja nao katika vikao vichache vijavyo na madhumuni makuu ya mafunzo - haya yameainishwa hapo awali katika mwongozo huu, lakini kwa ufupi:

- Kuozwa kwa watoto ni nini na hufanyika kwa nini.
- Athari na matokeo ya kuozwa kwa watoto.
- Njia za kuzuia kuozwa kwa watoto: jinsi ya kuwezesha uanaharakati kuleta mabadiliko.
- Njia za kukusanya ushahidi kuonesha athari ya kazi yako na jinsi mambo yanaweza kubadilika.

Tahadhari ya masuala nyeti na kuwalinda watoto

Katika sehemu hii, utaelezea pia tahadhari ya masuala nyeti na kuwalinda watoto (angalia sehemu ya awali kuhusu kanuni hizi za ulinzi). Kuwa tayari umeziandika kwenye karatasi ya chati unayobandika kwenye ukuta wakati wote wa warsha, kama ukumbusho wa kile mnachotaka kufikia hapa pamoja, na viwango vya msingi vya ulinzi ambavyo nyote mnahitaji kutimiza.

Uliza kikundi ikiwa wanahisi kuna mada zinazokosekana ambazo wangependa kujadili kama sehemu ya mafunzo. Ziandike kwenye karatasi ya chati ambayo unaita 'nafasi ya maegesho' - ambayo utaendelea kuiongezea kikao kinapoendelea. Hii ni nafasi tupu ambayo unaweza kutumia kuweka maoni, mapendekezo na maswali ambayo yatajitokeza kwenye warsha ambayo mtashughulikia mwishoni pamoja, au ambayo itakusaidia kuandaa vikao vyako vya siku zijazo ili kutosheleza mahitaji na maombi ya kikundi.

Shughuli 4: Kazi ya vikundi - Matarajio na madhumuni

Eleza kikundi shughuli inayofuata ambayo wote watafanya pamoja.

Washiriki watabaki katika vikundi vile vile ambavyo viliundwa awali katika sehemu ya utangulizi, lakini waulize wachague mwandishi wa hoja tofauti. Wape kila kikundi karatasi ya chati, na uwaulize kama kikundi waandike mambo mawili wanayotarajia kutoka kwa mafunzo (nini wanatarajia kupata kama sehemu ya warsha au kile wanachotaka kujifunza). Wanaweza pia kutaja ikiwa wana wasiwasi wowote kuhusu mafunzo au kuhusu suala lenyewe ambalo mnashughulikia. Waeleze waandike haya kwenye karatasi hiyo na kila kikundi kiwasilishe matokeo kuu kwa ufupi. Ni muhimu sana kufanya hivi mwanzoni, kwani hii itakusaidia kushughulikia matarajio yoyote yasiyoweza kufikiwa na kupunguza kutokuelewana.



KUMBUKA

Ikiwa unahisi kuwa kikao hiki kinachukua muda mwingi, kinaweza kugeuzwa kuwa kipindi kifupi cha jumla ambapo washiriki wote wanaweza kushiriki matumaini na wasiwasi wao kwa pamoja, ambazo unaweza kuandika kwenye karatasi, badala ya kuwa na vikundi vidogo vinavyojadili na kushiriki.









Shughuli 5: Kazi ya vikundi - Kuweka kanuni za kufanya kazi pamoja

Ni muhimu washiriki waweke sheria za msingi za kufanya kazi pamoja, kwani kuweka sheria za msingi za shughuli ni muhimu kuhakikisha mazingira ya starehe. Vikao vya mafunzo vinaweza kuvurugwa ikiwa sheria za msingi hazitawekwa mwanzoni. Ikiwa hizi zimewekwa na washiriki wenyewe, watahisi umiliki kuhusu mchakato, na kutakuwa na uwezekano mkubwa zaidi kwamba watazingatia sheria. Ikiwa watakuwa wamesahau kutaja sheria kadhaa, jisikie huru kuzishirikisha kwao, kama vile: fika kwenye warsha kwa wakati unaofaa, usizungumze na wengine wakati mtu anazungumza au anapowasilisha, kuhakikisha kila mtu anamheshimu mwenzake na anawasikiliza wengine, na kuhakikisha kuwa washiriki hawatamii simu zao za rununu kwenye warsha. Kuna miongozo mingine mingi rahisi ambayo inasaidia kila mtu kuheshimiana na kuhakikisha pahala salama pa kufanyia kazi za warsha - angalia sehemu ya "Jitayarishe Kuanza" kwa mifano zaidi.

Moduli 1 - Kikao 2

Kuozwa kwa watoto ni nini? Utangulizi

 <p>Lengo</p> <p>Kusaidia washiriki kuelewa ufafanuzi wa kuozwa kwa watoto, jinsi kunavyosababishwa, na mambo yanayokithirisha suala lenyewe</p>  <p>Idadi ya washiriki: Chini ya 24</p>	 <p>Muhtasari wa kikao</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kujadiliana kuhusu kuozwa kwa watoto na kuelewa kile washiriki wanajua kuhusu suala hilo • Utangulizi wa suala hili: misingi wa kuozwa kwa watoto  <p>Wakati unaohitajika: Saa 1 Dakika 30</p>	 <p>Vitu vya kuandaa mapema</p> <ul style="list-style-type: none"> • Soma Maelezo ya Usuli kwenye ukurasa 30 na uyaelewe vizuri ili ujisikie jasiri kuwasilisha kwa kikundi cha jumla. • Slaidi za uwasilishaji (za kielektroniki au kwenye karatasi ya chati) zenye hoja muhimu kuhusu kuozwa kwa watoto ili uweze kuzirejelea na kuwezesha kikundi kusoma na kufuata • Fanya mazoezi ya shughuli ya kuisimua kama utafanya pamoja na kikundi 	 <p>Vifaa vinavyohitajika</p> <ul style="list-style-type: none"> • Karatasi za chati • Kalamu za alama au kalamu nene • Slaidi za mawasilisho
--	--	---	--

Shughuli	Wakati uliotengwa	Muhtasari
1	Dakika 5	Karibu • Makumbusho na utangulizi (ikiwa ni kikao cha pekee)
2	Dakika 35	Kazi ya vikundi: Kufafanua kuozwa kwa watoto • Majadiliano ya wazi (dk 10) • Kazi ya vikundi (dk 15) • Mawasilisho ya vikundi (dk 10)
3	Dakika 10	Uwasilishaji wa mkufunzi: Mafunzo ya msingi- kuozwa kwa watoto
4	Dakika 20	Kazi ya vikundi: Sababu za kuozwa kwa watoto katika jamii yako
5	Dakika 15	Uwasilishaji wa mkufunzi: Sababu za kuozwa kwa watoto
6	Dakika 5	Wakati wa maswali na hitimisho

1.2 Mwongozo wako wa mkufunzi

Shughuli 1: Karibu

Karibisha kikundi chako pamoja tena. Ikiwa unafanya kikao hiki peke yake (baada ya siku moja au wiki moja baada ya kikao cha kwanza) basi mwombe kila mshiriki ajitambulisha tena ili wote wakumbuke majina ya wengine. Wakumbushe sababu ya kuwa pamoja - kwamba sisi sote tuko hapa kujifunza na kushiriki kuhusu kuozwa kwa watoto na jinsi ya kuwa wanaharakati shupavu wa kukomesha utamaduni huu. Tunapendekeza pia upitie haraka ukumbusho wa sheria za msingi mlizoweka pamoja, na pia ukumbusho wa tahadhari ya masuala nyeti tena. Eleza kikundi kuwa katika kikao hiki tutakuwa tunajifunza na kufafanua kuozwa kwa watoto pamoja.

Shughuli ya kulisimua

Shughuli 'Ngurumo' imebuniwa kuwachangamsha washiriki wote. Uliza kila mtu asimame kwenye duara (au tu mahali alipo kwenye chumba, lakini hakikisha kuna nafasi ya kutosha kwa kila mtu kutembea chumbani). Eleza kwamba watafanya vitendo vifuatavyo vya kuigiza utakapoita maneno yafuatayo:

- **Mvua:** gonga mikono yako yote juu ya mapaja yako haraka na kwa mfululizo.
- **Ngurumo:** gonga sakafu na miguu yako kwa mfululizo (mguu mmoja kisha mwingine).
- **Radi:** nyoosha mikono yote miwili ukihakikisha mkono wa kulia umeelekezwa juu (upande wa kaskazini-mashariki) na mkono wa kushoto umeelekezwa chini (upande kusini-magharibi)

Onyesha mwendo wa kila neno unapoliita.

Kisha waombe washiriki wafanye vitendo hivyo pamoja kama mazoezi.

Sasa unaweza kuanza. Taja maneno na uulize kikundi kifanye vitendo vinavyofaa wakati unapoita neno fulani; kwanza kwa utaratibu ulioonyeshwa hapo juu na kisha anza kuchanganya utaratibu wa maneno. Endelea kuita maneno tofauti haraka na haraka zaidi - utaanza kuona kila mtu akichanganyikiwa na kucheka!



KUMBUKA

Ikiwa unaendesha kikao hiki moja kwa moja baada ya **Moduli ya 1: Kikao cha 1 bila kupumzika**, basi huhitaji kumtambulisha kila mtu tena, na tunapendekeza uende moja kwa moja kwenye shughuli ya kulisimua.



Haya ni mazungumzo ya wazi; Mtu yeyote ambaye anataka kuzungumza anaweza kuinua mkono wake na kusema kile kinachokuja akilini mwake.



Shughuli 2: Kazi ya vikundi - Kufafanua kuozwa kwa watoto

2.1 Majadiliano ya wazi: dakika 10

Weka karatasi ya chati ambayo imeandikwa mada 'Kuoza kwa watoto' ukutani au kwingine ambapo utaweza kuandikia. Waulize washiriki waeleze kwa uhuru kile kinachokuja akilini mwao au kile wanachofikiria kuhusu wanaposikia maneno kuoza kwa watoto. Eleza kikundi kuwa haya ni majadiliano ya wazi: mtu yeyote anayetaka kuzungumza anaweza kuinua mkono wake na kusema kile kinachomkuja akilini, na eleza kwamba utaandika kile kinachosemwa kwenye karatasi ya chati. Waulize wajadili kile wanachodhani ni tofauti kati ya ndoa za mapema, za kulazimishwa na za watoto. Watu wengi hawajui tofauti, kwa hivyo ni vizuri kuwafanya wafikirie kuhusu tofauti hizi. Ikiwa huelewi ni nini na ni kwa nini mshiriki anasema jambo fulani, muulize aeleze zaidi. Watie moyo washiriki kuulizana maswali pia. Pamoja, tumieni dakika 10 kwa mjadala huu.

2.1 Kazi ya vikundi: Dakika 25

Sasa, wagawanye washiriki katika vikundi (unda idadi ya vikundi / nambari ya washiriki katika kila kikundi itakayokufaa zaidi). Wawezeshe kuingia kwenye vikundi kwa kuuliza mshiriki mmoja ahesabu kwa sauti nambari kuanzia moja, mshiriki wa pili akihesabu kwa sauti mbili, kisha wa tatu akisema tatu na kadhalika - sitisha shughuli kwa idadi ya vikundi unavyotaka kwenye chumba, na kisha anayefuata kuhesabu aanze kuhesabu moja tena. Baada ya haya, wataingia katika vikundi kwa kuunganisha wale wote walioita 'moja' pamoja, wote walioita 'mbili' pamoja na kadhalika. Hii itachukua takriban dakika 5.

Eleza kwamba lengo la kazi ya vikundi ni kuwahimiza washiriki kuzungumza kuhusu uhusiano wao na suala la kuozwa kwa watoto, linamaanisha nini kwao, na kwa nini suala hili ni muhimu kwao. Kila kikundi kinapaswa kuteua mtu ambaye atachukua mazungumzo kwa kuyaandika kwenye karatasi ya chati (mwandishi wa hoja) na kisha kuwasilisha muhtasari kwa kikundi cha jumla. Waulize washiriki watafakari yafuatayo:

1. Ni nini kilichotokea kilichowafanya waamue kufanya kazi ya kukomesha kuozwa kwa watoto (kwa mfano tukio au hali), na kuibua hamu ya kuwa mwanaharakati wa suala hili?
2. Eleza ni kwa nini kuozwa kwa watoto ni suala wanalojali kwa undani. Vikundi vina dakika 10 kwa mazungumzo yao ya pamoja.

Kila kikundi kiwasilishe matokeo yake kuu katika kikundi cha jumla. Kwa pamoja, vikundi vyote vitakuwa na dakika 10 kwa jumla kuwasilisha matokeo yake, kwa hivyo kila kikundi kina takriban dakika 2 kutoa maoni makuu kuhusu kile walichojadili.

Shughuli 3: Uwasilishaji wa mkufunzi: Mafunzo ya msingi- kuozwa kwa watoto

Kama mkufunzi, sehemu hii ni kwa ajili yako kupitia mafunzo ya msingi kuhusu kuozwa kwa watoto pamoja na kikundi na kuelezea masuala kuu yanayohusika. Unapaswa kuonesha uwasilishaji (kutumia karatasi ya chati au njia ya elektroniki) ukipeana muhtasari wa hoja kuu ulizoandaa kabla ya kikao hiki - ili wote waweze kufuata mafunzo ya msingi. Kisha utahitaji kuunganisha taarifa unayotoa na yale ambayo washiriki wameandika hapo awali. Tumekuandalia uwasilishaji wa mfano ambao unaweza kuonesha kuhusu sababu za kuozwa kwa watoto, lakini jisikie huru kuongeza kile unachofikiria ni muhimu kushiriki na kikundi kutoka kwa Maelezo ya Usuli (uk 30).



AU



AU



Mfano wa Uwasilishaji: Mafunzo ya msingi - kuozwa kwa watoto

- Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Watoto ni mkataba muhimu zaidi wa haki za binadamu unaoelezea haki ZOTE za watoto.
- Kuozwa kwa watoto ni miungano isiyo au iliyo rasmi ambapo mtu mmoja au wote wawili wana umri wa chini ya miaka 18.
- Wasichana milioni 12 wanaozwa kila mwaka kabla hawajafikia umri wa miaka 18: Mmoja kila sekunde 2. Hii inapaswa kukomesha!
- Ni ukiukaji wa haki za binadamu na huathiri wasichana zaidi ya wavulana.
- Hutokea kote ulimwenguni na katika tamaduni na dini tofauti.
- Wavuti ya *Girls Not Brides* ina maelezo zaidi, kwa hivyo tembelea www.girlsnotbrides.org

Maelezo ya usuli ya kutumika kwa Uwasilishaji 1 wa Mkufunzi kuhusu kuozwa kwa watoto

Mtoto ni nini?

- Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Watoto (unaofupishwa kawaida kama CRC au UNCRC) ni mkataba wa haki za binadamu unaoainisha haki za watoto za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiafya na kitamaduni. Unaweza kusoma zaidi kuhusu hapa: <https://bit.ly/2HjzOxV>
- Mkataba huu unafafanua mtoto kama binadamu yeyote mwenye chini ya umri wa miaka 18.

Kuozwa kwa watoto ni nini?

- Kuozwa kwa watoto ni muungano rasmi au usio rasmi ambapo mtu mmoja au wote wawili wana umri wa chini ya miaka 18.
- Kulingana na takwimu za hivi karibuni za UNICEF, inakadiriwa kuwa wasichana milioni 12 wanaozwa kila mwaka kabla ya kufikia umri wa miaka 18. Hii inamaanisha wasichana 23 kila dakika, au mmoja kila sekunde 2 - wanaozwa mapema na wakiwa wachanga zaidi, hivyo kuhatarisha ukuaji wao wa kibinafsi, afya na ustawi wao kwa jumla.
- Tendo hili huwaathiri wasichana zaidi kuliko wavulana. Wanawake milioni mia sita na hamsini walio hai leo waliozwa kabla ya kusherehekea siku yao ya kuzaliwa ya 18, ikilinganishwa na wanaume milioni 156.
- Kuozwa kwa watoto huzingatiwa kwa ujumla kuwa ukiukaji wa haki za binadamu na pia kuwa aina ya dhuluma dhidi ya wasichana.

Inatokea wapi?

- Kuozwa kwa watoto ni tatizo ulimwenguni kote, inayotokea katika mikoa, nchi na tamaduni tofauti. Inafanyika kwa takriban kila nchi ulimwenguni na katika dini na makabila tofauti.
- Nchi zingine zina viwango vya juu zaidi vya aidha mzigo (asilimia ya idadi ya watu waliozwa wakiwa chini ya umri wa miaka 18) au uenezi (idadi ya wale walioathirika kutokana na kuozwa kwa watoto). Niger ina kiwango cha juu zaidi cha mzigo duniani ambapo 76% ya wanawake wote wenye umri wa miaka 20 hadi 24 nchini wanasema kwamba waliozwa kabla ya kufikia umri wa miaka 18. India ina idadi kubwa kabisa ya kuozwa kwa watoto ambapo karibu wanawake na wasichana milioni 27 wameathirika.

Kwa habari zaidi

- Tembelea wavuti ya *Girls Not Brides* kwa habari zaidi kuhusu kuozwa kwa watoto na takwimu za kisasa ulimwenguni na kwa kila nchi: www.girlsnotbrides.org

Shughuli 4: Kazi ya vikundi – Sababu za kuozwa kwa watoto katika jamii yako

Kugawanya vikundi vyako

Kabla ya kikao, unahitaji kubainisha ni vikundi vingapi vitafaa kulingana na idadi ya washiriki wako kwa jumla. Jaribu kuwa na vikundi vidogo: kwa hivyo ikiwa una washiriki 20, vikundi vinne vya watu watano vitafaa. Ukitumia mpango huo, kwa mchezo huu utahitaji majina ya matunda manne tofauti, na vipande ishirini vya karatasi. Kwenye vipande vitano vya karatasi, andika jina au picha ya mojawapo ya matunda ulizochagua. Baada ya kuandika majina ya matunda yote manne ukitumia mtindo ulioelezwa, waambie washiriki kwamba watagawanywa katika vikundi kwa kuchagua kipande cha karatasi kilicho na jina la tunda fulani kutoka kwenye bakuli. Kisha wanahitaji kuita tunda kwa sauti kupata ‘marafiki’ wao wengine walio na tunda kama lao, kwa hivyo wa maembe wote watakuwa pamoja na kadhalika, na hivyo kuunda vikundi.

Kazi ya vikundi

Vikundi vyote vinahitaji karatasi ya chati na kalamu za alama kwa kikao hiki. Eleza kwamba kila kikundi watajadili kile wanachofikiria ni sababu za kuozwa kwa watoto katika jamii zao. Tena, wanahitaji kuchagua mwandishi hoja ambaye atawasilisha muhtasari mfupi wa majadiliano yao mwishoni. Anayeandika hoja anahusika na kuandika vidokezo muhimu kutoka kwa majadiliano ambayo wote wanafikiri ni muhimu zaidi. Wana dakika 10 kwa majadiliano haya ya vikundi.

Jukumu lako ni kuwezesha majadiliano na kuhakikisha kuwa vikundi vinazingatia wakati uliotengwa wanapowasilisha.

Maoni na majadiliano ya wazi

Wakati wa kufanya kazi kwa vikundi ukikamilika, waulize wote wabandike karatasi zao zenye jumbe muhimu ukutani na kushiriki kile walichoandika na kikundi cha jumla. Vikundi vinaweza kuulizana maswali au kupata ufafanuzi kuhusu kile kilichoandikwa. Wanaweza kutoa mifano ambayo wamejionea wenyewe kujadili ni kwa nini walitaja hoja fulani. Jukumu lako ni kuwezesha majadiliano na kuhakikisha kuwa vikundi vinazingatia wakati vinapowasilisha. Una jumla ya dakika 15 kwa majadiliano yote katika kikao hiki cha maoni.

Shughuli 5: Uwasilishaji 2 wa mkufunzi - Sababu za kuozwa kwa watoto

Sasa ni zamu yako kuwasilisha tena. Tumia mawasilisho (karatasi ya chati au slaidi ya kielektroniki) uliyoandaa mapema kuangazia taarifa muhimu iliyotolewa hapa chini kuhusu sababu za kuozwa kwa watoto. Uganisha uwasilishaji wako na kile ambacho kikundi kilisema kwenye kikao hapo awali na ueleze sababu kuu. Utakuwa na dakika 10 kuwasilisha kuhusu sababu hizi. Tunapendekeza utumie dakika 5 mwisho wa uwasilishaji wako kwa majadiliano ya wazi ili kikundi cha jumla kiulize maswali yoyote kuhusu mada uliyoshughulikia, au ili kuwauliza washiriki maoni yoyote kuhusu masuala uliyoibua.



AU



AU



Mfano wa Uwasilishaji: Sababu kuu za kuozwa kwa watoto

- Ukosefu wa usawa wa kijinsia ndio sababu kuu ya kuozwa kwa watoto. Namna wasichana na wavulana na wanawake na wanaume wanavyozingatiwa katika jamii siyo sawa na mara nyingi wasichana hawathaminiwi na wanaonekana kama mzigo.
- Umaskini: ikiwa familia ni maskini, kumuoza binti yao mapema kunaonekana kama kupunguza mzigo kwa familia, kwa rasilimali zilizo chache tayari, na idadi ya watu wa kulisha.
- Kuozwa kwa watoto mara nyingi huonekana kama sehemu ya utamaduni na mila ya jamii. Wakati mwingine hata dini zingine huruhusu mazoea hayo.
- Kuozwa mapema, kwa kulazimishwa na kuozwa kwa watoto mara nyingi hufikiriwa kuwa njia ya kulinda wasichana dhidi ya unyanyasaji wa kingono, unyanyasaji wa kijinsia, vitendo vya ngono 'haramu', na uasherati.
- Kukosekana kwa usalama na vurugu katika jamii pia ni sababu, na hivyo familia zinafikiria kuoza watoto wa kike mapema ni njia ya kuwapa usalama.
- Mifumo dhaifu ya serikali: kuna sheria zinazopinga kuozwa kwa watoto lakini mara nyingi hazitekelezwi na serikali, au kuna sehemu zilizotulizwa ndani ya sheria.
- Elimu kidogo na upungufu wa chaguzi za kiuchumi kwa wasichana ni vichochezi vikuu kwa familia zinazooza mabinti zao wakiwa wachanga zaidi.
- Ukosefu wa ufahamu: watu wengi, haswa wasichana wadogo, hawajui haki zao au jinsi ya kuzilinda.

Sababu za kuozwa kwa watoto

- Kuozwa kwa watoto ni suala gumu linalosababishwa na mambo mengi tofauti - ambayo tunayaita 'vichochezi' vya tatizo hili. Hizi zinaweza kuwa tofauti kutoka nchi moja hadi nyingine na hata jamii moja hadi nyingine, na zinaweza kubadilika kwa muda ndani ya jamii moja au muktadha.
- Sababu kuu ya kuozwa kwa watoto ni ukosefu wa usawa wa kijinsia na thamani ndogo inayopewa wasichana na wanawake katika jamii. Wavulana mara nyingi huzingatiwa kuwa na thamani ya juu kwa familia kwa sababu ya uwezo wao wa kimapato unaozingatiwa kuwa wa juu.



KUMBUKA

Jinsia inahusu tofauti za kijamii na uhusiano kati ya wanaume na wanawake na majukumu wanayochukua katika jamii - si tofauti ya kibiolojia kati yao.

Usawa wa kijinsia ni haki, majukumu, fursa, matendo na thamani sawa zinazopewa wanawake na wanaume, wasichana na wavulana - maishani na kazini. Usawa wa kijinsia inamaanisha kuwa watu wa kila kizazi na jinsia wana nafasi sawa za kufanikiwa maishani.

- Katika jamii nyingi ambapo kuozwa kwa watoto kunatendwa, wasichana hawathaminiwi kama wavulana na mara nyingi huonekana kama mzigo zaidi kwa familia zao. Kuoza binti akiwa na umri mdogo kunaweza kuonekana kama njia ya kupunguza wasiwasi kwa familia zilizo na mapato madogo, kwa kuhamisha 'mzigo' huu kwa familia ya mumewe.
- Kuozwa kwa watoto pia kumehusishwa sana na taasubi za kiume (inayoitwa pia imani ya ubwana wa kiume) ambayo hutawala jamii nyingi, na kudhibiti ujinsia wa kike. Kwa mfano, inajumuisha kudhibiti jinsi msichana anapaswa kuenenda, jinsi anapaswa kuvaa, ni nani anapaswa kuruhusiwa kumuona, na ni nani atamuoa - kawaida na baba yake, au wanaume katika familia au jamii.
- Katika jamii nyingi, familia zinalinda kwa ukaribu ujinsia wa mabinti zao. Ubikira una bei ya juu na ni muhimu kuulinda na kuudumisha, kwani unahusishwa na heshima ya familia, na kwa msichana kuzingatiwa kuwa nadhifu. Wasichana ambao wana uhusiano wa kingono au wanapata ujauzito nje ya ndoa mara nyingi huonekana kama wanaleta aibu na ukosefu wa heshima kwa familia.

Utamaduni na mila

- Katika jamii nyingi kuozwa kwa watoto ni mila, inayochukuliwa kama sehemu ya mila au tamaduni, au wakati mwingine dini, na ambayo imeendelea kwa vizazi.
- Kwa mfano, katika jamii zingine, msichana anapoanza kupata hedhi anazingatiwa kuwa mwanamke mbele ya jamii. Ndoa inaonelewa kama hatua inayofuata ili kumpa hadhi yake kama mke na mama, bila kujali umri wake.
- Itikadi zingine za kitamaduni mara nyingi huhusishwa na kuozwa kwa watoto, haswa utendaji hatari dhidi ya wasichana, kama vile ukeketaji au ukataji wa kike (FGM/C). Hii inachukuliwa kama mpito wa kidesturi wa kuwa mwanamke na hakikisho kuwa msichana anaonekana "nadhifu".
- Ingawa desturi ya kuozwa kwa watoto imejikita katika mila na desturi, haya ni mazoea yaliyotengenezwa na binadamu ambayo yanaweza kubadilishwa na kusasishwa. Kwa hivyo, kuna matumaini ya kuhakikisha mabadiliko na kukomesha vitendo hivi vinavyodhuru na kuharibu wasichana.

Umaskini

- Katika jamii zilizo na umaskini wa viwango vya juu, familia (wakati mwingine hata wasichana wenyewe) wanaamini kuwa kuozwa mapema itakuwa suluhisho la kupata usalama katika maisha yao ya baadaye. Maoni haya yanaruhusu wazazi kudhani wamepunguza gharama za kifamilia kwani wanaonelea kuwa wamepunguza mtu mmoja wa kulisha, kuvisha na kuelimisha.
- Katika jamii ambazo mahari au ‘malipo ya mke’ hulipwa, mara nyingi ni chanzo cha mapato kinachokaribishwa kwa familia masikini. Katika zile ambazo familia ya bibi harusi hulipa mahari kwa ya bwana harusi, mara nyingi hulazimika kulipa pesa kidogo ikiwa bibi harusi ni mchanga na hajasoma, kwa hivyo familia hufanya hivyo ili kupunguza gharama.
- Uchumi una athari kubwa katika mitazamo ya mazoea ya kuozwa kwa watoto kwa sababu wasichana wanaonekana kama wategemezi wa uchumi, wala sio wanaoweza kutengeneza mapato. Lakini kuozwa kwa watoto huendeleza mzunguko wa umaskini, kwani wasichana wanaooswa wakiwa wachanga hawatasomeshwa vyema au kushiriki katika kufanya kazi .

Ukosefu wa usalama na vurugu

- Katika nchi zilizo na vita na mizozo, wasichana wako katika hatari kubwa ya kunyanyaswa na kushambuliwa kimwili au kingono. Katika mikoa isiyo salama, wazazi mara nyingi wanaamini kwa dhati kwamba kuwaoza mabinti wao mapema ni kwa faida yao kuwalinda kutokana na tishio.
- Ukweli ni kwamba wasichana walioozwa wanakabiliwa na tishio kubwa zaidi la dhuluma, na wana upungufu wa nguvu ya kutumia haki zao, haswa na mabwana zao.

Mifumo dhaifu ya serikali

- Kuozwa kwa watoto ni haramu katika nchi nyingi duniani. Lakini sheria inaweza kubadilishwa kwa njia na muktadha nyingi, kwa mfano ikiwa inajumuisha tofauti za kipekee, kama vile katika idhini ya wazazi kama walezi halali. Sheria zinatafsiriwa tofauti au kwa njia zisizo na usawa.
- Katika nchi nyingi umri wa chini wa ndoa unawekwa na sheria ya kimila au ya kidini, ambayo kawaida inapingana na sheria za kitaifa na mikataba ya kimataifa. Nchi nyingi pia hazina sheria, au njia za kutekeleza sheria, na zina miundo dhaifu ya utawala - kwa hivyo sheria ni muhimu lakini hazijitoshelezi kwa kipekee.

Elimu kidogo na hali ya chini ya uchumi

- Kuhudhuria shule na kuwa na viwango vya juu vya elimu husaidia kulinda wasichana kutokana na uwezekano wa kuozwa wakiwa watoto na kuwawezesha kujua kuhusu haki zao. Katika nchi nyingi, kuelimisha wasichana hakupewi kipaumbele kama kuelimisha wavulana.
- Wakati jukumu muhimu zaidi kwa mwanamke linafikiriwa kuwa lile la kuwa mke, mama na mtunza nyumba, kusomesha wasichana na kuwaandaa kwa maisha ya kufanya kazi haionekani kuwa muhimu. Hata familia ambazo zinataka kupeleka watoto wao wa kike shuleni mara nyingi hukosa kupata shule za karibu, zenye ubora na pia hukosa pesa za kulipia gharama. Mara nyingi inaonekana kuwa salama na kwa faida zaidi kiuchumi kutumia rasilimali chache kuwafundisha wavulana, kuliko wasichana.

Kukosa uhamasisho

- Kuozwa kwa watoto pia ni matokeo ya kukosa uhamasisho kati ya wazazi, jamii na watoto wenyewe kuhusu sheria za kitaifa na kuhusu haki za watoto na wanawake. Wengi hawajui kuhusu haki za kimataifa au mikataba - au jinsi ya kuhakikisha haki zao zinalindwa.

Shughuli 6: Wakati wa maswali na hitimisho

Jaribio la haraka

Mara tu unapomaliza uwasilishaji wako, waeleze washiriki kwamba sasa unataka kufanya jaribio kuhakikisha kwamba wamekuwa wakisikiliza na kuelewa masuala kuu kuhusu kuozwa kwa watoto. Wakati wa jaribio: uliza kikundi kizima maswali haya na uwaambie watu wataje majibu yao kwa sauti.

- Mtoto ni nini?
- Kuozwa kwa watoto ni nini?
- Sababu zake ni zipi? (kila mmoja ataje sababu moja)

Una dakika 3 za kuuliza maswali na kupata majibu kutoka kwa kila mshiriki.

Malizia

Shukuru kila mtu kwa kazi yake nzuri na ufunge kikao kwa kupeana makumbusho ya yale umeandika na mada ambazo utazungumzia katika warsha inayofuata. Ikiwa mtafanya kikao kinachofuata baadaye ndani ya wiki au wiki inayofuata, mkumbushe kila mtu wakati na tarehe ya kikao. Ikiwa utasimamia kikao hicho kama sehemu ya mafunzo ya siku hii nzima, tunapendekeza upumzike sasa ili kuruhusu kikundi chako kunyoosha miguu na kupata viburudisho. Mapumziko ya mara kwa mara husaidia kuhakikisha kwamba kikundi chako kinasisimuka, kina nguvu na kiko tayari kujifunza na kushiriki!



Moduli 1 - Kikao 3

Kuozwa kwa watoto – athari na ukingaji

 <p>Lengo</p> <p>Washiriki wataelewa athari za kuozwa kwa watoto kwa wasichana, mikakati mbalimbali ya kuizuia ambayo inapatikana, na jukumu watu tofauti wanaweza kuchukua katika kushughulikia suala hili.</p>  <p>Idadi ya washiriki: Chini ya 24</p>	 <p>Muhtasari wa kikao</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kujifunza kuhusu athari za kuozwa kwa watoto • Kujadiliana kuhusu masuluhisho yanayoweza kukomesha kuozwa kwa watoto  <p>Wakati unaohitajika: Saa 1 Dakika 30</p>	 <p>Vitu vya kuandaa mapema</p> <ul style="list-style-type: none"> • Soma maelezo ya usuli na uyajue vizuri ili uwe na ujasiri wa kuwasilisha haya kwa kikundi cha jumla • Slaidi za uwasilishaji (za kielektroniki au kwenye chati) zenye hoja kuu kuhusu athari za kuozwa kwa watoto • Fanya mazoezi ya shughuli ya kuisimua kama utaifanya pamoja na kikundi • Andaa zoezi la kazi ya vikundi 5: andaa majina ya vikundi (serikali, asasi za kiraia, na jamii) na jinsi utagawanya vikundi 	 <p>Vifaa vinavyohitajika</p> <ul style="list-style-type: none"> • Karatasi za chati • Kalamu za alama au kalamu nene • Slaidi za mawasilisho • Hati za mchoro unaonyesha 'athari za kuozwa kwa watoto' • Hati za Nadharia ya Mabadiliko ya <i>Girls Not Brides</i> • Bakuli kwa ajili ya kuweka karatasi zenye majina ya vikundi katika shughuli 4
--	---	--	---

Shughuli	Wakati uliotengwa	Muhtasari
1	Dakika 5	Karibu <ul style="list-style-type: none"> • Utangulizi na makumbusho (ikiwa hiki ni kikao cha pekee) • Utangulizi mfupi wa lengo na mada za kikao (ikiwa utafanya kikao kwa mfululizo baada ya Moduli ya 1: Kikao cha 2)
2	Dakika 10	Uwasilishaji wa mkufunzi: Athari na matokeo ya kuozwa kwa watoto
3	Dakika 15	Group discussion: Consequences of child marriage that you see in your community or from your experience.
4	Dakika 30	Group work session: What prevention strategies would work in your community?
5	Dakika 15	Trainer presentation: Strategies for prevention
6	Dakika 15	Open floor discussion and close of the session

1.3 Mwongozo wako wa mkufunzi

Shughuli 1: Karibu

Ikiwa hiki ni kikao cha pekee

Karibisha kikundi chako pamoja tena. Kama ilivyo kwenye kikao cha 2 cha moduli hii, ikiwa hiki ni kikao cha pekee (kumaanisha unafanya kikao hiki siku nyingine au wiki baada ya kikao kilichopita) basi mwambie kila mtu ajitambulishe ili wote wakumbuke majina ya kila mmoja. Wakumbushe ni kwa nini sisi sote tuko pamoja kisha pitia makumbusho ya sheria za msingi mlizoainisha pamoja na tahadhari ya unyeti. Eleza kikundi kuwa katika kikao hiki, tutakuwa tunajifunza pamoja kuhusu athari za kuozwa kwa watoto. Ni muhimu pia kupitia haraka hoja kuu ulizozungumzia katika kikao kilichopita - tunapendekeza upitie haraka mawasilisho mawili uliyoonyesha katika kikao cha 2.

AU

Ikiwa unafanya kikao hiki kama sehemu ya warsha kamili ya mafunzo

Ikiwa unasimamia kikao hiki kama sehemu ya warsha kamili ya mafunzo (kumaanisha kimejumuishwa na vikao vingine), basi tunapendekeza sasa uwe wakati wa kuwa na shughuli ya kusisimua, maana hutahitaji kufanya makumbusho au marudio. Unaweza tu kuwasilisha malengo makuu ya kikao, mada kuu ambazo utajadili, na ukumbusho mfupi kuhusu unyeti na umuhimu wa kila mtu kuheshimu maoni ya mwenzake.



Shughuli 2: Uwasilishaji wa mkufunzi - Athari za kuozwa kwa watoto

Ni muhimu katika sehemu hii kutumia chati ya kikao kilichopita kuhusu kuozwa kwa watoto kama ukumbusho kwa washiriki wote. Sasa ni wakati wa kuwasilisha kikao chako, ambacho kitachunguza athari za kuozwa kwa watoto. Tumia jedwali lifuatalo kwa mifano ya vidokezo rahisi ambavyo unaweza kujumuisha katika uwasilishaji wako kwa kikundi. Tunapendekeza utumie mchoro ambao tumejumuisha kusaidia kuonesha athari za kuozwa kwa watoto. Tunapendekeza washiriki tofauti wasome mstari mmoja kisha mwingine kwa sauti, badala ya wewe kusoma kama mtangazaji anayesimamia kikao. Uliza kila mshiriki anayesoma maoni yake kuhusu taarifa waliyosoma. Hii ni njia bora ya kuwafanya washiriki wafikirie kuhusu mada na kuwashirikisha katika kile unachojadili kwenye kikao.



AU



AU



Mfano wa Uwasilishaji: Matokeo ya kuozwa kwa watoto ni gani?

- Kuna mambo mengi mabaya yanayotokea kama athari za kuozwa kwa watoto. La muhimu zaidi ni kwamba huwanyima wasichana ulinzi na utekelezaji wa haki zao za msingi za afya, elimu na maendeleo.
- Kuozwa kwa watoto huathiri vipengee vyote vya haki msingi za kibinadamu za wasichana: afya, elimu, uchumi, ukosefu wa usawa, na kunaongeza tishio kwao la dhuluma na umaskini.
- Kuozwa kwa watoto hunawanyima wasichana haki ya kupata elimu.
- Kunamfanya afungiwe katika mzunguko wa umaskini.
- Kunamnyima haki ya maisha yenye afya au haki ya kudhibiti afya yake ya kijinsia na ya uzazi kwa kuhimiza ujauzito wa kulazimishwa na uzazi wa mapema. Hii inasababisha kuongezeka kwa hatari ya kifo au kujeruhiwa wakati wa ujauzito na wakati wa kujifungua.
- Humwacha bila au na fursa ndogo ya kufikia habari na huduma za kuzuia ujauzito au maambukizo, na kuongeza uwezekano wa kuwa na watoto wengi kwa mfululizo.
- Inamuondolea nguvu ya kujadili au kudhibiti maamuzi yake mwenyewe. Kwa mfano, inaweza kuwafanya watu kuwa katika tishio zaidi la kuambukizwa VVU / UKIMWI, na inaweza kusababisha wasichana washindwe kupata chaguzi salama za ngono. Pia inaongeza nafasi zake za kukumbana na dhuluma za kimwili, kihemko au maneno.

Je, kuozwa kwa watoto kunamaanisha nini kwa wasichana?

UMASKINI

Watoto walioozwa hawapati fursa za kielimu na kiuchumi zinazosaidia kuwainua wao na familia zao kutoka kwenye umaskini. **WANAWEZA KUWA MASKINI NA KUBAKI MASKINI.**



ELIMU

Watoto walioozwa wana uwezekano wa **KUONDOKA SHULENI**, kuziwa ukuaji wao wa kibinafi, maandalizi ya utu uzima na uwezo wao wa kimapato.



UKOSEFU WA USAWA

Watoto walioozwa huwa na **UWEZO MDOGO WA KUAMUA NI LINI AU NI NANI WATAOA**. Ndoa mara nyingi hukomesha fursa za wasichana kupata elimu, kazi zinazolipa bora zaidi nje ya nyumbani mwao na majukumu ya kufanya maamuzi katika jamii zao.



AFYA

Watoto wanaozwa wanakabiliwa na tishio kubwa la kifo au kujeruhiwa: wasichana ambao hujifungua kabla ya umri wa miaka 15 **WANA UWEZEKANO MKUBWA ZAIDI WA KUFUWA WANAJIFUNGUWA** kuliko wanawake wenye miaka 20-24. Watoto wao wana uwezekano mdogo wa kuishi zaidi ya siku yao ya kuzaliwa ya 1.



VVU / UKIMWI

Watoto walioozwa wanakabiliwa na ngono ya mara kwa mara, na bila kinga kwa ajili ya shirikizo la kuonesha uzazi wao, na wanakosa maarifa na nguvu ya kujadili mazoea salama ya ngono. Watoto walioozwa mara nyingi huozwa kwa waume watu wazee kuwaliko, **HILI HUONGEZA HATARI KWAO KUAMBUKIZWA VVU.**



DHULUMA

Kuozwa kwa watoto kunaweka wanawake na wasichana katika tishio kubwa la dhuluma katika maisha yao yote. Watoto walioozwa **WANA UWEZEKANO MKUBWA ZAIDI WA KUELEZA KWAMBA WALIPO PITIA NGONO MARA YA KWANZA, WALILAZIMISHWA.**



Huu ni mfano wa picha wasilishi ambayo unaweza kutumia kwa uwasilishaji wako kwani ni muhimu kuonesha kile unachojadili. Ili kupata nyenzo kama hizo, tembelea tovuti yetu:

www.girlsnotbrides.org

Vidokezo vya wakati unapowasilisha picha

Eleza vikundi vyako kwamba ikiwa hatutazuia kuozwa kwa watoto kutokea, kuna mlolongo wa watu ambao wataendelea kuathiriwa. Hii ni kwa sababu wanawake wengi ambao wanalazimishwa kuolewa wakiwa watoto hupoteza haki zao na nguvu zao kuzuia hili kutokea kwa watoto wao. Tunapendekeza uzungumzie hoja kwenye picha na uwape washiriki tofauti fursa ya kusoma na kuzungumzia kile wanachofikiria kuhusu kila sehemu.

Maelezo ya usuli ya uwasilishaji wako

Athari za kuozwa kwa watoto

- Kuozwa kwa watoto ni ukiukaji wa haki za binadamu. Huwanyima wasichana wadogo haki zao za msingi za afya, elimu, maendeleo na ulinzi. Mienendo hii haiathiri wasichana tu wenyewe, bali pia watoto wao na familia zao, na pia jamii nzima.
- Afya: Kuozwa mapema hunawanyima wasichana haki ya kuishi maisha yenye afya. Mara nyingi wao hushinikizwa kuwa akina mama wenye umri mdogo, na hili huongeza hatari la kifo au kujeruhiwa wakati wa ujauzito na wa kuzaa. Pia huongeza hatari ya kifo na matatizo ya kiafya ya muda mrefu kwa watoto wachanga.
- Huongeza uwezekano wa wasichana kupata VVU / UKIMWI, kwani wasichana hawawezi kushawishi ngono salama. Huongeza hatari kwao kupitia unyanyasaji wa kimwili, kingono na kihemko. Wasichana ambao wanaozwa kabla ya umri wa miaka 18 wana uwezekano mkubwa wa kukumbana na ukatili ndani ya ndoa kuliko wasichana ambao wanaolewa baadaye, kwa sababu ya ukosefu wa usawa wa mamlaka kwenye uhusiano.

- Huwanyima wasichana haki ya kuchagua na kujifanyia maamuzi muhimu kuhusu maisha yao. Watoto waliozwa hawana uwezo wa kuamua kuhusu ikiwa wataoa au ni lini na ni nani wataoa.
- Kuozwa kwa watoto humnyima msichana haki ya kupata elimu. Kuozwa mara nyingi husababisha msichana kuondolewa shuleni. Hii huathiri uwezo wake wa kujifunza ujuzi anaohitaji ili kupata kazi na kupata fursa sawa za kiuchumi kama wavulana. Bila fursa hii, hataweza kuvunja mzunguko wa umaskini na hivyo atabaki amenaswa.

Shughuli 3: Majadiliano ya kikundi – Je, ni athari zipi za kuozwa kwa watoto unaziona katika jamii yako?

Waambie washiriki kwamba sasa mmepitia matokeo ya kuozwa kwa watoto na athari zake kwa maisha ya wasichana. Eleza kwamba ungependa kuwa na mazungumzo ya wazi na wao kuhusu kile wanachosea ni athari za kuozwa kwa watoto ndani ya jamii zao. Hii ni kuwawezesha wafikiri athari ni nini kutoka kwa mitazamo yao na katika jamii zao, na pia ni njia ya kuhakikisha wanaelewa athari mbalimbali ambazo mazoea haya huleta kwa maisha ya wasichana. Popote inapohitajika, waulize washiriki wafanue kuhusu kile wanachosema na kuelezea zaidi, au kutoa mifano kutoka kwa waliyopitia wenyewe. Kwa mfano, ikiwa wanasema ‘dhuluma’ au ‘afya duni’, basi waulize waeleze zaidi au watoe mifano ya kile wanachomaanisha. Kama mkufunzi, unapaswa kuandika kile ambacho washiriki tofauti wa kikundi wanasema kwenye karatasi ya chati. Una dakika 15 kwa majadiliano ya wazi na kikundi chote.

Shughuli 4: Kazi ya vikundi - Ni mikakati gani ya kuzuia kuozwa kwa watoto inaweza kufaulu katika jamii yako?

Kuingia kwenye vikundi

Kwa shughuli hii, tunapendekeza ugawanye kikundi cha jumla kuwa vikundi vitatu vya ‘wahasika’ wakuu au wadau ambao ni muhimu kushirikisha ili kushughulikia kuozwa kwa watoto. Vikundi hivi ni serikali, asasi za kiraia, na jamii yenyewe. Wagawanye washiriki wote katika vikundi hivyo ambavyo baadaye vitakuwa wadau hawa ili waweze kuelewa ni nini kila kikundi kinahitaji kuzingatia, na thamani ambayo kila kikundi kinachangia kukomesha kuozwa kwa watoto. Ili kufanya hivyo, unahitaji kutenganisha kila mtu katika vikundi vitatu. Unahitaji vipande vya karatasi vilivyoandikwa ‘Serikali’, ‘Asasi za Kiraia’ na ‘Kiongozi wa Jamii’ na kisha uzikunje kwenye bakuli ili watu wasione maneno. (Gawanya idadi katika kikundi cha jumla kwa tatu, kisha tengeneza idadi hizo za karatasi kwa kila kikundi cha washikadau - ili kila mshiriki apate karatasi moja.) Pitisha bakuli na umwambie kila mtu achukue karatasi (bila kuangalia ndani yake hadi wote wapate karatasi). Waambie vikundi vitatu vitafutane kwa kuita neno lililo ndani ya karatasi zao kisha wakae katika vikundi vyao kwenye meza tofauti. Una dakika 5 kuwapanga katika vikundi.

Kazi za vikundi

Eleza kwa vikundi vitatu kwamba kuozwa kwa watoto kumeenea nchini mwao na wamepewa jukumu kama waigizaji wakuu kuimaliza. Lazima wabuni hatua tatu muhimu au mikakati ya kuuzuia. Ingekuwa vyema kwao kutafakari kuhusu kile ambacho tayari kinatekelezwa kuhusu suala hili katika nchi / jamii yao, na kisha ni nini zaidi kinachohitajika kufanywa kulishughulikia hili na jukumu lao litakuwa nini katika kusaidia.

Kama ilivyo kwa kazi nyinginezo za kikundi, sharti kila kikundi kiwe na mtu anayeandika muhtasari ambaye atanasa mjadala na kuwasilisha kwa kikundi kikubwa. Eleza kwamba wanaweza kutumia Nadharia ya Mabadiliko ya *Girls Not Brides* kuwasaidia kujua njia ambazo wanaweza kukomesha kuozwa kwa watoto. Vikundi vina dakika 15 kujadili hili kati yao. Waambie vikundi waandike mikakati yao na wawasilishe kwa kikundi cha jumla: kuna dakika 10 kwa vikundi vyote kuwasilisha, kwa hivyo hakikisha wanazifanya hoja zao kuwa rahisi na fupi.

Shughuli 5: Uwasilishaji wa mkufunzi - Mikakati ya kuzuia kuozwa kwa watoto

Hiki ni kikao kinachofuata cha kuwasilisha kama mkufunzi, na lengo lake ni kuzungumza kuhusu mikakati anuwai ya kuzuia kuozwa kwa watoto. Ni muhimu kuonesha uhusiano kati ya uwasilishaji wako kuhusu mikakati ya kuuzuia na kile ambacho tayari kimewekwa kwa chati na kikundi kutoka kikao kilichopita cha maoni yao kuhusu athari pamoja na jinsi mikakati hii inavyofanya kazi kupunguza athari hizi mbaya. Tunapendekeza utumie dakika 10 kwa uwasilishaji huu na utenge dakika 5 mwishoni ya kuwa na mazungumzo ya wazi ikiwa mtu yeyote ana maswali yoyote au anataka kupitia mambo tena kwa undani zaidi.

Maelezo ya usuli kwa uwasilishaji wako

Mikakati ya kuzuia kuozwa kwa watoto

- Maana kuna sababu au vichochezi vingi vya kuozwa kwa watoto, haishangazi kwamba kuna njia nyingi ambazo tunaweza kufanya kazi ili kumaliza mazoea haya.
- Kuzuia kuozwa kwa watoto kunamaanisha tunahitaji hatua katika viwango vyote: kutoka kiwango cha ulimwenguni hadi kwenye jamii. Na tunahitaji pia mbinu za umoja, na zisizobagua, zikitumika na vikundi anuwai, vyote vikifanya kazi pamoja katika nyanja zote: kutoka serikali hadi asasi za kiraia, wazazi na viongozi wa jamii, hadi kwako, na kisha moja kwa moja hadi kwa vikundi vilivyoathiriwa.
- Nadharia ya Mabadiliko ya *Girls Not Brides* inaonyesha kuwa kila mtu ana jukumu katika kusaidia kuzuia kuozwa kwa watoto, na pia kwa kusaidia wasichana walioolewa. Inapatikana kwenye tovuti yetu.



Mambo ambayo serikali zinaweza kufanya...

- Kutunga sheria za kupiga marufuku kuozwa kwa watoto na kuondoa vifungu vyovyote vinavyoruhusu ubaguzi wa hali fulani, kama vile kuozwa kwa idhini ya wazazi au dini.
- Serikali zinahitaji kuunda mikakati ya kitaifa ambayo ni mipango ya utekelezaji ya kuzuia au kuchelewesha kuozwa kwa watoto. Katika mikakati hii ya kitaifa, uwekezaji wa rasilimali unahitajika kulenga wasichana masikini na waliotengwa zaidi, kwani ndio walio katika tishio zaidi la kuozwa kwa watoto.
- Kutoa huduma bora kama vile elimu, huduma za afya na ulinzi, na kufanya kazi kuhakikisha wasichana wanapata huduma hizi, bila kujali asili yao au mapato. Hii pia itasaidia kuhimiza wazazi kuwapeleka wasichana wao shuleni na kuwaweka shuleni kwa muda mrefu iwezekanavyo.

Mambo ambayo asasi za kiraia (AZAKi) zinaweza kufanya...

- Kusaidia kuongeza uelewa kuhusu suala hili na mambo yote yanayohusiana nayo! Kwa kuwa hili bado ni suala la mwiko katika nchi nyingi, majadiliano ya kutia moyo husaidia kuongeza ufahamu na kuelimisha jamii. Kushiriki athari za kuozwa kwa watoto - kupitia habari kuhusu haki za kimsingi za kibinadamu - yote husaidia watu kuelewa anuwai ya athari hizi kwa wasichana na wanawake. Ni muhimu kuwashirikisha wanaume na wavulana pia ili waweze kuwa na uwezo katika mapambano ya kukomesha kuozwa kwa watoto.
- Kutekeleza miradi ya kuwawezesha wasichana na jamii zao kusema hapana wanapokabiliwa na ushawishi wa kuozwa. Hii ni kwa kujenga ustadi, ujuzi na uwezo wa kufikia mifumo ya msaada ambayo itasaidia kuimarisha wasichana kufanya maamuzi na kukithirisha ufikiaji wa fursa. Mifumo ya msaada wa rika ni muhimu mno katika kufikia hili.
- Fanya kazi na wadau wengine: kusaidia utekelezaji wa sheria za serikali dhidi ya kuozwa kwa watoto, kushinikiza kutengenezwa kwa sheria ambapo hazipo tayari. Wahamasishwa na kuwaelimisha viongozi wa dini na wazee wa jamii kuhusu athari mbaya za mila, kama vile kuozwa kwa watoto.

Mambo ambayo viongozi wa jadi wanaweza kufanya...

- Kusaidia kubadilisha maoni - mazoea ya jadi na kitamaduni ambayo hudhuru wasichana na wanawake yanaweza kubadilishwa. Haitoshi tu kusema 'ni utamaduni wetu' - na viongozi wa jadi ni muhimu sana katika kuelewa athari mbaya na kusaidia kubadilisha mazoea, hasa kubadilisha maoni ya jadi, ya kibaguzi kuhusu ufikiaji wa elimu kwa wasichana.
- Kusaidia juhudi za serikali na asasi za kiraia kupitisha sheria dhidi ya kuozwa kwa watoto, na kusaidia kuhakikisha kuwa sheria hizi zinazingatiwa. Pia kusaidia kueneza habari kadiri inavyowezekana ili wanajamii wote waunge mkono mabadiliko.
- Hakungekuwa na kuozwa kwa watoto ikiwa wanaume katika jamii zilizoathiriwa hawangechagua kuoa watoto. Kwa hivyo ni muhimu kwamba wanaume waelimishwe kuhusu haki za wasichana na jinsi ndoa ya mapema inaweza kuwa na madhara kwa afya na furaha ya wasichana, na vilevile kuwa uharibifu kwa kitengo cha familia. Kwa maana viongozi wengi wa jadi au dini ni wanaume, wao ni muhimu katika kusaidia jamii kubadilika ili kuona thamani ya wanawake na wasichana.


Shughuli 6: Majadiliano ya jumla na kuhitimisha kikao

Tunapendekeza utenge dakika chache mwisho wa kikao chote kama nafasi wazi kwa mtu yeyote kuuliza maswali, kuuliza kupitia masuala fulani au kurejelea kutoka kwa vikao vingine, au tu kukujulisha chochote kilicho muhimu kwao. Hili pia linaweza kuwa kikao muhimu kuuliza kikundi yale wanahisi wamejifunza hadi sasa. Kisha unaweza kujumlisha masuala uliyoyashughulikia kwa kupitia tena chati zilizo ukutani. Kama kawaida, shukuru kila mtu kwa ushiriki wao kamili na ueleze muhtasari wa kikao kijacho.





Picha © Allison Joyce / Girls Not Brides



Moduli 2: **Kufanya utafiti** **kuhusu kuozwa** **kwa watoto** **katika jamii yako**

Muhtasari wa Moduli

- Kuchunguza jinsia na jinsi inavyoathiri maisha yetu ya kila siku.
- Jinsi ya kufanya uchambuzi wa kijinsia unapofanya kazi katika jamii yako.
- Kufanya kazi na wanaume na wavulana.

Moduli 2 - Kikao 1

Kuchunguza jinsia



Lengo

Kila mtu kwenye kikundi aelewe tunamaanisha nini tunaposema usawa wa kijinsia na jinsi ya kutekeleza uchambuzi wa kijinsia. Tutachunguza pia ni kwa nini tunahitaji kuwashirikisha wavulana na wanaume wakati tunashughulikia suala la kuozwa kwa watoto



Idadi ya washiriki:
Chini ya 24



Muhtasari wa kikao

- Kujifunza kuhusu jinsia; usawa wa kijinsia ni nini
- Jinsi ya kufanya uchambuzi wa kijinsia
- Kuangalia jinsi ya kufanya kazi pamoja na wanaume na wavulana kama mabingwa wa suala hili



Wakati unaohitajika:
Saa 2 Dakika 35



Vitu vya kuandaa mapema

- Soma maelezo ya usuli na uyajue vizuri ili uwe na ujasiri wa kuwasilisha haya kwa kikundi cha jumla
- slaidi za uwasilishaji (za kielektroniki au kwenye karatasi)
- Fanya mazoezi ya shughuli ya kuisimua kama utaifanya pamoja na kikundi
- Tengeneza nakala za jedwali la mienendo ya kijinsia zitakazotumika na kila mtu katika kikundi chako



Vifaa vinavyohitajika

- Karatasi za chati
- Kalamu za alama au kalamu nene
- Mawasilisho

Shughuli	Wakati uliotengwa	Muhtasari
1	Dakika 5	Karibu • Utangulizi na makumbusho (ikiwa hiki ni kikao cha pekee) AU • Shughuli ya kuisimua na utangulizi mfupi wa lengo la kikao (ikiwa unafanya kikao kwa mfululizo baada ya Moduli 1)
2	Dakika 5	Majadiliano ya wazi: Jinsia ni nini?
3	Dakika 20	Majadiliano ya kikundi: Kumbukumbu za kwanza za jinsia
4	Dakika 10	Uwasilishaji wa mkufunzi: - Jinsia ni nini?
5	Dakika 10	Majadiliano ya wazi: Usawa wa kijinsia
6	Dakika 25	Majadiliano ya kikundi: Ukosefu wa usawa wa kijinsia
7	Dakika 10	Uwasilishaji wa mkufunzi: - Je, tofauti ni ipi kati ya ukosefu wa usawa wa kijinsia na usawa wa kijinsia?
8	Dakika 10	Uwasilishaji wa mkufunzi: - Uchambuzi wa kijinsia
9	Dakika 35	Kazi ya vikundi: Kufanya uchambuzi wa kijinsia
10	Dakika 5	Kuwaza: Kwa nini uwahusishe wanaume na wavulana?
11	Dakika 10	Uwasilishaji wa mkufunzi: - Kufanya kazi na wanaume na wavulana
12	Dakika 10	Hitimisho na kufunga kikao

2.1 Mwongozo wako wa mkufunzi

Shughuli 1: Karibu

Ikiwa hiki ni kikao cha pekee

Karibisha kikundi chako. Kama ilivyo kwa kikao cha awali cha Moduli 1, ikiwa hiki ni kikao cha pekee (kumaanisha unafanya kikao hiki siku nyingine au wiki baada ya kikao kilichopita) basi uliza kila mtu ajitambulishe ili wote wakumbuke majina ya kila mmoja. Wakumbushe ni kwa nini sisi sote tuko pamoja na haraka, pitia makumbusho ya sheria za msingi mlizoainisha pamoja na tahadhari ya masuala nyeti. Eleza kikundi kwamba katika kikao hiki tutachunguza suala la jinsia na jinsi ya kufanya uchambuzi wa kijinsia kwa uanaharakati wako. Inafaa pia kupitia haraka hoja kuu ulizozisoma katika vikao vya awali. Tunakushauri upitie kwa kifupi slaidi za uwasilishaji ambazo umefanya hapo awali - lakini ikiwa huna wakati, kurejelea haraka kwa mawasilisho yako ya kikao kilichopita kunasaidia kukumbusha kikundi kwa kasi kuhusu masuala ambayo umeangazia.

AU

Ikiwa unafanya kikao hiki kama sehemu ya warsha kamili ya mafunzo

Ikiwa unasimamia kikao hiki kama sehemu ya warsha kamili ya mafunzo (kumaanisha kimejumuishwa na vikao vingine), basi tunapendekeza sasa uwe wakati wa kuwa na shughuli ya kulisimua, na hutahitaji kufanya makumbusho kamili au kikao cha kurejelea masuala mliyoyapitia hapo awali. Unaweza tu kuwasilisha malengo makuu ya kikao, mada kuu ambazo utajadili, na ukumbusho mfupi kuhusu unyeti na umuhimu wa kila mtu kuheshimu maoni ya mwenzake.

Shughuli ya kulisimua: Ununuzi sokoni

Shughuli ya kulisimua husaidia kila mtu kujenga urafiki na kuunda mazingira ya kufurahisha na ya starehe. Pia, ni nzuri kwa kuhakikisha watu wameamka, wako macho na wako tayari kufanya kazi.

Waeleze kikundi kuwa huu ni mchezo wa kumbukumbu. Panga kila mtu kwenye mduara: chagua mtu wa kuanza shughuli na ueleze kwamba kila mtu anahitaji kuongeza kwenye ununuzi wa wale waliotaja vifaa fulani kabla yao, kwa hivyo lazima wasikilize vizuri. Mtu wa kwanza anasema 'Kwenye soko, ninanunua...' halafu anasema bidhaa anayotaka kununua. Halafu mtu aliye karibu nao anafuata kwa kusema: 'Kwenye soko, nilinunua xxx (ataje kifaa kilichotajwa na mtu aliyezungumza kabla yake) na ninaongeza yyy (ongeza mboga / matunda / bidhaa nyingine ya mboga kwenye kikapu). Kila mtu anafuata kwa mfululizo, akijenga kwenye orodha ya ununuzi, bila kusahau chochote.

Shughuli 2: Majadiliano ya wazi - Jinsia ni nini?

Uliza kikundi cha jumla kiseme kile kinachokujia akilini wanaposikia neno 'jinsia'. Wewe kama mkufunzi unapaswa kuandika kile washiriki wanasema kwenye chati / karatasi. Simamia majadiliano ya wazi kwa dakika 5.



Shughuli 3: Majadiliano ya kikundi - Kumbukumbu za kwanza za jinsia

Waulize washiriki wamgeukie mtu aliyeketi kulia kwao na waungane wawili wawili. Waulize kila kikundi wajadili kwa dakika 10 kumbukumbu yao ya kwanza ambapo waligundua kuwa walikuwa mvulana au msichana, au wakati waligundua tofauti kati ya jinsia, na jinsi hii iliwafanya wahisi. Makundi yote yanapaswa kuandika mazungumzo yao kwenye karatasi. Kila kikundi kinapaswa kushiriki kwa kifupi kile mwenza wao alizungumzia kwenye kundi cha jumla. Fanya hivi kwa dakika 10. Mara baada ya kila mtu kumaliza, uliza ikiwa kuna mtu yeyote anataka kujadili kitu kingine chochote na uwe na dakika chache kwa majadiliano ya wazi. Hakikisha umeshiriki uliyoyapitia pia.

Shughuli 4: Uwasilishaji wa mkufunzi - Jinsia ni nini?

Unapofanya kazi ya kushughulikia kuozwa kwa watoto, ni muhimu kuelewa ni vipi kanuni za kijinsia huchangia katika kudumisha mazoea ya kuozwa kwa watoto. Jinsia haina maana sawa na jinsi. Jinsi inahusu sifa za kibiolojia za wanaume na wanawake. Kwa mfano: wanaume hutoa manii, wanawake hutoa mayai. Jinsia inahusu majukumu na tabia zilizoainishwa kijamii kwa wanaume na wanawake. Tunapotarajia wanaume na wanawake kutenda mambo kwa njia fulani, kwa sababu tu ni wanaume na wanawake, basi tunafuata 'kanuni za kijinsia'. Tamaduni tofauti zinaweza kuwa na kanuni tofauti za kijinsia au njia tofauti ambazo wanatarajia wanaume na wanawake waenende. Kwa mfano, tamaduni zingine zinataraajia wanawake kukaa nyumbani na kufanya kazi za nyumbani, wakati wanaume wanapaswa kwenda kufanya kazi. Kanuni hizi pia huitwa majukumu ya kijinsia, ambayo ni majukumu maalum wanaume na wanawake wanatarajiwa kutekeleza katika jamii au hata katika familia. Jinsia inahusu sifa za kiuchumi, kijamii na kitamaduni na fursa zinazoambatana na kuwa mwanamume au mwanamke katika jamii fulani. Inabainisha yale mwanamume au mwanamke anaweza kufanya, anaweza kuwa au anaweza kupata katika jamii maalum. Majukumu ya kijinsia hutofautiana kutoka kizazi hadi kingine, wakati mmoja hadi mwingine na utamaduni mmoja hadi mwingine.

- Watu huzaliwa wakiwa wa kike au wa kiume, lakini hufunzwa jinsi ya kuwa wasichana na wavulana ambao baadaye wanakua wanawake na wanaume.
- Majukumu ya kijinsia ni tabia zilizofunzwa katika jumuiya, jamii au kikundi kingine fulani kingine cha kijamii. Hizi huamua shughuli, kazi na majukumu ambayo yanaonekana kuwa yanafaa wanaume au wanawake.
- Wasichana na wavulana wanafundishwa tabia na mitazamo sahihi, majukumu na shughuli zinazofaa kwao, na jinsi wanavyopaswa kuingiliana na watu wengine. Tabia hii iliyofunzwa ndiyo inayounda utambulisho wa kijinsia, na huamua matarajio na majukumu ya kijinsia.
- Majukumu ya kijinsia yanatofautiana sana kutoka utamaduni mmoja hadi mwingine, na kutoka kikundi kimoja cha kijamii, kisiasa na kiuchumi hadi kingine ndani ya utamaduni mmoja.
- Majukumu ya kijinsia pia yanatofautiana wakati unavyobadilika. Majukumu yaliyofafanuliwa kijamii kwa wasichana na wavulana na wanawake na wanaume katika jamii moja yanaweza kubadilika kwa vizazi, na katika jamii zingine zinaweza kuendelea kwa muda mrefu kwa njia ile ile. Kwa mfano, huko Misri ya Kale wanaume walikaa nyumbani na kufanya ufumaji. Wanawake waliendesha bishara za familia. Wanawake walirithi mali na wanaume hawakurithi. Katika Misri ya kisasa, majukumu haya yamebadilika.



AU



AU



Mifano ya Uwasilishaji: Jinsia

- **Jinsia** inahusu matarajio na majukumu ya kiuchumi, kijamii na kitamaduni yaliyopewa mwanamume au mwanamke katika jamii.
- **Majukumu ya kijinsia** yanaweza kubadilika na ni tofauti kutoka kizazi hadi kingine na utamaduni hadi utamaduni mwingine. Kwa mfano, katika Misri ya Kale wanaume walikaa nyumbani na kufanya ufumaji. Wanawake waliendesha biashara za familia. Wanawake walirithi mali na wanaume hawakurithi. Katika Misri ya kisasa, majukumu haya yamebadilika kabisa.
- **Inabainisha ni nini mwanamume au mwanamke anaweza kufanya**, kukuwa, au kupata katika jamii maalum.

Tofauti kati ya jinsi na jinsia

JINSI

- **Ni ya kibiolojia** (ya kimwili).
- **Inapatikana kwa kuzaliwa** (ni ya asili na inahusu tofauti zinazoonekana katika viungo vya uzazi vya wavulana na wasichana na tofauti zinazohusiana katika kazi ya uzazi).
- **Haiwezi kubadilishwa** - isipokuwa kwa njia ya kubadilisha homoni au upasuaji.

JINSIA

- **Ni ya kitamaduni.**
- **Hufunzwa kupitia ujamaa** (imeundwa na jamii na kwa hivyo inafundishwa na kujifunza).
- **Inaweza kubadilishwa na kupingwa:** wanawake wanaweza kufanya kazi kama wahandisi, marubani nk.

Shughuli 5: Majadiliano ya wazi - Usawa wa kijinsia ni nini?

Katika mazungumzo ya wazi na kikundi cha jumla, waulize washiriki wafikirie maoni yao kuhusu maneno usawa wa kijinsia. Andika wanachosema kwenye karatasi ya chati. Ruhusu dakika 10 kwa majadiliano au kwa maswali yoyote waliyo nayo.


Shughuli 6: Majadiliano ya kikundi - Ukosefu wa usawa wa kijinsia

Gawanya washiriki katika vikundi viwili: gawanya idadi yao katikati - kikundi kimoja kila upande wa chumba. Waulize wajiadili kile wanachofikiria ni mifano katika maisha yao ya ukosefu wa usawa wa kijinsia. Wanapaswa kufikiria mifano kutoka kwa viwango na muktadha tofauti: kama mtu binafsi, familia, jamii na ulimwenguni. Waeleze wachague mwandika muhtasari ambaye atawasilisha tena kwa kikundi cha jumla. Wana dakika 10 kujadili mifano.

Waombe kila kikundi watoe maoni yao kuhusu matokeo kuu au mifano waliyojadili. Kisha fungua sakafu kwa uchunguzi kamili wa mifano tofauti, mkiangazia ni kwa nini hizi zinatokea na athari zake ni zipi. Kwa mfano, ikiwa kikundi kinaandika kwamba kuna ukosefu wa usawa katika fursa zilizopewa wanawake kazini, basi uliza kikundi kichunguze ni fursa zipi wanakatazwa, kwa nini hili linatokea, na athari za ukosefu huu wa usawa. Ruhusu dakika 15 kwa majadiliano haya na uchunguzi.

Shughuli 7: Uwasilishaji wa mkufunzi - Je, kuna tofauti gani kati ya ukosefu wa usawa wa kijinsia na usawa wa kijinsia?

Wewe, kama mkufunzi, sasa unapaswa kutoa uwasilishaji mfupi kuhusu kile unachomaanisha unaposema usawa wa kijinsia, na sababu na athari za ukosefu wa usawa wa kijinsia. Una dakika 10 kwa uwasilishaji wako. Hapo chini tumejumuisha maoni kuu kwa kila dhana, na pia mifano ya slaidi za uwasilishaji ambazo unaweza kuonesha kikundi.



Usawa wa kijinsia

- Usawa wa kijinsia haimaanishi tu idadi sawa ya wanaume na wanawake au wavulana na wasichana wanaoshiriki katika shughuli zote, au kwamba wanawake na wanaume ni sawa. Inamaanisha kuwa wanaume na wanawake wanafurahia kutambuliwa na kupokea hadhi sawa katika jamii na wanapaswa kuonyeshwa heshima sawa.
- Inamaanisha kwamba kufanana na pia tofauti zetu zinatambuliwa na kuthaminiwa kwa usawa ili tuweze kufikia uwezo wetu wote wa kibinadamu. Hii inamaanisha sisi sote tunaweza kushiriki, kuchangia na kufaidika kwa usawa kutokana na maendeleo ya kitaifa, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kitamaduni.
- Usawa wa kijinsia inamaanisha kuthamini kwa usawa majukumu ya wanawake na wanaume, na michango yao, shughuli na kazi wanazofanya.
- Inafanya kazi kukomesha fikra potovu na ubaguzi ili jinsia zote ziweze kuchangia kwa usawa na kufaidika na maendeleo ya kiuchumi, kijamii, kitamaduni na kisiasa ndani ya jamii yao.
- Hoja kuu ya usawa wa kijinsia ni kwamba tofauti kati ya wanawake na wanaume haipaswi kuwa na athari mbaya kwa hali zao za maisha au kuzuia mgawanyo sawa wa madaraka kati ya wanawake na wanaume katika nyanja mbalimbali za maisha.
- Usawa wa kijinsia unahusu fursa na matokeo sawa kwa wanawake na wanaume. Hii inajumuisha kuondoa kila aina ya ukosefu wa usawa katika upatikanaji wa rasilimali, fursa na huduma, na kukuza haki sawa.
- **Usawa haimaanishi kuwa wanawake wanapaswa kuwa sawa na wanaume. Kukuza usawa kunatambua kuwa wanaume na wanawake wana majukumu na mahitaji tofauti, na inasisitiza umuhimu wa kuzingatia haya katika miradi na mipango ya maendeleo.**

Ukosefu wa usawa wa kijinsia ni nini?

- Wanaume na wanawake ni tofauti kimaumbile lakini ni tafsiri ya tofauti hizi kijamii, kiuchumi, kisiasa na kisheria ndizo zinazosababisha ukosefu wa usawa kati yao.
- Ubaguzi dhidi ya wanawake na wasichana - kama vile dhuluma ya kijinsia, ubaguzi wa kiuchumi, ukosefu wa usawa kwa afya ya uzazi na mazoea hasi ya jadi - unabaki kuwa aina ya kutokuwepo kwa usawa.
- Ukosefu wa usawa katika mazingira / jamii: wakati kazi ya wanaume ina hadhi na inatambuliwa kuwa ya thamani na muhimu kuliko kazi ya wanawake (kama vile kulea watoto, kupika na kusafisha). Hii pia hufanyika wakati wanawake wanapata ufikiaji mdogo wa huduma (kwa mfano, elimu na afya), na wakati kuna dhuluma moja kwa moja dhidi ya wanawake na wasichana kwa sababu ya jinsia yao.
- Kukosekana kwa usawa wa kiuchumi: wanawake wanakosa usawa wa rasilimali za kiuchumi, kama fursa za mafunzo ya ustadi, fedha, mikopo, kazi na ardhi, na nafasi ndogo za ajira na maendeleo ya kazi.
- Kukosekana kwa usawa wa kisiasa: wanawake wanawakilishwa kwa viwango vidogo katika ngazi zote za maamuzi rasmi katika jamii, na haswa katika viwango vya mkoa na kitaifa.
- Kukosekana kwa usawa wa kisheria: mfumo wa sheria katika nchi nyingi huwabagua wanawake katika nyanja za sheria za familia, urithi, mali na umiliki wa ardhi, uraia na sheria ya jinai. Hivyo basi, kesi za mashtaka zinazohusu dhuluma dhidi ya wanawake ni ngumu sana kutatua kwa njia ya usawa.



AU



AU



Uwasilishaji wa mfano: Usawa wa kijinsia

- Usawa wa kijinsia haimaanishi kuwa wanawake na wanaume ni sawa, lakini kwamba wana thamani sawa na wanapaswa kuzingatiwa kwa usawa.
- Kuthamini sawa majukumu ya wanawake na wanaume.
- Hii ni muhimu katika kuondoa vizuizi vinavyokithirisha ubaguzi na chuki.
- Mgawanyo sawa wa madaraka kati ya wanawake na wanaume.
- Kuondoa kila aina ya ukosefu wa usawa katika upatikanaji wa rasilimali, fursa na huduma, na kukuza haki sawa.
- Usawa unatambua kuwa wanaume na wanawake wana majukumu na mahitaji tofauti.

Shughuli 8: Uwasilishaji wa mkufunzi - Uchambuzi wa kijinsia

Eleza kwamba sasa tutajifunza kuhusu uchambuzi wa kijinsia. Una dakika 10 kwa uwasilishaji huu.

Je, uchambuzi wa kijinsia ni nini?

- Uchambuzi wa kijinsia ni njia ya kutafiti na kupata masuala muhimu ambayo yanaunda au kutekeleza ukosefu wa usawa wa kijinsia. Hii ni ili uweze kuelewa kabisa vichochezi na sababu ili ziweze kushughulikiwa vizuri na kurekebisha.
- Inakusaidia kuelewa tofauti zisizo sawa kati ya wanaume na wanawake. Inakusaidia kutambua, kuelewa na kuelezea mapungufu ya usawa kati ya wanaume na wanawake ambayo yapo nyumbani, katika jamii na nchi.
- Husaidia kukuonesha jinsi tofauti hizi za kijinsia na uhusiano wa mamlaka zinavyoathiri (na mara nyingi huimarisha) kuoza kwa watoto.
- Ni njia ya utafiti inayoangalia viwango tofauti vya mamlaka ambayo wanawake na wanaume wanashikilia; Mahitaji yao tofauti, vizuizi, na fursa; Na athari za tofauti hizi katika maisha yao.

Wakati wa kufanya uchambuzi wa kijinsia, kuna mambo matano makuu ambayo unaweza kuangalia ili kuelewa jukumu au hadhi ya wanaume na wanawake.

- Sheria, sera na kanuni katika jamii.
- Tamaduni na imani.
- Dhima za kijinsia, majukumu na wakati uliotumika kwa kila moja.
- Ufikiaji, au udhibiti wa rasilimali.
- Mifumo ya mamlaka na uamuzi.

Uchambuzi wa kijinsia utakusanya, kuchambua na kutafsiri habari kuhusu hali maalum kwa kuangalia dhima, majukumu, mahitaji na fursa za wasichana na wavulana / wanawake na wanaume. Hii inakusudia:

- Kutambua tofauti kati ya vikundi.
- Kuelewa ni kwa nini tofauti hizi zipo.
- Kuangalia ni matendo/masuala gani haswa hushawishi kuozwa kwa watoto.

Maswali kadhaa ya kujiuliza unapofanya uchambuzi wa kijinsia unaolenga kuozwa kwa watoto:

- Je, ni vikundi gani vya wasichana vinaathiriwa na kuozwa kwa watoto?
- Je, ni nani aliye katika tishio kubwa zaidi?
- Je, wasichana huwa na umri gani wakati wanaozwa?
- Je, wako shuleni au la?
- Je, wao ni sehemu ya kikundi kidogo au kikundi kilichotengwa katika jamii?



AU



AU



Uwasilishaji wa mfano: Je, uchambuzi wa kijinsia ni nini?

- Uchambuzi wa kijinsia husaidia kutambua masuala muhimu yanayochangia ukosefu wa usawa wa kijinsia.
- Inaangazia mapungufu yoyote kati ya wanaume na wanawake ambayo yapo katika nyumba, jamii na nchi.
- Inaelezea jinsi kanuni za kijinsia na uhusiano wa mamlaka zinavyoathiri (na mara nyingi kuimarisha) kuozwa kwa watoto.
- Huchunguza tofauti za majukumu na kanuni kati ya wanawake na wanaume, wasichana na wavulana: viwango tofauti vya madaraka waliyonayo; mahitaji yao tofauti, vizuizi, na fursa; na athari za tofauti hizi katika maisha yao.



Shughuli 9: Kazi ya vikundi - Kufanya uchambuzi wa kijinsia

Mweke kila mmoja katika vikundi vidogo vya washiriki wanne au watano (nambari hii itategemea ni watu wangapi unao katika mafunzo yote na ni vikundi vingapi unataka). Kama ulivyofanya katika Moduli 1, Kikao cha 2, Zoezi la 2.2, zigawanye kwa kumfanya kila mtu ahesabu moja, mbili, tatu na kadhalika, sitisha kwa idadi ya vikundi unavyotaka kwenye chumba, na kisha anayefuata kuhesabu arudi kwa kusema moja tena. Baada ya haya, wataingia katika vikundi kwa kuunganisha wale wote walioita 'moja' pamoja, wote walioita 'mbili' pamoja na kadhalika. Itachukua takriban dakika 5 kwao kuingia kwenye vikundi.

Wape kila kikundi nakala ya jedwali la mienendo ya kijinsia utakayopata kwenye kurasa zifuatazo. Wakumbushe mambo matano makuu ambayo unaweza kuangalia ili kutathmini hadhi ya wanaume na wanawake katika jumuiya au jamii fulani - haya yameorodheshwa katika Shughuli 8.

Eleza kwamba kila kikundi kinapaswa kukamilisha uchambuzi wa kijinsia kwa kujibu maswali katika hati hiyo. Ikiwa hawajui majibu ya maswali, waulize wafikirie kuhusu jinsi wanaweza kujua suala zaidi: wanapaswa kumuuliza nani au kwenda wapi kupata habari? Wana dakika 20 kupitia maswali na kujaribu kukusanya majibu yao.

Baadaye katika mazungumzo ya dakika 10 ya wazi, uliza kila mtu yale ambayo wamejifunza kuhusu majukumu ya kijinsia katika jamii yao. Waulize ikiwa wanaweza kuona jinsi masuala ya kijinsia na kuozwa kwa watoto zinahusiana. Ruhusu hii iwe nafasi wazi ambapo wanaweza kutoa maoni yao au kuuliza maswali yoyote.

Kutumika kwa shughuli 9: Kazi ya vikundi - Kufanya uchambuzi wa kijinsia

Jedwali la mienendo ya kijinsia: uchambuzi wa kijinsia unaolenga uchunguzi wa kuozwa kwa watoto

Jedwali hili linaonyesha uchambuzi wa kina wa kijinsia katika maeneo hayo matano. Kupata majibu ya maswali haya kutakusaidia kubuni mpango imara na wenye ufanisi zaidi.

Maeneo ya uchambuzi wa kijinsia	Maswali ya kukuongoza	Nyenzo ambazo zinaweza kukusaidia kupata majibu
1. Sheria, sera na kanuni	<ol style="list-style-type: none"> Je, kuna sheria za kitaifa kuhusu umri wa chini wa ndoa, vyeti vya ndoa na usajili wa kuzaliwa ili kuzuia ubaguzi wa kijinsia? Je, sheria hizi zinatekelezwa katika viwango vya kitaifa na vya mitaa? Je, wanawake na wasichana wanaweza kupata haki (kama vile polisi na mahakama) au wanajitahidi kufanya hivyo? Je, watu, familia na jamii wanajua sheria? Je, sheria na sera zinaathiri vipi maamuzi kuhusu ndoa katika viwango vya mitaa? Au sheria ya kimila inaruhusu kuozwa kwa watoto, kupingana na sheria ya kitaifa? Kwa mfano, ikiwa sheria ya kitaifa inasema umri wa chini wa ndoa, je, sheria hii ndio hasa watu wanasikiliza? 	<ol style="list-style-type: none"> Watunga sera, taasisi za kisheria, AZAKi zinazoshughulikia suala hilo. Unaweza pia kuzitafuta kwenye tovuti au tembelea habari maalum ya nchi kwenye tovuti ya Girls Not Brides. Ongea na watu mbalimbali ambao wanaweza kukusaidia: majaji, polisi, maafisa wa serikali na wafanyakazi wa serikali, taasisi za kisheria za mitaa na AZAKi zinazohusika na suala hili au kufanya kazi katika jamii yako, wanawake na wasichana wenyewe. Viongozi wa jadi, dini na jamii, serikali za mitaa, viongozi wa dini, wazee, wanawake na wasichana, wanaume na wavulana.
2. Itikadi na imani za kitamaduni	<ol style="list-style-type: none"> Je, ni mazoea gani yanayokubalika na imani kuhusu majukumu ya wasichana na wanawake kama wake na akina mama - na majukumu ya wavulana na wanaume kama waume na kina baba? Je, ni mazoea gani ya kitamaduni na mila yameunganishwa na ndoa? Hii inaweza kujumuisha bei ya kuozwa, mahari, ukeketaji / ukataji wa kike (FGM / C), ndoa za wake wengi, utekaji nyara wa wake na usisitizaji wa ubikira wa kike. Je, ndoa inaashiria shughuli ya kifedha, kama mahari au bei ya kuozwa? 	Viongozi wa jadi, dini na jamii; Wazee; Wazazi; Wanawake na wasichana; Wanaume na wavulana.

<p>3. Dhima za kijinsia, majukumu na wakati uliotumika kwa kila moja.</p>	<ol style="list-style-type: none"> 1. 1. Je, wanawake na wasichana hutumia muda gani kufanya kazi za nyumbani na za matunzo? Hii inaweza kujumuisha kuwatunza ndugu wadogo, wazazi wazee, au wanafamilia walio na changamoto za kimwili. Je, hii inalinganishwaje na wakati ambao wanaume na wavulana hutumia kufanya kazi hizi? Je, wasichana wamewahi kutolewa shuleni kufanya kazi za nyumbani na matunzo? 2. 2. Je, ni kwa jinsi gani wanawake na wasichana ambao walikuwa wameolewa wakiwa wadogo (kabla ya miaka 18) hutumia wakati wao tofauti na wanawake na wasichana ambao hawajaolewa? Na kuna tofauti yoyote kati ya jinsi wasichana na wavulana wanavyotarajiwa kutumia wakati wao? 	<p>Wanawake na wasichana, wanaume na wavulana, wazee wa familia.</p>
<p>4. Ufikiaji na udhibiti wa nyenzo</p>	<ol style="list-style-type: none"> 3. 1. Je, kuna tofauti gani kati ya wanaume na wanawake katika suala la kufikia mapato, kumiliki ardhi au kupata mali na rasilimali zingine (kama simu)? 4. 2. Je, wanawake na wasichana ambao wamepitia kuozwa kwa watoto wanakabiliwa na kutengwa na jamii? Kwa mfano, je, hawaruhusiwi kuona marafiki wao au kwenda shule? 	<p>Wanawake na wasichana, wanaume na wavulana.</p>
<p>5. Mifumo ya mamlaka na uamuzi</p>	<ol style="list-style-type: none"> 5. 1. Ni nani katika familia au jamii hufanya maamuzi kuhusu ikiwa, wakati gani, na nani msichana anapaswa kuoa? Je, ni jamii gani na viongozi wa dini wanaathiri maamuzi kuhusu ndoa? 6. 2. Je, umri wa ndoa na tofauti ya umri kati ya wenzi huathiri vipi uhusiano? Ni nani ana mamlaka na anashikilia maamuzi yote katika ndoa? 	<p>Viongozi wa jadi, dini na jamii; Wazee; Wazazi; Wanawake na wasichana; Wanaume na wavulana.</p>



Picha © Samantha Sophia/ Unsplash

Shughuli 10: Kujadiliana na mazungumzo wazi - Kufanya kazi na wanaume na wavulana

Kama majadiliano ya kikundi, waulize washiriki waeleze ni kwa nini tunapaswa kufanya kazi na wanaume na wavulana, na haswa kwa nini tunapaswa kuwashirikisha tunaposhughulikia kuozwa kwa watoto. Wape wito wa kusema majibu yao kwa sauti na unaweza kuyaandika kwenye karatasi ya chati ili kurekodi maoni yao. Una dakika 5 tu kuwa na mawazo ya haraka kuhusu hili.

Shughuli 11: Uwasilishaji wa mkufunzi - Kwa nini ufanye kazi na wanaume na wavulana?

Una dakika 10 za kuwasilisha masuala yafuatayo kuhusu kufanya kazi na wanaume na wavulana wakati unaposhughulikia kuozwa kwa watoto katika jamii.

Kwa nini ufanye kazi na vijana?

Wavulana pia huozwa wakiwa watoto, na wanaume milioni 156 walio hai leo walioa kabla ya umri wa miaka 18. Lakini wasichana wameathiriwa kwa kiasi kikubwa na kuozwa kwa watoto, na wana uwezekano zaidi ya mara saba kuathiriwa na mazoea hayo. Ni muhimu kukumbuka kwamba vijana ni wahasiriwa na pia mawakala wa mabadiliko.

Utafiti wa hivi karibuni umeonyesha kuwa kuwashirikisha wavulana na wanaume ni muhimu katika kujenga usawa wa kijinsia. Ili kuboresha usawa kati ya wanaume na wanawake, ni muhimu kwamba wanaume na wavulana wabadilishite mitazamo na mazoea yao kwa wanawake na wasichana. Ikiwa tunataka kukomesha kuozwa kwa watoto, basi wavulana na wanaume lazima wachukue jukumu muhimu katika kufanikisha hili. Ni muhimu waelewe na waamini kuwa haya ni mazoea mabaya. Kuwaacha wanaume na wavulana nje ya mpango wowote kutamaanisha kuwa ni sehemu ndogo tu za shida zinazopatikana kwa wanawake na wasichana wadogo ndizo zitashughulikiwa. Shida kuu bado haitakuwa imeshughulikiwa, kama vile uhusiano wa mamlaka uliopo kati ya wanaume na wanawake.

Ili kukomesha kuozwa kwa watoto, lazima tuelewe majukumu ya kitamaduni na jinsia katika jamii ambayo inachangia mazoea haya. Katika nchi nyingi, wanaume na wavulana wamejumuiika kuchukua jukumu la kutafuta riziki, kuwa na mamlaka na kufanya maamuzi mengi ya kifamilia. Wanawake wanalelewa kuendesha mambo ya nyumbani: kupika, kusafisha, kupata watoto na kuwatunza.

Kukomesha kuozwa kwa watoto basi kunahitaji kuchunguza jukumu la kila mtu katika jamii na kufanya kazi kwa bidii ili kubadilisha kanuni na tabia za kijamii katika viwango vyote vya jamii. Akina baba, kaka, waume, wakuu wa vijiji, viongozi wa dini, waamuzi - ili tabia hii potovu iishe, tunahitaji kufanya kazi pamoja na kila mtu, kupata msaada wa wanaume / wavulana wote ambao wanajua ni vibaya, na kushirikiana kuwashawishi wale wote ambao hawajui. Ni muhimu kushirikisha wanaume na wavulana katika kukomesha kuozwa kwa watoto kwa sababu:

- Kuozwa kwa watoto sio suala la wanawake au wasichana pekee.
- Kama watoa maamuzi na waume wa siku zijazo, wanaume na wavulana ni kiini cha juhudi zozote za kukomesha kuozwa kwa watoto.
- Wazee wa dini na viongozi wa jamii mara nyingi ndio wafanya maamuzi muhimu katika jamii ambapo ndoa za mapema au kuozwa kwa watoto ni kawaida. Mara nyingi huwa ni wanaume. Kushirikisha na kuwaelimisha wanaume hawa wenye mamlaka ni ufunguo wa kubadilisha mitazamo ya jamii kuhusu kuozwa kwa watoto.
- Matarajio ya kijamii kuhusu maana ya kuwa mwanamume au mvulana huamuru jinsi wanaume na wavulana wanavyoenenda.
- Wanaume na wavulana wanapaswa kuchunguza majukumu ya kijinsia.
- Wajibu kama baba, mume, mwana na kaka zinafaa kuhamia kuwa zenye matunzo, zinazounga mkono na zisizo na vurugu, zenye kugawa kazi za nyumbani na kufanya maamuzi.
- Wanaume na wavulana hawana nafasi ya kuhoji kanuni hizi za kijinsia.
- Wanaume na wavulana wana ushawishi wa moja kwa moja katika maisha ya wanawake na wasichana.
- Ikiwa hatuwashirikishi wanaume na wavulana hatuwezi kuleta mabadiliko kwenye masuala nyeti kama kuozwa kwa watoto.
- Wanaume na wavulana wanahitaji kujua kuhusu haki za wasichana na jinsi ndoa za mapema zinaweza kuwa na madhara kwa afya na furaha yake pamoja na kuharibu familia.



AU



AU



Uwasilishaji wa mfano: Kushiriki wanaume na wavulana

- Sote tunahitaji kuelewa kanuni tatanishi za kijinsia na kitamaduni zinazoendeleza utamaduni wa kuozwa kwa watoto. Kuozwa kwa watoto sio tu suala la wanawake / wasichana.
- Waamuzi katika jamii / nyumbani kawaida ni wanaume. Kama watoa maamuzi na waume wa siku za usoni, wanaume na wavulana ni msingi wa juhudi zozote za kumaliza kuozwa kwa watoto.
- Wanaume na wavulana wamelelewa kuchukua jukumu la kutafuta riziki, kuwa na mamlaka na kufanya maamuzi mengi ya kifamilia. Wanawake wanalelewa kutunza nyumba (kupika, kusafisha, kupata watoto na kuwatunza).
- Jukumu la kitamaduni la baba, mume, mwana na kaka linahitaji kubadilika kuwa la matunzo, linalounga mkono na lisilo na vurugu, zenye kugawa kazi za nyumbani na kufanya maamuzi.
- Wanaume na wavulana wanahitaji kuchunguza na kubadilisha majukumu ya kijinsia.
- Wanaume na wavulana wana ushawishi wa moja kwa moja katika maisha ya wanawake na wasichana.


Shughuli 12: Hitimisho na kufunga kikao

Kama vikao vingine vya awali, tumia dakika 10 za mwisho wa warsha kumaliza majadiliano na upeane muda wa kushughulikia maswali yoyote ambayo kikundi kinaweza kuwa nayo. Washukuru kwa ukakamavu wao na bidii katika kikao, na ufanye makumbusho ya haraka ya masuala kuu ambayo umezungumzia.





Picha © Graham Crouch / Girls Not Brides



Moduli 3: Chukua hatua Imarisha mkakati wa uanaharakati

Muhtasari wa Moduli

- Kikao cha 1: Malengo na madhumuni - kufafanua mabadiliko unayotaka kuona.
- Kikao cha 2: Kuunda rasimu ya mikakati ya uanaharakati na kuunda jumbe.

Moduli 3 - Kikao 1

Malengo na madhumuni



Lengo

Kufafanua mabadiliko unayotaka kuona na hatua unazohitaji kufikia mabadiliko hayo.



Idadi ya washiriki: Chini ya 24



Wakati unaohitajika: Saa 1 Dakika 20



Muhtasari wa kikao

- Jifunze jinsi ya kufafanua mabadiliko unayotaka kuona
- Jinsi ya kuweka malengo na madhumuni yako
- Je, maisha yako ya baadaye unayotamani ni yapi?
- Jinsi ya kufikia mabadiliko unayohitaji



Vitu vya kuandaa mapema

- Soma maelezo ya usuli na uyajue vizuri ili uwe na ujasiri wa kuyawasilisha kwa kikundi cha jumla
- Slaidi za uwasilishaji (za kielektroniki au kwenye karatasi ya chati)
- Jizoeze shughuli ya kusisimua ikiwa utafanya na kikundi



Vifaa vinavyohitajika

- Magazeti, makasi na utepe
- Karatasi za chati
- Kalamu za alama au kalamu nene

Shughuli	Wakati uliotengwa	Muhtasari
1	Dakika 5	Karibu • Kutambulishana upya na makumbusho (ikiwa hiki ni kikao cha pekee) AU • Shughuli ya kusisimua na utangulizi mfupi wa lengo la kikao (ikiwa unafanya kikao kwa mfululizo baada ya Moduli 2)
2	Dakika 35	• Kazi ya vikundi: Je, ni maisha yapi ya usoni unayotamani?
3	Dakika 15	• Uwasilishaji wa mkufunzi: Kuweka malengo na madhumuni
4	Dakika 15	• Kazi ya vikundi: Kufafanua lengo lako - ni mabadiliko gani unayotaka kuona?
5	Dakika 10	Majadiliano ya hitimisho na kufunga kikao

3.1 Mwongozo wako wa mkufunzi

Shughuli 1: Utangulizi wa kikao, tahadhari ya masuala nyeti na ulinzi

Kama mkufunzi, anza kikao kwa muhtasari wa moduli na mpango wa kikao uliopewa kwenye ukurasa uliopita. Kisha, rejelea tahadhari ya unyeti na ulinzi (ambayo imeainishwa mwanzoni mwa mwongozo wa mkufunzi). Hii ni kuhakikisha kwamba vikao vyote vinaanza kwa njia ile ile, na kwamba unakumbusha kikundi chako umuhimu wa ulinzi kila wakati.

Ikiwa hiki ni kikao cha pekee

Karibisha kikundi chako pamoja. Kama ilivyo kwenye vikao vya awali katika Moduli 1 na 2, ikiwa hiki ni kikao cha pekee (kumaanisha unafanya kikao hiki siku nyingine au wiki baada ya kikao kilichopita) basi mwombe kila mtu ajitambulisha ili wote wakumbuke majina ya kila mmoja. Wakumbushe ni kwa nini sisi sote tuko pamoja na haraka, pitia makumbusho ya sheria za msingi mlizoainisha pamoja na tahadhari ya unyeti. Eleza kikundi kusudi la kikao cha warsha hii. Ni muhimu pia kupitia haraka vidokezo kuu ulivyoangazia kwenye vikao vya awali. Tunapendekeza upitie kwa kifupi slaidi za uwasilishaji za hapo awali - lakini ikiwa huna wakati, basi kurejelea haraka uwasilishaji wako wa kikao kilichopita utasaidia kukumbusha kikundi kwa kasi kuhusu masuala ambayo umeangazia.

AU ...

Ikiwa unafanya kikao hiki kama sehemu ya warsha kamili ya mafunzo

Ikiwa unasimamia kikao hiki kama sehemu ya warsha kamili ya mafunzo (kumaanisha kimejumuishwa na vikao vingine), basi tunapendekeza sasa uwe wakati wa kuwa na shughuli ya kulisimua, na hutahitaji kufanya ukumbusho kamili au kikao cha kurudia mliyoyapitia hapo awali. Unaweza tu kuwasilisha malengo makuu ya kikao, mada kuu ambazo utajadili, na ukumbusho mfupi kuhusu unyeti na umuhimu wa kila mtu kuheshimu maoni ya mwenzake.

Shughuli ya kulisimua: Tembo anasema...

Shughuli ya kulisimua husaidia kila mtu kujenga urafiki na kuunda mazingira ya kufurahisha na ya starehe. Pia, ni nzuri kwa kuhakikisha watu wameamka, wako macho na wako tayari kufanya kazi.

- Mwambie kila mtu asimame kwenye duara au safu mbili zikiangaliana. Eleza sheria za mchezo, ambayo ni yafuatayo. Unaposema: 'Tembo anasema...' kisha kuongeza shughuli, kama 'simama kwa mguu mmoja,' kikundi lazima kifuatake amri ya tembo na kisha kukaa katika nafasi ambayo umewaambia.
- Lakini ikiwa unatoa amri kwa shughuli bila kusema 'Tembo anasema...' wanahitaji kupuuza amri (na kubaki jinsi walivyokaa). Wakati wa mazoezi! Kwa mfano, sema: 'Tembo anasema... gusa sikio lako la kushoto kwa mkono wako wa kulia' - na utumie mkono wako kana kwamba ni mkono wa tembo kugusa sikio lako.
- Kisha sema: 'Jikune juu ya kichwa na tumbo kwa wakati mmoja.' Washiriki wanapaswa kuweka mkono wao wa kulia kwenye sikio la kushoto kwa sababu haukuongeza amri 'Tembo anasema ...' Endelea kucheza hadi washiriki wawe na burudani ya kutosha.

Shughuli 2: Kazi ya kikundi – Je, unatamani maisha ya aina gani ya siku za usoni?

Wagawanye washiriki wako katika vikundi vidogo (washiriki wanne au watano kwa kila kikundi), na uulize kila kikundi wawaze kwamba wamekuwa nje ya nchi kwa miaka kumi. Wamefika kurudi na kugundua kuwa ndoto zao kuhusu jinsi jamii inapaswa kuwa, baada ya kuondoa shida walizozigundua kuhusu suala la kuozwa kwa watoto, zimetimizwa. Shida zinatatuliwa na jamii inaendelea kama vile walivyotamani mwanzoni. Omba vikundi wachora picha (au wanaweza kutumia picha kutoka kwa majarida) ya jinsi jamii kama hiyo ingeonekana, kwa kutumia rangi, miundo, maneno na / au picha. Waambie wakubaliane na kuweka lengo moja la jamii hiyo bora wanayotamani. Wana dakika 15 kwa jumla kubuni jamii yao kikamilifu, na kujadili mipango yao ndani ya vikundi vyao.

Baadaye, waulize kila kikundi wawasilishe kwa muda mfupi mchoro wao kwa wengine wa kikundi cha jumla. Wakati wa uwasilishaji wao, andika maneno muhimu yanayotokea kutoka kwa mada muhimu zinazoibuka kwenye mawasilisho. Ruhusu dakika 10 kwa jumla kwa vikundi vyote kuwasilisha.

Baada ya kila kikundi kuwasilisha, jaribu kuona ikiwa, kwa kutumia maneno muhimu ambayo umeandika, kikundi kizima kinaweza kupata lengo moja kwa pamoja. Ruhusu dakika 10 kwa majadiliano ya wazi kuhusu taarifa yao ya lengo.

Shughuli 3: Uwasilishaji wa mkufunzi - Kuweka malengo na madhumuni

Huu sasa ni wakati wako wa kuwasilisha kuhusu kuelezea malengo ni nini, jinsi ya kuyaweka, na tunavyomaanisha tunapozungumza kuhusu kuunda malengo SMART. Una dakika 10 kwa uwasilishaji ufuatao. Tumia dakika 5 za mwisho kujibu maswali yoyote au kupitia hoja zozote ambazo kikundi kinaweza kuwa nazo..

Kuweka lengo inamaanisha:

1. Kufafanua mabadiliko ya mwisho unayotaka kuchangia. Lengo ni wazo wazi la ulimwengu unayotaka kuunda - hali ya mwisho unayotaka kuona ikitekelezwa na maono ya mwisho unayotaka kufikia kupitia kazi yako. Inapaswa kuwa ya kuvutia na kuelezea wazi kile unachopigania. Lengo sio jambo ambalo unaweza kufikia peke yako. Kwa mfano, kwa *Girls Not Brides* maono na lengo letu kuu ni: ulimwengu usio na kuozwa kwa watoto ambapo wasichana na wanawake wanafaulu hali sawa na wavulana na wanaume na wanaweza kufikia uwezo wao kamili katika nyanja zote za maisha yao.
2. Kufikiria kuhusu kipimo na kiwango cha matendo yako. Tathmini ni muda gani kila mmoja anaweza kutoa kufikia lengo lako. Yawe ya kuaminika. Kadiri unavyojifunza zaidi, na kujumuisha watu zaidi kufanya kazi nao, ndivyo lengo lako na madhumuni yako yanaweza pia kukua. Unaweza kutaka kulenga kusudi lako kwa jamii au kikundi cha watu maalum, au kuwa na kikundi maalum cha kulenga na kushughulikia masuala yao maalum.
3. Kutathmini kile utafiti wako na uchambuzi wa kijinsia umefichua katika jamii yako. Je, una motisha na shauku ya kushughulikia jambo lipi kama lengo? Je, ni masuala gani maalum kutoka kwa uchambuzi na kutathmini ambayo unaweza kushughulikia?



AU



AU



Mfano wa Uwasilishaji: Ufafanuzi na tofauti kati ya malengo na madhumuni

Lengo

Ufafanuzi

- Lengo kuu ambalo unajitahidi kufikia .
- Hii ndio taswira kuu au maono unayotaka kuona ulimwenguni.
- Hili ni jambo ambalo tunataka kujitahidi kufikia.
- Malengo hayapimiki kabisa au hayashikiki.
- Inafikiwa baada ya muda mrefu.

Mfano: 'Ninataka kufanikiwa kukomesha kuozwa kwa watoto.'

Madhumuni

Ufafanuzi

- Kitu ambacho tunalenga juhudi zetu au matendo kufikia; Ni kusudi au lengo letu.
- Hizi ni hatua ndogo, maalum zaidi ambazo zitakusaidia kufikia lengo lako.
- Lazima ziweze kupimika na ziwe na matokeo yanayoonekana.
- Zinafikiwa kwa muda mfupi au unaoweza kupimika wa utekelezaji

Mfano: 'Ninataka kufanya utafiti kuhusu kuozwa kwa watoto mwishoni mwa mwezi huu.'



AU



AU



Uwasilishaji wa mfano: Kufafanua lengo lako

- Lengo linaweka wazo wazi la ulimwengu unaotaka kuunda.
- Hii ndio hali ya mwisho, inayotakikana au hali ambayo unataka kuona ikitimizwa mwishoni mwa kazi yako.
- Ili uanze, unahitaji kuelezea unachotaka kubadilisha, ni mambo gani kuu unashughulikia, na ni hatua gani unahitaji kuchukua kuyafanikisha.
- Hii inasaidia kuhama kutoka kwa mawazo yasiyoeleweka kikamilifu na kukuwezesha kupanga mipango maalum na mabadiliko yanayoweza kufikiwa katika jamii / nchi yako.
- Malengo ni ya muda mrefu zaidi (kama vile baada ya miaka mitano) lakini kuna hatua mahususi kabisa unaweza kuchukua kuzifikia.

Mara tu unapokuwa na taarifa ya lengo, unahitaji kufikiria masuluhisho halisi dhidi ya kuozwa kwa watoto ambayo yatakusaidia kufikia lengo lako. Yatakuwezesha kufikia lengo kupitia kazi yako, na kusaidia kuzingatia na kuipa kipaumbele kazi yako na yale utahitaji kufanya hivyo. Madhumuni yako yanaonyesha ni mabadiliko gani maalum au matokeo unataka kufikia kwa muda mfupi.



Kama kikundi, wazeni kuhusu madhumuni ambayo yatawasaidia kufikia lengo lenu. Yanapaswa kuwa SMART, ambayo kwa Kiingereza inamaanisha:

S-specific, M- measurable, A- achievable, R- relevant, na T- timed. Kwa Kiswahili, inamaanisha kwamba madhumuni yenu yanafaa kuwa:

- **Maalum/Specific:** yanakueleza haswa ni kiasi gani (nambari wazi - kama vile 40%) ya kile unataka kufikia au kubadilisha (ni tabia gani ya kikundi unayotaka kubadilisha, au ni matokeo gani ungependa kuona kutokana na juhudi zako) na yanajumuisha wakati unaolenga kuyafikia (tarehe wazi ya kufanya kazi - kwa mfano, ifikapo mwaka 2020).
- **Yanapimika/Measurable:** kumaanisha kuwa taarifa inayohusu lengo lako inaweza kukusanywa, kugunduliwa, au kupatikana (angalau kuwe na uwezekano) ili uweze kutathmini athari na kupima mabadiliko yanayotokana na juhudi zako.
- **Yanaweza kufanikishwa/ Achievable:** madhumuni yako yanapaswa kuweza kufanikishwa kwa kweli pamoja na mabadiliko unayotaka kuona. Hii inamaanisha kuwa sio tu madhumuni yenyewe yanawezekana, bali pia kuna uwezekano kwamba kwa pamoja (kufanya kazi pamoja na washiriki) mtaweza kuyafanikisha.
- **Yanahusiana na maono/ Relevant:** kuwe na uelewa wazi wa jinsi madhumuni haya yanavyoingiliana na maono ya jumla ya kikundi au kazi unayofanya.
- **Yametengewa wakati maalum/ Timed:** kikundi chako kinaweza kuandaa ratiba ya wazi kuhusu ni lini madhumuni yatatimizwa. Fanya hii iwe wazi katika kila dhumuni.



AU



AU



Uwasilishaji wa mfano: Kufafanua madhumuni

Unda mkusanyiko wa masuluhisho halisi ya kupambana na tatizo la kuozwa kwa watoto utakazohitaji kufikia lengo lako. Hizi ni hatua ndogo unazohitaji kuchukua kukusaidia kufikia maono yako. Dhumuni linapaswa kuwa SMART, ambayo kwa kimombo inamaanisha: S-specific, M- measurable, A- achievable, R- relevant, na T- timed. Kwa Kiswahili, inamaanisha kwamba madhumuni yako yanafaa kuwa:

- **Maalum:** idadi wazi au lengo la kile unachotaka kufanikiwa au kubadilishwa; Ni matokeo gani unayotaka kuona kutokana na juhudi zako; Na muda unaolengwa kufikia haya.
- **Yanayopimika:** kumaanisha kuwa taarifa inayohusu lengo lako inaweza kukusanywa, kugunduliwa, au kupatikana (angalau kuwe na uwezekano) ili uweze kutathmini athari na kupima mabadiliko yanayotokea kama matokeo ya uingiliaji wako.
- **Yanayoweza kufanikishwa:** linaweza kufikiwa kwa kweli, na kwamba mabadiliko unayotaka kuona yanawezeka kufanikishwa ukifanya kazi pamoja na washiriki.
- **Yanahusiana na maono:** linaingiliana na lengo la jumla la kikundi au kazi unayofanya.
- **Yametengewa wakati maalum:** ratiba ya wazi kuhusu lini madhumuni yatakamilishwa.

Shughuli 4: Kazi ya vikundi - Kufafanua lengo lako: ni mabadiliko gani ungependa kuona?

Mkufunzi wa kikundi:(atasema)

Sasa kwa kuwa tumepitia vikao vingi vya mafunzo, unapaswa kujua masuala kadhaa muhimu, kama vile kuelewa masuala ya msingi kuhusu kuozwa kwa watoto na yale ambayo yanaisababisha. Umetathmini haya katika jamii yako au nchi, na vilevile umefikiria jinsi jinsia inavyoathiri masuala haya na athari zenyewe kwa njia nyingi. Kwa hivyo uko tayari kuchukua hatua na kukuza lengo la kazi yako.

Gawanya kikundi cha jumla katika vikundi vitatu vidogo kwa njia yoyote ya haraka ambayo umetumia katika vikao vya awali. Eleza vikundi wafanye majadiliano ya haraka kuhusu wanachofikiria ni ufafanuzi sahihi wa lengo na madhumuni - na ni hatua zipi wanahitaji kuchukua kuyafikia. Ruhusu dakika 10 kwa majadiliano ya kikundi na kisha dakika 5 za majadiliano ya wazi kuhusu kile walichoona ni muhimu zaidi na maoni yao ni yapi.

Shughuli 5: Majadiliano ya hitimisho na kufunga kikao

Katika dakika 10 za mwisho za kikao, unaweza kuuliza maswali kadhaa kama mazungumzo ya wazi ili kuhakikisha kuwa kila mtu ameelewa maoni ambayo umekuwa ukijadili.

- Lengo ni nini?
- Madhumuni ni nini?
- Kuna tofauti gani kati ya lengo na madhumuni?
- Lengo SMART ni lipi?

Waambie wazungumze na wenzao kuhusu jambo moja kuu ambalo wamejifunza leo, kisha fungua kikao.

Moduli 3 - Kikao 2

Kuunda rasimu ya mikakati ya uanaharakati



Lengo la kikao

Kuunda mkakati wa uanaharakati na kujua ni nini hutengeneza ujumbe mzuri unaolenga 'kichwa, moyo na mikono' ya wasikilizaji wako - jinsi ya kuwafanya wafikiri, wahisi na wachukue hatua. Tunajumuisha maoni kuhusu jinsi ya kufanya kazi na vyombo vya habari na kuelewa jinsi ya kufanya shughuli kama hizo za mawasiliano.



Idadi ya washiriki:
Chini ya 24



Muhtasari wa kikao

- Kuandaa mkakati wa uanaharakati
- Ujumbe ni nini na jinsi ya kukuza ujumbe wenye ufanisi.
- Jinsi ya kutumia mawasiliano kuunda ujumbe wenye nguvu na matokeo



Wakati unaohitajika:
Saa 2 Dakika 5



Vitu vya kuandaa mapema

- Soma maelezo ya usuli na uyajue vizuri ili uwe na ujasiri wa kuyawasilisha kwa kikundi cha jumla
- Slaidi za uwasilishaji (iwe za kielektroniki au kwenye chati)
- Nakala ya jedwali zozote au violezo unazotaka kikundi kitumie
- Jizoeze shughuli ya kulisimua ikiwa utaifanya na kikundi
- Andika maneno machache ya kufurahisha, ya kuchekesha kwenye vipande kadhaa vya karatasi kwa mchezo wa 'Nong'onozea'



Vifaa vinavyohitajika

- Karatasi za chati
- Kalamu za alama au kalamu nene
- Utepe au kitu cha kubandikia karatasi ukutani
- Mawasilisho
- Nakala za jedwali hizo mbili za kuwapa kila mmoja

Shughuli	Wakati uliotengwa	Muhtasari
1	Dakika 10	Karibu • Utangulizi na makumbusho (ikiwa hiki ni kikao cha pekee)
2	Dakika 15	Kazi ya vikundi: Kupata sauti yako na mamlaka
3	Dakika 10	Uwasilishaji wa mkufunzi: Je, mkakati wa uanaharakati ni nini?
4	Dakika 40	Kazi ya vikundi: Kuunda mkakati wako wa uanaharakati
5	Dakika 10	Shughuli ya Kusisimua
6	Dakika 15	Uwasilishaji wa mkufunzi: Kuunda ujumbe wenye ufanisi
7	Dakika 15	Kazi ya vikundi au shughuli ya kulisimua: Mawasiliano madhubuti
8	Dakika 10	Hitimisho na kufungwa kwa kikao

3.2 Mwongozo wako wa mkufunzi

Shughuli 1: Utangulizi

Kama ilivyokuwa katika vikao vingine vyote, karibisha kikundi chako kwa muda mfupi. Anza kikao na muhtasari wa moduli. Eleza kikundi kwamba katika kikao hiki tutaandaa mkakati wa uanaharakati na tuchunguze ni kwa nini mawasiliano ni muhimu kwa mpango wako wa uanaharakati pamoja na jinsi ya kuunda ujumbe maalum. Kisha upitie tahadhari ya unyeti na ulinzi (ambayo imeainishwa mwanzoni mwa mwongozo wa mkufunzi) ili vikao vyote vianze kwa njia ile ile.

Ikiwa hiki ni kikao cha pekee

Karibisha kikundi chako. Kama ilivyokuwa katika vikao vya awali katika Moduli 1 na 2, ikiwa hiki ni kikao cha pekee (kumaanisha unafanya kikao hiki siku nyingine au wiki baada ya kikao kilichopita) basi uliza kila mtu ajitambulishe ili wote wakumbuke majina ya kila mmoja. Wakumbushe ni kwa nini sisi sote tuko pamoja na haraka, pitia makumbusho ya sheria za msingi mlizoainisha pamoja na tahadhari ya unyeti. Eleza kikundi kusudi la kikao cha warsha hii. Inafaa pia kupitia haraka hoja kuu ulizoangazia katika vikao vya awali. Tunapendekeza upitie kwa kifupi slaidi za uwasilishaji ambazo umetumia hapo awali - lakini ikiwa huna wakati, basi kurejelea haraka uwasilishaji wako wa kikao kilichopita kutasaidia kukumbusha kikundi kwa kasi kuhusu masuala ambayo umeangazia.

AU

Ikiwa unafanya kikao hiki kama sehemu ya warsha kamili ya mafunzo

Ikiwa unasimamia kikao hiki kama sehemu ya warsha kamili ya mafunzo (kumaanisha kimejumuishwa na vikao vingine), basi tunapendekeza sasa uwe wakati wa kuwa na shughuli ya kuisimua, na hutahitaji kufanya ukumbusho kamili au kikao cha kurudia mliyoyapitia awali. Unaweza tu kuwasilisha malengo makuu ya kikao, mada kuu ambazo utajadili, na ukumbusho mfupi kuhusu unyeti na umuhimu wa kila mtu kuheshimu maoni ya mwenzake.



Shughuli 2: Kupata sauti yako na mamlaka

Lengo la kikao hiki kama mkufunzi

Shughuli hii ni ya kutoa nafasi kwa washiriki kufikiria kuhusu jukumu lao wenyewe kama wenye uwezo wa kuleta mabadiliko katika jamii zao - haswa kwa wanaokuwa au watakaokuwa wanaharakati wachanga na watetezi wa kukomesha kuozwa kwa watoto . Shughuli hii inakusudia kuongeza ujasiri na imani yao kwamba kweli wanaweza kuchukua hatua kuhusu suala hili na kile wanachofanya kinaweza kuleta mabadiliko. Tayari wameunda maoni yao ya siku zijazo wanazotamani; Sasa ni wakati ambao wanaweza kuona ni jinsi gani kila mmoja wao anaweza kusaidia kufikia siku hizo za usoni.

Una dakika 15 kwa zoezi hili la kuigiza

1. Waombe washiriki wote katika kikundi chako waungane wawili wawili. Ikiwezekana, watie moyo waungane na mtu ambaye hawajafanya kazi naye kwa karibu hapo awali.
2. Waambie kuwa watafanya zoezi la kuigiza kwa pamoja ambapo kila mchezaji anajifanya kuwa mhusika katika mazungumzo. Mtu mmoja kati ya wawili hao atakuwa mtu mzima mwenye ushawishi katika jamii wanayoishi; Kwa mfano, wanaweza kuwa mwalimu mkuu au kiongozi wa jamii. Mhusika yule mwingine katika majadiliano atakuwa mtu mchanga kutoka kwa jamii.
3. Sasa ni wakati wako kuunda mazingira. Hali wanayopaswa kuigiza ni ifuatayo: mtu mzima haamini kwamba kuozwa kwa watoto ni suala, au kwamba vijana wanaweza kuchukua hatua kumaliza tabia hii. Pia wanafikiri kuwa vijana hawapaswi kuingilia kati masuala kama haya, kwani ni mazoea ya kijamii na ya kitamaduni. Walakini, kijana huyo anajali kwa shauku kuhusu kuozwa kwa watoto na anaamini kweli kwamba vijana wanapaswa kushiriki katika juhudi za kumaliza mazoea haya, na kwamba tabia hii inahitaji kubadilika katika jamii yao.
4. Omba vikundi vitumie dakika 5 kufanya zoezi la kuigiza - ambapo wanaigiza majukumu yao tofauti - na hivyo kila mmoja atoe hoja zake kwa / dhidi ya vijana kuchukua hatua kuhusu suala hili.
5. Mwishoni mwa maigizo, waulize wote wafikirie maswali yafuatayo:
 - Je, ni hoja gani mtu mzima alitumia kusema kwamba vijana hawapaswi kuhusika katika suala hili?
 - Je, kijana huyo alitumia hoja gani?
 - Je, unafikiri nani alishinda majadiliano katika kundi lako?
 - Je, ni nini kingesaidia kuimarisha hoja yako kama mwanaharakati mchanga?

Sasa tumia uwasilishaji wa mfano kwa ukurasa ufuatao kushiriki ujumbe muhimu. Uliza kikundi ikiwa inawezekana kwa vijana kuwa na KIASI CHA, ikiwa sio ujuzi huu WOTE?



AU



AU



Mfano 1 wa Uwasilishaji

Kuwa mwanaharakati madhubuti kunahitaji:

- Shauku na nguvu.
- Uvumilivu wa kuendelea na majadiliano na mapambano.
- Maono wazi ya mabadiliko unayotaka kuona / kufikia.
- Uwezo wa kufanya kazi na wengine.
- Utayari wa kutenga wakati na nguvu kwa ajili ya lengo lako.
- Kuelewa kuwa sio kila mtu ana maoni sawa na wewe, na jinsi ya kuwashawishi watu hao.
- Uhodari wa mawasiliano kuelezea ujumbe wako wazi na kwa urahisi, na kuwashawishi watu kuunga mkono upande wako.

Mfano 2 wa Uwasilishaji

Vijana huwa wanaharakati shupavu sana kuhusu masuala ya kuozwa kwa watoto kwa sababu:

- Wanaathiriwa moja kwa moja na wanahusika katika suala hilo.
- Wana ufikiaji wa habari ambao watu wazima hawawezi kuwa nao, na maoni tofauti kuhusu mila au kanuni za kijamii ambazo zinaweza kubadilika kwa kila kizazi, badala ya kubaki zilivyo.
- Wanaweza kusaidia kutambua wasichana walio katika tishio na mara nyingi wanaweza kusaidia kuingilia kati.
- Wanaelewa shinikizo ambazo vijana wanapitia kutoka kwa wazazi wao na jamii, haswa kuhusu mazoea ya kitamaduni.
- Wanaweza kuchambua ikiwa suluhisho linalopendekezwa la suala hilo litafaulu au la, na kutoa suluhisho au hatua ambazo wengine hawajafikiria.

Majadiliano ya kikundi

Sasa waulize kikundi cha jumla wanajisikiaje baada ya kufanya zoezi hili kwa kuashiria kwa kifupi hisia zao. Ikiwa wanaamini vijana wanaweza kuchukua hatua kumaliza kuozwa kwa watoto na wanaweza kuwa mawakala wa mabadiliko, wanapaswa kwenda upande mmoja wa chumba. Ikiwa hawaamini, wanapaswa kwenda ule mwingine. Ikiwa vijana wowote hawaamini wanaweza / wanapaswa kuchukua hatua kuhusu suala hili, waulize waeleze mawazo yao na wazungumzie haya kama kikundi kidogo. Kila mtu anapaswa kuhisi amewezeshwa kuwa mleta mabadiliko, na kwamba wao ni waleta mabadiliko. Wahimiza waendeleo kuhudhuria mafunzo, na sema kwamba wanaweza kubadilisha mawazo yao wakati mafunzo yanaendelea. Eleza kuwa zoezi linalofuata - kuandaa mkakati wa uanaharakati - utawasaidia kuona ni jinsi gani wanaweza kuwa watetezi imara wa mabadiliko. Kila mtu ndani ya chumba ana uwezo wa kuathiri na kubadilisha hali zao. Kwa hivyo tunaendelea sasa kuona jinsi kutengeneza mkakati kutasaidia kukuwezesha wewe, kama mtetezi mchanga wa mabadiliko.

Shughuli 3: Uwasilishaji wa mkufunzi - Kuandaa mkakati wa uanaharakati

Sasa ni wakati wako, mkufunzi, kuwasilisha kuhusu yale ambayo kikundi kinahitaji kufanya ili kuunda mkakati wa uanaharakati wa kukuza uanaharakati wa vijana. Una dakika 10 kuwasilisha maoni kuu ambayo tumejumuisha hapa chini.

Uwasilishaji kwa kikundi

Sasa kwa kuwa umetengeneza lengo lako kuu na madhumuni yako, uko tayari kuyachunguza kwa undani zaidi na kufikiria ni hatua gani za utendaji unaweza kuchukua pamoja na wengine ili kuzifanikisha - hatua moja kwa nyingine. Mkakati wa uanaharakati ni njia moja ya kusaidia kupanga mchakato huu. Inakuwezesha kupanga kila shughuli ya kibinafsi ambayo itachangia kufikia 'taswira kuu' au lengo unalojitajidi kufikia. Inakusaidia pia kufikiria ni nani katika timu yako atafanya shughuli gani, na walengwa wako au wadau wako watakuwa nani. Hii ni kupanga ramani za hatua unazohitaji kuchukua kufikia mabadiliko unayotaka kuona. Mkakati wako utaelezea mkusanyiko wa shughuli ambazo zinahitajika kufanywa kutimiza lengo lako la muda mrefu. Kurahisisha, unapaswa kupitia na kujibu maswali yafuatayo:

- Tuko wapi sasa?
- Tunataka kwenda wapi?
- Tutafikaje hapo?

Kila hatua itahitaji kujumuisha:

- Njia za kufanya kazi kwa ufanisi, kutokana na fursa na changamoto za mazingira / hali ambapo unafanya kazi.
- Kugawanya nyenzo ulizonazo.
- Jinsi ya kusimamia uhusiano kati ya wadau, na mashirika unayofanyia kazi.
- Jumbe maalum zinazolenga hadhira na vikundi maalum ambao watakusaidia katika lengo lako.

Kuwa na mchakato wakati wa kupanga mkakati wako wa uanaharakati ni njia muhimu ya kukabiliana nayo. Kuwa na mchakato na utaratibu, yaani kumaanisha kuwa fikira za hatua kwa hatua kuhusu ni nini kinahitaji kufanyika, husaidia kuhakikisha unashughulikia kila shughuli inayohitajika, na huwasaidia wengine kujua mipango yako na kuona ni jinsi gani wanaweza kuhusika.

Unahitaji kuweka lengo ya ni wapi unataka kwenda, na kisha ugawe safari hiyo kuwa sehemu tofauti. Hii haiwezi kufanywa bila mbinu iliyozingatiwa, na inayochukua hatua kikamilifu. Jumbe za kimkakati ni muhimu na zinahitajika katika kusaidia kufikia mabadiliko unayotaka kuona. Ni muhimu kuzifanya hati zilenge hadhira husika, kutoa mawasiliano bora na uanaharakati kuhusu suala lako. Inasaidia pia kuvunja malengo mapana na malengo makubwa ili ziwe hatua ndogo zinazoweza kudhibitiwa.

Ni juu yako kuamua ikiwa ni muhimu kujadili na kukagua mkakati wako kila mwezi, au baada ya kila miezi kadhaa, kulingana na ratiba unayotengeneza na lengo lako kuu. Mikakati ya uanaharakati huwa si moja kwa moja katika muundo na utekelezaji wake na itahitaji kubadilishwa na kusahihishwa unapoendelea, kwani muktadha na mazingira unapofanyia kazi yanaweza kubadilika pia. Utahitaji kukagua na kurekebisha tena shughuli na vitendo unapoanza utekelezaji halisi. Hii ni ili kuhakikisha kuwa unashughulikia masuala anuwai kwa kadiri uwezavyo, na unawajumuisha watu wote, au kukosa kushughulikia mazingira halisi katika kikundi au jamii unapofanyia kazi. Sasa tutapitia kiolezo kilichopendekezwa kinachojumuisha mifano ya kila kipande cha fumbo unachohitaji kukuza ili kuunda mkakati wako.

Tunapendekeza umpe kila mshiriki nakala ya mkakati wa uanaharakati wa mfano na fomu ya kiolezo ambayo tumejumuisha hapa chini.

Kutumia jedwali la mfano (ambalo limejumuishwa kwenye ukurasa unaofuata), lipitie na kikundi chako na ueleze ni nini unahitaji kuingiza kwenye kila safu kukuza mkakati wako. Unaweza kuelezea hatua zifuatazo:

- Anza kwa kukamilisha lengo lako katika safu ya juu - haya ni mabadiliko ya mwisho unayotaka kufikia kupitia kazi yako.
- Kisha, ongeza madhumuni yako kwenye safu ya kushoto kabisa. Jaribu kuwa na madhumuni matatu au tano unayotaka kufikia kupitia kazi yako.
- Kuanzia kushoto kwenda kulia kwenye kila safu, waza kuhusu shughuli zinazohitajika na ni nani anayeweza kuzifanya pamoja katika kikundi chako na kuzijumuisha katika kila sehemu.
- Ikiwa umeweza kukamilisha uchambuzi wa kijinsia tuliopitia hapo awali, urejeele hapa. Hii pamoja na utafiti na uchambuzi mwingine wowote uliufanya utakusaidia kujua unawalenga kina nani, wakati halisi utakaohitaji, na masuluhisho yepi zinaweza kutumiwa.
- Soma mifano iliyojumuishwa kwenye jedwali ikiwa utakwama au ikiwa unahitaji msukumo zaidi.



1. Mfano wa kiolezo kilichokamilishwa cha mkakati wa uanaharakati

Lengo: Haya ni maelezo mafupi ya jambo ambalo unatamani kufikia baada ya muda mrefu, au 'taswira kuu' unayotaka kufikia kupitia kazi yako au kushiriki kwako.

Mfano wa lengo: Kupunguza idadi ya watoto wanaooswa kwa 25% katika vijiji viwili kwa mwaka mmoja.

Madhumuni	Walengwa	Washirika	Shughuli	Nyenzo	Hatari zinazoweza kutokea	Muda	Wanaowajibika	Vigezo vya Mafanikio
Je, unataka kufikia nini? Je, ni mabadiliko gani ya mwisho unataka kuona?	Je, ni watu gani muhimu zaidi unahitaji kulenga au kushawishi kufikia mabadiliko unayotaka kuona?	Je, ni watu gani unahitaji kufanya kazi nao na watakusaidia katika kazi yako?	Je, ni hatua gani au vitendo utahitaji kuchukua kufikia kila lengo ili ufanikiwe?	Je, utahitaji nini kufikia lengo lako? Ikiwa utahitaji pesa au bajeti, kuwa wazi kuhusu kiasi utakachohitaji na hii itatoka wapi.	Je, kuna tishio, athari mbaya au changamoto gani ambazo zinaweza kutokea kwa sababu ya kazi yako kwenye suala hili? Pia fikiria kuhusu masuala ya kijinsia yanayohusika.	Kuwa wazi kuhusu ni hatua zipi zinahitaji kuchukuliwa, ni mpangilio upi unahitaji kufuatwa, na ni lini zinahitaji kutekelezwa.	Kuwa wazi ni nani anayeongoza kwa kazi gani maalum, na jukumu lao ni nini katika kuhakikisha hatua imekamilika.	Utajuaje ikiwa umefanikisha malengo yako, na unahitaji nini kufuatitia hadhi yako kufikia kile unachohitaji kufanya?
Shiriki majadiliano ya radio kuhusu athari za kuozwa kwa watoto	<ul style="list-style-type: none"> Maafisa elimu wa eneo Mkuu wa polisi na maafisa wengine Wanajamii 	<ul style="list-style-type: none"> Vyombo vya habari vya jamii Walimu wa eneo Polisi 	<ul style="list-style-type: none"> Tembelea kituo cha radio ili kuweka wazo lako Zungumza na binamu ambaye anajua DJ wa radio na ulize ushauri wake kuhusu jinsi ya kuweka hili wazo na jinsi ya kupanga majadiliano 	<ul style="list-style-type: none"> Fedha za usafiri Hakikisha vijana wa kike wanachangia kwenye kipindi / jopo. 	<ul style="list-style-type: none"> Jamii ya wenyeji wanapingana na maoni yako, kwa hivyo mwalike kiongozi mzee awe kwenye kipindi 	<ul style="list-style-type: none"> Katika miezi miwili: kukamilika mwishoni mwa Februari 	<ul style="list-style-type: none"> Peter: kuzungumza na DJ au mtangazaji wa radio Seline: kuandaa mwandiko na hoja kuu za kuzungumzia 	<ul style="list-style-type: none"> Kipindi cha mazungumzo ya radio kimekamilika

2. Kiolezo cha mkakati wako wa uanaharakati: cha kutumia katika vikundi wako

Lengo:

Madhumuni	Walengwa	Washirika	Shughuli	Nyenzo	Hatari zinazoweza kutokea	Muda	Wanaowajibika	Vigezo vya Mafanikio
Je, unataka kufikia nini? Je, ni mabadiliko gani ya mwisho unataka kuona?	Je, ni watu gani muhimu zaidi unahitaji kulenga au kushawishi kufikia mabadiliko unayotaka kuona?	Je, ni watu gani unahitaji kufanya kazi nao na watakusaidia katika kazi yako?	Je, ni hatua gani au vitendo utahitaji kuchukua kufikia kila lengo ili ufanikiwe?	Je, utahitaji nini kufikia lengo lako? Ikiwa utahitaji pesa au bajeti, kuwa wazi kuhusu kiasi utakachohitaji na hii itatoka wapi.	Je, kuna tishio, athari mbaya au changamoto gani ambazo zinaweza kutokea kwa sababu ya kazi yako kwenye suala hili? Pia fikiria kuhusu masuala ya kijinsia yanayohusika.	Kuwa wazi kuhusu ni hatua zipi zinahitaji kuchukuliwa, ni mpangilio upi unahitaji kufuatwa, na ni lini zinahitaji kutekelezwa.	Kuwa wazi ni nani anayeongoza kwa kazi gani maalum, na jukumu lao ni nini katika kuhakikisha hatua imekamitika.	Utajuaje ikiwa umefanikisha malengo yako, na unahitaji nini kufuatilia hadhi yako kufikia kile unachohitaji kufanya?

Hapa kuna maswali ya kukusaidia kuchagua shughuli zinazowezezana katika mkakati wako wa uanaharakati

1. Je, sifa za mlengwa au walengwa wako ni gani; Wanapenda na hawapendi nini, wanavutiwa na nini? Je, unajua nini kuhusu kazi yao na jinsi unavyoweza kuvuta umakini wao? Fikiria kuhusu ni shughuli au mbinu zilizowahi kufaulu kwao hapo awali ili kuwafanya watambue suala fulani au zilizowavutia, au jinsi bora ya kuwafikia moja kwa moja. Kwa mfano, ikiwa unalenga mwanasiasa mtulivu asiyependa kuhusika na vyombo vya habari, basi ripoti fupi inayoonyesha ushahidi dhahiri wa mambo yanayoweza kukomesha kuozwa kwa watoto inaweza kuwa na mafanikio zaidi kuliko maandamano makubwa nje ya ofisi yake au kumtumia ombi.
2. Je, una bajeti ya shughuli zako? Ikiwa siyoy, basi kuandaa hafla, na gharama zinazohusiana kama vile viburudisho, kukodisha ukumbi n.k., inaweza isiwezekane. Fikiria kuhusu mambo ambayo unaweza kufanya ambayo hayagharimu pesa maana huna bajeti: kwa mfano, kuhusisha vyombo vya habari mara nyingi hakuna gharama. Au ikiwa shughuli ni muhimu, basi fikiria kufanya kazi na mwenzako au kufanya hivi pamoja; Hii inaweza kusaidia kupunguza gharama au mwenzako anaweza kusaidia kwa kukupa bajeti ya ziada.
3. Je, kwa kweli ni muda upi unaweza kutoa kwa shughuli hii? Tenga wakati halisi ambao uko tayari kutumia na kile unakusudia kufikia.



AU



AU



Uwasilishaji wa mfano: Kuunda mkakati wa uanaharakati

- Mkakati wa uanaharakati hukusaidia kupanga kila hatua au shughuli ambayo itakusaidia kufikia 'taswira kuu' au lengo uliloweka kwa kazi yako.
- Kwa maneno rahisi, mkakati unakusaidia kuwa wazi kuhusu: tuko wapi sasa, ni wapi tunataka kwenda na ni nini tunahitaji kufika huko.
- Shughuli kwenye mkakati wa uanaharakati zinahitaji kukusaidia katika:
 - Kutathmini fursa na changamoto zinazoweza kutokea kwa kufanya kazi katika mazingira maalum, na ni hatua gani unahitaji kuchukua ili kushinda changamoto au tishio zozote.
 - Kuhakikisha umetenga rasilimali na bajeti zilizopo, na umetenga kazi na shughuli kama vile kuripoti na kutathmini.
- Kusimamia uhusiano na wadau wengine au watendaji, na kusimamia muungano wako. Pia itasaidia kukuonesha ni nani unahitaji kufanya kazi naye.
- Jinsi ya kuunda ujumbe wako kushawishi hadhira lengwa unayohitaji kushughulikia.
- Mpango wa kimkakati ni mchakato wa kimfumo unaowezesha wengine kujua mipango yetu ili kujihusisha na suala.
- Kuunda jumbe za kimkakati kutakusaidia kulenga hadhira husika na kutoa mawasiliano yenye ufanisi zaidi, na hivyo kufikia matokeo makubwa.
- Inasaidia pia kuvunja lengo lako kuu (au lengo pana) katika hatua zinazoweza kudhibitiwa zaidi. Hizi zitakusaidia kukaribia kufikia mabadiliko unayotaka kuona kama matokeo ya kazi yako.

Shughuli 4: Kazi ya vikundi - Kuunda mkakati wako wa uanaharakati

Gawanya washiriki wako katika vikundi vitatu kwa kuhesabu kila mtu kuanzia moja, mbili na tatu, kisha kurudia hadi kila mtu awe na nambari, na kisha kukusanya nambari zinazofanana pamoja. Eleza kuwa katika vikundi, sasa tutaandaa mkakati wa uanaharakati pamoja.

Huu ni mkakati au mpango ambao utatusaidia kuamua ni nini, lini na ni nani tutafanya shughuli zetu naye - yote kufikia lengo letu kuu ambalo tumechagua. Kila kikundi kinapaswa kupitia nguzo kwenye mkakati wa kiolezo na kukamilisha kadiri wawezavyo ili kuweka mkakati wao wa uanaharakati. Waambie kila kikundi wajaze madhumuni yao katika jedwali na wafikirie kuhusu shughuli wanazoweza kufanya ili kuchangia kufikia malengo, kisha wayaandike katika hati uliyowapa. Ikiwa vikundi vya sasa ni vile vile vya hapo awali, wacha warudi kwenye violezo vya malengo ambavyo walitumia kufanyia mazoezi kwenye vikao vilivyopita. Hivi vilivasaidia kutambua ni malengo gani wanahitaji, madhumuni yao yalikuwa nini na kadhalika, na hivyo litasaidia katika kuboresha kile wanachotaka kusema katika zoezi hili la mawasiliano.

Zoezi hili ni mfano tu wa kuwawezesha kufikiria kuhusu maeneo tofauti na masuala ambayo wanahitaji kufikiria wakati wanapopanga shughuli zao za uanaharakati, kwa hivyo ni vizuri kupitia mifano hii ili kila mtu atambue shughuli zote zinazohusika. Wakumbushe pia wafikirie kuhusu muda watakaohitaji, ni nani atawajibika kwa kila kazi, na ni rasilimali gani watahitaji kufikia lengo. Watakuwa na dakika 20 kupitia sehemu mbali mbali kwenye kiolezo pamoja na kuanza mipango yao. Uliza kila kikundi watoe wasilisho fupi la mkakati wao wa uanaharakati na mpango wao wa utekelezaji ili kufikia lengo lao kuu. Wape kila kikundi dakika 5 kuwasilisha shughuli walizoandika. Wakati utakaotumika kwa mawasilisho utategemea idadi ya vikundi ulivyonavyo, lakini ikiwa una vikundi vitatu, basi ruhusu dakika 15 kwa shughuli hii.

Toa dakika 5 za mwisho wa shughuli kwa maoni au maswali yoyote kutoka kwa kikundi cha jumla. Ni muhimu kila mmoja aelewe jinsi ya kutimiza na kinachohitajika ili kukamilisha mkakati huu.



Shughuli 5: Shughuli ya Kusisimua

Mara tu unapomaliza zoezi la kazi ya vikundi, unapaswa kutathmini kiwango cha nguvu ndani ya chumba. Tunapendekeza utumie shughuli hii kwani ni njia rahisi na nzuri ya kuonesha kikundi chako jinsi ujumbe unaweza kubadilika au kuwa tofauti kabisa wakati watu wanawasiliana. Inasaidia kuonesha jinsi ilivyo muhimu kuwa na mawasiliano na ujumbe wazi na rahisi, haswa wakati wa kujadili suala gumu kama vile kuozwa kwa watoto.

Nong'onozea, nong'onozea...

Waambie kikundi waunde mistari miwili, kila mtu akiangalia mbele ya chumba, na hakikisha kuna nafasi kati ya mistari. Kabla ya shughuli hii, andika kwenye vipande vya karatasi hadithi chache za kuchekesha, zisizo sahihi au zinazoeleza dhana tofauti kuhusu kuozwa kwa watoto kwenye muktadha wa kikundi chako. Toa taarifa moja kwa mtu wa kwanza katika kila mistari. Waambie wasome ujumbe huo kimya kisha wamng'onozee mtu aliye nyuma yao. Kila mtu aliye nyuma atafanya jambo lile lile: kunong'onozea ujumbe waliopata mtu aliyesimama nyuma yao. Endelea hivi mpaka ujumbe ufike mwisho wa mistari. Waulize washiriki wa mwisho waseme kwa sauti kubwa ujumbe ambao wamesikia. Hii kwa kawaida huchekesha sana kwa sababu ujumbe hupotoshwa unapopitishwa chini ya mistari.


Tumia hii kama fursa muhimu ya kutanguliza wazo kuhusu kikao kinachofuata - kuunda ujumbe wenye ufanisi - kujadili suala hili la ujumbe na kutoelewana. Waulize washiriki ni nini kilipotoka na kwa nini, na ni jinsi gani wanafikiria wangeweza kuzuia hili au kuliboresha. Ruhusu dakika 10 kwa kikao hiki chote cha kuisisimua.

Shughuli 6: Uwasilishaji wa mkufunzi - Kuunda ujumbe wenye ufanisi

Sasa ni wakati wa uwasilishaji mwingine mfupi kutoka kwako kama mkufunzi. Dakika 10 (usipitishie dakika 15) zimetengewa kikao hiki. Lengo la kikao ni kuwasilisha kwa kikundi kuhusu jinsi ya kukuza jumbe muhimu ili kuhakikisha mawasiliano yako yana ufanisi na yanaimarisha uanaharakati wako. Kwa hivyo ni muhimu kuelezea yafuatayo kwa kikundi cha jumla.

Baada ya kuandaa mkakati wako wa uanaharakati, ni muhimu kutambua jumbe muhimu. Hizi ni taarifa fupi zinazoelezea dhamira na lengo lako, mabadiliko unayotaka kuona au kufikia, na jinsi unavyotaka kufanikisha haya. Ujumbe unaelezea wazi kwa hadhira yako kuhusu suala; ni lipi, ni nini wanaombwa wafanye / wanahitaji kufanya ili kusaidia kulifanikisha, kwa nini suala linahitaji kusuluhishwa, na matokeo mazuri yatakayoonekana baada ya kuchukua hatua.

Taarifa au ujumbe wa jumla imara ni muhimu kushikilia mkakati wako wa uanaharakati pamoja. Ikiwa una jumbe nyingi sana, au hazieleweki au ni ngumu sana, huenda zisiwavyutie walengwa wako au huenda zikose kuwa na athari ya kudumu. Sio lazima taarifa ya jumla iwe sentensi moja tu, lakini jaribu kufanya iwe fupi na yenye uhakika ili kuvuta umakini wa hadhira yako.



Ujumbe wako unapaswa:

- Kuwashawishi na kuwahasisha watu, kuwafanya wapate msukumo kuhusu jinsi wanaweza kufanya mabadiliko.
- Kujenga ufahamu kuhusu suala hili, na kuwafanya watu wajali kwa nini suala hili ni muhimu.
- Kuhamasisha kuhusu suala lako. Kwa mfano, kuwajulisha watu kuhusu ukosefu wa haki, au athari mbaya za kuozwa kwa watoto, kutasaidia kuhamasisha msaada. Unahitaji kuwaambia ni kwa nini wanapaswa kujali.
- Kufanya vyombo vya habari na washawishi muhimu katika jamii yako wapendezwe na watake kushiriki.
- Kuwa na athari na kujitokeza kutoka kwa 'machafuko ya mawasiliano' mengine ambayo watu husukumwa kila siku. Kila mtu anakabiliwa mno na habari za aina zote kupitia vyombo vyote vya habari - jaribu kufanya ujumbe wako uwe rahisi lakini imara ili uwe bora kuliko zingine.

Ujumbe unapaswa kujumuisha:

- Taarifa ya msingi inayoelezea wazo lako kuu au mambo yanayosababisha tatizo. Inaelezea ni kwa nini mabadiliko ni muhimu kabisa, na lengo lako kuu ni lipi. Lengo lako kuu ni kile unachotaka kufikia kupitia uanaharakati wako, kwa hivyo wadau wote wanahitaji kuelewa na kufahamu hilo mara moja.
- Mifano kadhaa ya ushahidi ya kuunga mkono taarifa hiyo, na ukweli na takwimu zinazoeleweka.
- Lugha inayofaa muktadha huo ambayo itawavutia walengwa wako wakuu. Kwa mfano, hadithi halisi kutoka kwa waathiriwa na kutoa athari za suala unayovutia umakini kuhusu husaidia kuvutia na kuwafanya watu waelewe, kwani hii inaweka sura ya mwanadamu binafsi kwa uwasilisho wa suala lako.
- Ni hatua zipi zinahitaji kuchukuliwa, na ni nini hadhira yako inaweza kufanya kuchangia mabadiliko, ili suluhisho la suala lifikiwe.



AU



AU



Mfano wa Uwasilishaji: Kubuni ujumbe wako

Ujumbe unawaambia walengwa wako ni nini wanapaswa kufanya ili kusaidia kutimiza lengo lako: kile wanachoulizwa kufanya, kwa nini ni muhimu kufanya, na matokeo mazuri ya kushiriki.

Ujumbe unapaswa kuangazia:

- Kile unachotaka kufikia.
- Kwa nini unataka kulifikia (na kwa nini wengine wangependa kulifikia pia).
- Jinsi unavyopanga kulifanikisha.
- Ni hatua gani maalum unataka walengwa wako wachukue.

Ujumbe unapaswa:

- Kushawishi na kuwahasisha watu, kuwafanya wapate msukumo kuhusu jinsi wanaweza kufanya mabadiliko.
- Kujenga ufahamu kuhusu suala hili, na kuwafanya watu wajali kwa nini suala hili ni muhimu.
- Kuonesha hali ya ukosefu wa haki ili kuhamasisha msaada: waambie watu ni kwa nini wanapaswa kujali.
- Kufanya vyombo vya habari na washawishi muhimu katika jamii yako wapendezwe na watake kushiriki.
- Kuwa na athari na kujitokeza kutoka kwa 'machafuko ya mawasiliano' mengine ambayo watu husukumia kila siku.

Sehemu ya 2 ya uwasilishaji: Ni nini hutunga ujumbe mzuri?

Mawasiliano, au jinsi unavyowasilisha ujumbe wako, ni sehemu muhimu ya kazi yako ya uanaharakati. Ni muhimu kufikiria ni jumbe zipi zitafaa zaidi unapotoa hoja yako, haswa kwa walengwa wako tofauti. Kuwaza na kujadili pamoja husaidia kuhakikisha kila mtu kwenye timu yako au kwenye kikundi chako ana uelewa sawa. Kufanya kazi pamoja, haswa kwenye shughuli zenye changamoto zaidi kama kuunda jumbe zako, husaidia mno katika kujenga mawasiliano imara.

Jumbe zenye ufanisi:

- Zinapaswa kufupisha mabadiliko unayotaka kuleta.
- Zinapaswa kuwa fupi na rahisi.
- Zimeundwa kulenga hadhira.
- Zinapaswa kujumuisha tarehe ya mwisho ambapo unataka kufikia lengo / madhumuni yako.
- Zinajumuisha ni kwa nini mabadiliko ni muhimu.
- Zinaweza kukumbukwa kwa urahisi.
- Zinapaswa kuchanganya jumbe za kihemko na za mantiki.
- Ni muhimu kujadili na kufikiria ni jumbe zipi zitakuwa na ufanisi zaidi.

Hapa chini kuna vidokezo muhimu kutoka kwa kiolezo cha Plan International kuhusu jinsi ya kuunda ujumbe imara. Inahimiza wanaharakati kufikiria kuhusu jinsi ujumbe mzuri utakusaidia kuungana na vikundi unavyolenga au unahitaji kushiriki. Kuna maeneo matatu ambayo unapaswa kulenga kuwafanya watu wafikiri na kutenda kwa ajili ya suala lako.

- Vichwa vyao: huu ni ujumbe wa kiakili, wenye busara ambao utawafanya wafikiri, watambue au wajifunze kuhusu kitu ambacho hawakujua hapo awali, na kufahamu ni nini matokeo au athari ya mtindo huo mbaya.
- Mioyo yao: huu ni ujumbe wa kihemko na wa kibinafsi, na huwafanya watu kuhisi kwa undani ili kuwafanya watamani kuchukua hatua.
- Mwishowe mikono yao: huu ni ujumbe unaowaonyesha kwa lugha rahisi ni njia zipi wanaweza kutumia au ni hatua zipi wanaweza kuchukua kusaidia kuchangia mabadiliko na kusaidia kwa ajili ya suala lako.
- Usisahau hata hivyo - ujumbe unapaswa kuwa mfupi na wenye uhakika kila wakati.





AU



AU



Uwasilishaji wa mfano: Jumbe zenye ufanisi

Jumbe zenye ufanisi :

- Zinapaswa kufupisha mabadiliko unayotaka kuleta.
- Zinapaswa kuwa fupi na rahisi.
- Zimeundwa kulengwa kwa hadhira.
- Zinapaswa kujumuisha tarehe ya mwisho ambapo unataka kufikia lengo / madhumuni yako.
- Zinajumuisha ni kwa nini mabadiliko ni muhimu.
- Zinapaswa kukumbukwa.
- Zinapaswa kuchanganya jumbe za kihemko na zenye busara.
- Ni muhimu kujadili na kufikiria ni jumbe zipi zitakakuwa na ufanisi zaidi.
- Kufaa kwa aina tofauti za vyombo vya habari itakuwa muhimu kukusaidia kufikisha ujumbe wako kwa watu unaotaka kufikia.

Sehemu ya 3 ya uwasilishaji: Kufanya kazi na vyombo vya habari

Kufanya kazi na vyombo vya habari ni muhimu kwa uanaharakati wowote mzuri au mpango wa kampeni. Hii ni pamoja na kila aina ya chombo - mifumo ya jadi zaidi na majukwaa mapya kama vile mitandao ya kijamii. Kufanya kazi na aina tofauti ya vyombo vya habari itakuwa muhimu kukusaidia kufikisha ujumbe wako kwa hadhira unayotaka kuungana nayo, na itasaidia kueneza ujumbe wako kwa hadhira pana. Fikiria yafuatayo:

- Kuunda orodha ya mawasiliano ya mitandao, ikiwa ni pamoja na vituo vya redio vinavyolenga vijana na vituo vya runinga na watu maarufu - wanaweza kuwa washirika wa nguvu.
- Kuandika nakala kuhusu suala lako na kuziwasilisha kwa magazeti yako ya kijamii au ya kitaifa.
- Kuzungumza kwenye vipindi vya redio ya kijamii ni njia nyingine muhimu ya kufikisha ujumbe wako na kusikika.
- Kuunda majukwaa yako mwenyewe ili kukuza sauti yako: hii inaweza kujumuisha shughuli kama maonyesho ya ukumbi, kufanya sanaa ya barabarani, kuunda majarida ya kibinafsi au blogi mtandaoni. Una chaguzi nyingi.
- Fanya utafiti kuhusu jinsi mashirika mengine yameweza kuunda ujumbe na kampeni zilizofanikiwa.

Shughuli 7: Majadiliano ya vikundi - Mawasiliano madhubuti

Tunashauri chaguzi hizi mbili katika kukamilisha shughuli hii na kikundi chako:

A) Shughuli ya kulisimua

Ikiwa hukufanya shughuli ya kulisimua kutoka kwa Shughuli 1 ya kikao hiki (nong'onozea nong'onozea...), basi tunapendekeza uitangulize hapa. Kuwezesha vikundi kuwa na tajiriba na kuelewa jinsi ujumbe unavyoweza kubadilika au kupotoka kwa ajili ya ukosefu wa mawasiliano kutawasaidia kuelewa umuhimu wa kutoa taarifa za uanaharakati zilizo wazi, zinazoeleweka na zenye ufanisi ili kuwasiliana kuhusu lengo kuu na jinsi ya kulifanikisha. Ikiwa unafanya shughuli hii, huhitaji kufanya majadiliano ya jumla, kwa hivyo ruka sehemu inayofuata hadi kwa hitimisho.

Au

B) Majadiliano ya jumla

Ikiwa ulifanya shughuli ya kulisimua hapo awali, au ikiwa shughuli lenyewe halifai kwa muktadha wa kikundi chako, hapa kuna shughuli mbadala ya kumalizia kikao. Ambia vikundi vikae kwenye miduara mitatu - wanaweza kuwa katika vikundi vile vile walivyotumia kwa Shughuli 4. Waeleze kila kikundi waje na hadhira za mfano na jumbe za vitendo au kitengo maalum cha jumbe: fikiria, hisi au fanya.

Kwa mfano, ikiwa mlengwa wako ni afisa wa elimu wa eneo lako, hatua moja ni kujadili jinsi ya kuimarisha jumbe dhidi ya kuozwa kwa watoto katika viwango fulani vya shule, au ni mikakati gani waalimu wanaweza kuweka ili kuhakikisha wasichana wanabaki shuleni na hawaozwi.

Kila kikundi kina dakika 10 kuunda jumbe za mfano za kuunga mkono eneo lao la kichwa (kufikiria), moyo (kuhisi) au mikono (kufanya). Kila kikundi kinaweza kuwasilisha tena jumbe zao kwa kikundi cha jumla: wana dakika 10 ya majadiliano.

Shughuli 8: Hitimisho

Baada ya majadiliano ya dakika 10 katika sehemu iliyopita, unganisha warsha, shukuru kila mtu kwa mchango wake na kisha funga kikao.



Picha © Princeakachi / Unsplash



Moduli 4: Pamoja, tuna nguvu zaidi!

Muhtasari wa Moduli

- Kuelewa faida na changamoto za kufanya kazi kwenye mada ngumu.
- Kueleza jinsi ya kutumia hatua za kijamii kushawishi michakato mikubwa zaidi kama vile ajenda pana za kitaifa.
- Kukuza uzoefu wa kufanya uchambuzi wa tishio na kueleza ni kwa nini hili ni muhimu.

Moduli 4 - Kikao 1

Upande hatari wa uanaharakati



Lengo

Kuelewa wazo la hatari na jinsi unaweza kufanya kazi kupunguza hatari zozote wakati wa kazi yako ya uanaharakati.



Idadi ya washiriki:
Chini ya 24



Muhtasari wa kikao

- Kumfahamisha mwanaharakati mchanga kuhusu wazo la hatari.
- Jinsi ya kutathmini na kuzuia hatari



Wakati unaohitajika:
Saa 1 Dakika 40



Vitu vya kuandaa mapema

- Soma maelezo ya usuli na uyajue vizuri ili uwe na ujasiri wa kuyawasilisha kwa kikundi cha jumla
- Slaidi za uwasilishaji (iwe za kielektroniki au kwenye chati)
- Jizoeze shughuli ya kulisimua ikiwa utafanya na kikundi
- Nakala za jedwali yoyote au violezo unazotaka kikundi kitumie: mfano wa tathmini ya hatari ambayo haijajazwa, na uchambuzi wa kisa kuhusu kazi ya vijana



Vifaa vinavyohitajika

- Karatasi za chati, kalamu za alama au kalamu nene, utepe au kitu cha kubandikia karatasi ukutani
- Mawasilisho
- Hati za mazoezi

Shughuli	Wakati uliotengwa	Muhtasari
1	Dakika 5	Utangulizi
2	Dakika 5	Shughuli ya Kulisimua
3	Dakika 20	Uwasilishaji wa mkufunzi: Tunamaanisha nini tunapozungumzia hatari, kudhibiti hatari na ulinzi wa wanaharakati vijana
4	Dakika 20	Kazi ya vikundi: Kutathmini hatari
5	Dakika 10	Uwasilishaji wa mkufunzi: Tathmini ya hatari na jinsi tunavyoifanya
6	Dakika 10	Kazi ya vikundi: Hatari
7	Dakika 10	Uwasilishaji wa mkufunzi: Nguvu ya ushirikiano - kufanya kazi pamoja kufikia mabadiliko
8	Dakika 10	Kazi ya vikundi: Faida na changamoto za kufanya kazi pamoja
9	Dakika 10	Hitimisho

4.1 Mwongozo wako wa mkufunzi

Shughuli 1: Utangulizi

Tanguliza moduli ukitumia utangulizi sawa na ilivyoainishwa katika vikao vya awali: utangulizi wa jumla, ukumbusho wa ulinzi, na ukumbusho wa sheria za utendakazi. Kama tulivyoeleza katika mipango mingine ya kikao, kuna njia tofauti za kuanzisha kikao ikiwa unakisimamia moja kwa moja baada ya vikao vingine, au ikiwa ni kikao cha kusimamia kipekee. Tafadhali soma tena tangulizi hizo na ufuata mwongozo huo huo.

Sasa unaweza kufahamisha kikundi kuhusu mada ya kikao hiki - una dakika 5 kwa shughuli hii.

Kikao hiki kinalenga kufafanua changamoto na fursa zinazoweza kupatikana na vijana wanaojihusisha na nafasi zinazongozwa na watu wazima, na matatizo ambayo wanaweza kukabiliwa nayo kama wanaharakati wachanga wanaoshughulikia masuala magumu kama kuozwa kwa watoto.

Vijana wana maoni na fikira muhimu na ya kipekee kuhusu masuala ambayo yanaathiri maisha yao. Wako katika nafasi bora zaidi kujua kinachowafaa zaidi na ni wabunifu kuhusu jinsi ya kutatua masuala. Kwa hivyo, maamuzi yanayowaathiri moja kwa moja au kwa njia nyingine yoyote lazima yafanywe kwa kushauriana nao. Vilevile, vijana wanaposikilizwa na kuchukua jukumu la kuongoza katika jamii, wanakuza uwezo na ustadi ambao unaboresha kujithamini kwao, ustawi na matarajio yao. Una jukumu muhimu la kuhakikisha watu wanakusikiliza na wanakadiria maoni yako kwa umakini, kwa sababu wewe ni hodari kama mwanaharakati mchanga mwenye nguvu anayepigania siku bora za usoni!

Lakini kuwa mwanaharakati kijana huambatana na vizuizi au changamoto, na si kazi rahisi kila wakati. Watu wazima mara nyingi huwa na mamlaka juu ya vijana na hivyo huishia kuwafanyia maamuzi. Watu wengi wanapuuza kufanya kazi na wewe, kwani 'wanajua mengi' kukuliko kwa sababu wewe ni mchanga sana kuelewa mambo. Matokeo yake ni kwamba kawaida vijana hawakadiriwi kama washiriki sawa. Huu ni ukweli wa kusikitisha, na tunahitaji kufanya kazi ili ubadilike. Kuna hatua ambazo zinaweza kukusaidia kuunda nafasi ya kusikilizwa, na kukusaidia kupaza sauti kubwa kuhusu suala hili.

Utahitaji kufanya juhudi za ziada kutengeneza nafasi ya sauti yako kusikika. Kwa kujua kuhusu tishio au changamoto zilizopo huko nje, na jinsi unavyoweza kuzizuia au kuzipunguza, unaweza kujilinda, kuhisi umehamasishwa na kufanikiwa kama mwanaharakati mchanga. Kwa kuhakikisha kuwa una jumbe rahisi na madhubuti, na mpango wazi wa uanaharakati wako, utajua ni hatua zipi unahitaji kuchukua, utawalenga kina nani, na ni shughuli gani unahitaji kufanya ili kufikia mabadiliko unayotaka kuona ulimwenguni. Kwa kufanya kazi pamoja kama muungano au ushirikiano, unaweza kusaidia kutoa kauli yenye nguvu na umoja. Hii ndio sababu tunatumaini mafunzo haya yatakusaidia kukuonesha zana muhimu na vidokezo vya kuwa mwanaharakati mchanga bora zaidi!



Shughuli 2: Shughuli ya kusisimua - Tupa mpira!

Waambie washiriki wasimame kwenye duara. Kutumia mpira, tutautupa kwenye duara kwa kila mmoja. Kabla ya kutupa mpira, lazima useme kwa sauti kubwa jambo moja ambalo umejifunza kwenye mafunzo; Kitu ambacho ni kipya kwako au ambacho kitakuwa muhimu kwa kazi yako. Kisha utatupa mpira kwa mtu mwingine, ukiita jina lake unapotupa. Wewe kama mkufunzi utaanza, kwa kusema kitu ambacho umejifunza, na utupe kwa mtu aliye mbali na wewe. Endelea mpaka watu wengi watupe mpira, au hadi dakika 5 zikamilike.

Shughuli 3: Uwasilishaji wa mkufunzi - Tunamaanisha nini kwa hatari, kudhibiti tishio na ulinzi wa wanaharakati vijana

Anza kwa kuwaza haraka pamoja na kikundi. Waulize waseme kinachokuja akilini mwao wanaposikia neno 'hatari'. Muulize mwandishi hoja aandike kile kinachosemwa kwenye karatasi ya chati. Tumia hadi dakika 5 kwa shughuli hii. Sasa ni wakati wako kuwasilisha kuhusu hatari na kile tunachomaanisha tunapozungumza kuhusu hatari zinazoweza kutokea na changamoto za kuwa mwanaharakati mchanga, na jinsi tunaweza kuzuia hatari katika kazi yetu. Una dakika 10 kwa sehemu hii yote, ukijumlisha sehemu ya kuwaza na kikundi pamoja na uwasilishaji.

Hatari

Hatari ni kitu kinachomweka mtu katika hali ambapo anaweza kupata madhara, hasara au matatizo. Hatari si sawa kwa kila mtu. Watu wote wanakabiliwa na hatari tofauti na wanaweza kuzipata katika viwango tofauti, unapojumuisha masuala tata kama jinsia, umri, ulemavu, n.k. Ni muhimu kutathmini tishio, na hatari zinazoweza kutokea kwa mpango wowote - hii inaweza kuwa shughuli kama mkutano, hadi mradi mzima unaoshughulikia kuozwa kwa watoto.

Unapoanza kupanga shughuli zako, ni muhimu ufanye uchanganuzi wa hatari kwanza ili uelewe kabisa muktadha unapofanyia kazi, na changamoto unazoweza kukumbana nazo. Hatari ni hali ambayo inaweza kuweka kitu au mtu katika matatizo, madhara au hasara. Kama mwanaharakati dhidi ya kuozwa kwa watoto, utapinga baadhi ya imani za kitamaduni, kanuni na maadili. Kwa hivyo ni muhimu uchukue wakati kuunda ramani ya hatari zinazoweza kutokea, na uamue njia za kupunguza pamoja na athari mbaya ambazo zinaweza kukupata wewe, wenzako au kazi yako.

Hatari zinazoweza kutokea ...

Kwa wanaharakati vijana:

- Kuna watu wengi ambao wana maoni ya kupinga mabadiliko ambao watajaribu kukuzuia katika kazi yako kwani hawataki kusababisha matatizo, kutoa changamoto kwa watu, au hawaamini tu unachowaambia.
- Kukasirika na chuki kutoka kwa viongozi wa jamii, dini au jadi.
- Wanafamilia kukosa kuelewa maoni yako na hivyo kuwa na chuki kwako kwa sababu unajaribu kuwafanya waache tabia hii ambayo kawaida ni sehemu ya mila zao.
- Wakati unaotumika kupinga kuozwa kwa watoto unaweza kupunguza shughuli zingine muhimu kama vile elimu yako, au kutafuta kazi, na inaweza kuwa na athari mbaya kwa maisha yako pamoja na uwezo wako wa kufanya majukumu muhimu.

Kwa wasichana wadogo, ambao hawajaozwa:

- Kuongezeka kwa hatari ya kulazimishwa kuolewa na wazazi wao.
- Kuchanganyikiwa wanapotambua ukosefu wa usawa na hivyo, kutaka kuona mabadiliko ya haraka katika jamii yao, lakini mwishowe hawana mamlaka ya kuyabadilisha.
- Wasichana kukosa uwezo wa kupinga ndoa za kulazimishwa, na kukosa njia mbadala au huduma za kupata msaada.

Kwa vijana wa kike walioolewa:

- Uwezekano wa dhuluma kutoka kwa waume (hii inaweza kuwa ya maneno, ya kimwili au ya kingono), haswa wanapokuwa na ujuzi zaidi kuhusu haki zao na kuongea waziwazi dhidi ya tabia hiyo.
- Kushutumiwa na jamii au kulipiza kisasi kwa wasichana na vijana wa kike ambao watauliza waziwazi ni kwa nini wameolewa.
- Wengi watapambana kusawazisha mahitaji na matarajio ya familia na uwezo wao wa kusaidia shughuli za uanaharakati.
- Kukumbushwa majeraha ya dhuluma ikiwa watachagua kushiriki waliyopitia pamoja na kikundi. Hii ni hatari haswa ikiwa hawawezi kupata huduma yoyote ya msaada kutokana na hayo.
- Kuhisi matarajio yao hayajatumizwa ikiwa hawajafarijiwa kabisa baada ya kuomba msaada.
- Hatari inaweza kutoka kwa mtu yeyote anayepinga msimamo wao au ambaye anahisi kutishiwa na jukumu lao kama wanaharakati, wanaoitisha mabadiliko.



AU



AU



Uwasilishaji wa mfano: Kukabiliana na tishio

Hatari ni hali ambayo inaweka kitu au mtu kwa hatari, madhara au hasara. Inaweza kuepukwa kwa kufanya uchanganuzi wa tishio na kuchukua hatua sahihi. Kama mwanaharakati wa kuozwa kwa watoto, utapinga mara nyingi mifumo ya imani za kitamaduni na maadili ya jamii, ambayo yatakuwa tishio kwako.

Hatari ina sehemu mbili: uwezekano wa jambo kuharibika, na athari mbaya ikiwa litafanyika.

Madhara yanayoweza kutokea kwenu kama vijana wanaharakati:

- Kushutumiwa na chuki kutoka kwa jamii na / au viongozi wa dini, na wanafamilia.
- Hii inaweza kusababisha kutengwa na jamii, na kupungua kwa uhuru wa kujieleza unapokabiliwa na athari za maoni yako.
- Ukosefu wa rasilimali au msaada wa kuweza kufanya kazi yako.
- Wakati unaotumika kupinga kuozwa kwa watoto unaweza kupunguza shughuli zingine muhimu, kama vile shule au majukumu ya familia.

Hatari zinazoweza kutokea kwa wasichana wadogo, ambao hawajaolewa:

- Kuongezeka kwa tishio la kulazimishwa kuolewa na wazazi wao.
- Kuchanganyikiwa wanapotambua ukosefu wa usawa na hivyo kukosa uwezo wa kubadilisha jambo hili.

- Wasichana kukosa uwezo wa kupinga ndoa za kulazimishwa, na kukosa njia mbadala au huduma za kupata msaada.

Hatari zinazoweza kutokea kwa vijana wa kike ambao wameolewa / waliowahi kuolewa:

- Dhuluma inayowezekana kutoka kwa waume au familia zao.
- Jamii kulipiza kisasi kwa maana kijana huyo amepaza sauti, unyanyapaa kutoka kwa wenzao na familia zao, kutengwa na wengine.
- Kukumbushwa majeraha ya awali tena au dhuluma ikiwa wanashiriki kuhusu waliyoyapitia.
- Kuhisi matarajio yao hayajitimizwa ikiwa hawajafarijiwa kabisa baada ya kuomba msaada.

Lakini usiwe na hofu! Kuna njia nyingi tofauti ambazo unaweza kujikinga kama mwanaharakati mchanga wa mabadiliko. UN (Umoja wa Mataifa) ina mikataba mingi ya kulinda wanaharakati wanaopigania maisha bora ya baadaye, ikiwa ni pamoja na haki za uhuru wa kujumuika na kujieleza. Angalia katiba na sheria za nchi yako ili uhakikishe unajua ni sheria na sera gani zinaweza kukulinda kisheria pia. Kufanya kazi pamoja kama kikundi husaidia kuifanya sauti yako kuwa na nguvu na zaidi, kwa kuonesha umoja kwa idadi, ambayo ni njia muhimu sana ya kulindana.

Shughuli 4: Kazi ya vikundi - Kutathmini hatari

Waombe washiriki waingie katika vikundi vinne kwa kipindi cha kazi ya vikundi; Unaweza kutumia njia moja tuliyoupendekeza katika vikao vingine kugawanya vikundi, au washiriki wanaweza kufanya kazi na wale ambao wanataka. Waulize wachague mtangazaji wa kuwasilisha baadaye kwa kikundi cha jumla. Kama kikundi, waombe wjadili ni hatari gani wanafikiria mwanaharakati dhidi ya kuozwa kwa watoto anaweza kukabiliwa nazo katika kazi yao. Wana dakika 10 kuwaza pamoja kwa haraka kuhusu swali hili. Waambie kila kikundi kiwasilishe. Wezesha majadiliano ya kikundi cha jumla kuhusu hoja walizozungumzia - kwa kuulizia habari zaidi, kama vile jinsi wanaweza kushinda hatari wanazotaja au ni nini vijana wanaweza kufanya ili kuzuia hatari hiyo. Ruhusu dakika 10 kwa majadiliano haya.

Shughuli 5: Uwasilishaji wa mkufunzi - Tathmini ya hatari na jinsi tunavyoifanya

Sasa ni wakati tena wa kuwasilisha kwa kikundi cha jumla kuhusu jinsi ya kufanya tathmini ya hatari ili kusaidia kujilinda dhidi ya matatizo na changamoto katika siku zijazo. Una dakika 5 kuwasilisha sehemu hii.

Tathmini ya hatari

Tathmini ya hatari ni chombo kinachokusaidia kufikiria tishio na changamoto zinazoweza kutokea na athari zake - zote kwa utaratibu na kwa njia iliyofikiriwa vyema. Pia itakusaidia kufikiria ni jinsi gani unaweza kupunguza tishio hizi na ni nini unaweza kufanya ili kuzizuia au kuzikomesha. Tazama jedwali hapa chini kwa maelezo, pamoja na mfano wa jinsi ya kuikamilisha.

Pamoja na vikundi pitia mfano (1) katika jedwali linaloonyesha hatari inayoweza kutokea na jinsi ya kuitathmini.

1. Mfano wa rejesta ya hatari

Hatari / tishio linaloweza kutokea?	Ni nini kinachoweza kutokea?	Unawezaje kupunguza hatari?	Ni nani anayewajibika kulikwepa?	Je, hatua zinahitajika kuchukuliwa lini?
Mfano: Kupingwa na jamii.	Kiongozi wa kidini anakushutumu, au anakupinga kwa ukali sana.	Andaa pahala salama, wazi pa mazungumzo ili kujadili hoja wazi na bila hasira au kulipiza kisasi. Kwa mfano, hii inaweza kuwa kama sehemu ya kipindi cha redio. Ongea na watu ambao wanaweza kuleta vurugu kabla ya kipindi cha redio.	Mfano: Kupingwa na jamii.	Kiongozi wa kidini anakushutumu, au anakupinga kwa ukali sana.

2. Sasa ni zamu yako

Hatari / tishio linaloweza kutokea?	Ni nini kinachoweza kutokea?	Unawezaje kupunguza hatari?	Ni nani anayewajibika kulikwepa?	Je, hatua zinahitajika kuchukuliwa lini?

Kutumia zana hii unapaswa:

- Kuanza kufanya tathmini ya tishio au rejesta mapema, kabla ya kupanga shughuli.
- Ili kuwa na mazingira bora, jadili kuhusu tishio kama kikundi ili kuhakikisha kuwa umezingatia hali zozote kila kikundi kinaweza kukumbana nazo.
- Kuanza na safu wima ya kushoto, kwa kuuliza ni hatari gani zinaweza kutokea kwa kila shughuli katika mpango wako wa mkakati.
- Jadili na ukamilishe safu zingine nne.
- Zipe kipaumbele hatari kwa kutathmini ni zipi zina uwezekano wa hali ya juu kutokea na ni zipi zinaweza kuwa na athari kali zaidi.

HUPASWI kuendelea ikiwa:

- Uwezekano wa hatari na wa athari kali ni mkubwa (kwa mfano, ikiwa kuna uwezekano mkubwa wa vurugu ya kimwili au matusi au kujeruhiwa).
- Hakuna huduma za msaada na / au mashirika ambayo unaweza kutafuta ushauri na msaada kutoka kwao.



KUMBUKA

Maswali ya kuzingatia kwa wanaoelimisha rika zao au wale wanaohusika na ufikiaji katika jamii

1. Je, mitazamo ya mitaa kuhusu kuozwa kwa watoto ni zipi?
2. Je, ni majukumu, kanuni na maoni gani yaliyopo kwa wasichana, wavulana, vijana wa kike na wa kiume?
3. Je, uingiliaji wako unaweza kuathiri watu tofauti vipi katika jamii?
4. Ni nani (watu binafsi au vikundi) anayeweza kupinga kazi yako?
5. Mkakati wako ni upi wa kushughulikia hili?



AU



AU



Mfano wa Uwasilishaji: Tathmini ya Hatari

- Rejesta ya tathmini ya hatari ni zana ya kukadiria hatari zinazoweza kutokea na athari zake.
- Tumia mfano wa kielelezo cha tathmini ya hatari cha washiriki ambacho tumejumuisha katika Mwongozo wako ili kukusaidia kupitia tishio ambazo unaweza kukumbana nazo. Anza na safu ya kushoto kabisa, kwa kuuliza ni hatari gani inaweza kuwepo kwa kila shughuli katika mpango wako wa mkakati. Rejelea mpango wako wa mkakati wenyewe.
- Jadili na ukamilishe safu zingine nne kwa zamu.
- Zipe hatari kipaumbele kwa kutathmini ni zipi zina uwezekano wa hali ya juu kutokea na ni zipi zinaweza kuwa na athari kali zaidi, kwani hizi ndizo zinapaswa kuwa kipaumbele chako.
- Usiendeleo ikiwa uwezekano wa hatari na wa athari kali ni mkubwa pia (kwa mfano, ikiwa kuna uwezekano mkubwa wa vurugu ya kimwili au matusi au kujeruhiwa). Pia ikiwa hakuna huduma za msaada na / au mashirika ambayo unaweza kufanya kazi nayo.

Shughuli 6: Kazi ya vikundi - Hatari

Ili kuelewa tathmini ya hatari, tutafanya kazi kupitia mfano wa kazi ya vijana, na ni hatari gani zinazoweza kutokea kupitia mfano huo. Toa mfano ufuatao kwa vikundi:

Mfano wa hali inayohitaji tathmini ya hatari

Kikundi cha vijana sita (wasichana wawili na wavulana wanne) kutoka Sierra Leone wameanzisha mradi ambao unakusudia kukuza uelewa kuhusu athari za kuozwa kwa watoto nchini mwao. Vijana hawa sita ndio timu kuu iliyounda mradi huo na walikuwa na jukumu la usimamizi, wakisaidiwa na mfanyakazi mwingine wa vijana. Kikundi kinaenda katika jamii ambayo hawajawahi kwenda hapo awali ili kufanya uhamasishaji wa msingi kwa wasichana na wavulana kuhusu kuzuia kuozwa kwa watoto. Eneo wanalotembelea ni la mashambani na jamii haijawasiliana sana na mashirika ya nje. Sehemu hiyo pia inakabiliwa na hali kali ya hewa wakati wa mwezi ambao wanalizuru. Mfadhili anatembelea jamii pamoja na kikundi kuangalia kazi zao na ataandaa ripoti.

Sasa ni wakati wa vikundi vyako kujaribu kufanya tathmini ya hatari. Waeleze watumie Jedwali 2 kujadili hatari zinazoweza kutokea kwa kikundi na jinsi wanaweza kuzidhibiti au kuzizuia. Waambie vikundi wajaadili na kujaza jedwali kwa dakika 10. Kuwa na majadiliano mafupi ya wazi ili kila kikundi kiweze kuwasilisha kuhusu hatari moja walilogundua na kile walipanga kufanya ili kupunguza hatari hiyo. Wape dakika 10 za majadiliano.

Sasa wajumuishe wote katika mazungumzo kwa kikundi cha jumla kuhusu hatari za kibinafsi ambazo washiriki, wanaoshughulikia masuala nyeti kama vile kuozwa kwa watoto, wamepata au wanakabiliwa nazo kwenye kazi zao. Waambie waeleze kikundi kuhusu tishio na jinsi wameweza kupunguza au kudhibiti hatari hiyo. Hakuna uwasilishaji wa kikao hiki - hiki ni kikao cha kushiriki kibinafsi cha kujifunza kutoka kwa kila mmoja na kusikia zaidi kuhusu tajiriba za washiriki. Lakini kuna maswali ambayo unapaswa kuuliza mwishoni mwa kikao.

Maswali ya kuweka kwenye slaidi ya uwasilishaji au karatasi ya chati

- Je, kila mmoja wenu anatarajia kukabili nini anapokuwa mwanaharakati wa kumaliza kuozwa kwa watoto katika jamii yake?
- Je, unaonelea hatari za kibinafsi ni zipi?
- Unafikiri unaweza kuzipunguza au kuzizuia vipi?
- Je, mnawezaje kusaidiana?

Ikiwa unakosa muda wa kupitia haya na kila mmoja wa washiriki wako, waombe waandike majibu ya kutafakari wenyewe. Lakini hakikisha wazungumze kuhusu swali la mwisho la jinsi wanaweza kusaidiana.

Shughuli 7: Uwasilishaji wa mkufunzi: Nguvu ya ushirikiano - kufanya kazi pamoja ili kufikia mabadiliko

Njia moja muhimu ya kupunguza hatari au changamoto kwa kazi yako, na kwako wewe kama mwanaharakati mchanga, ni kupata watu wanaoshughulikia suala kama lako wewe na kuunganisha jitihada ili kuwa na sauti yenye nguvu pamoja. Muungano au ushirikiano ni kikundi cha watu kutoka mashirika tofauti, au ndani ya kikundi cha jamii, ambao huungana kufanya kazi pamoja ili kufikia lengo moja. Huwa zinaundwa kwa muda mdogo au usio na kipimo, na zinaweza kutofautiana kwa ukubwa. Zipo ili kuleta umakini mpana na uchukuaji wa hatua kwa lengo kuu ambalo linaathiri watu wengi. Kwa jumla zina matokeo zaidi kuliko mashirika ya kibinafsi kwa sababu zinaweza kufikia watu wengi, kupata rasilimali zaidi na kuleta mitazamo tofauti. Mara nyingi huongozwa na mratibu na / au timu kuu ya watendaji. Tunaamini mna sauti na nguvu zaidi mnapofanya kazi pamoja.

Kufanya kazi na miungano au katika vikundi

Kuunda muungano au ushirikiano / vikundi vya uanaharakati ni mchakato wa kujenga uhusiano na mashirika au watu ambao wana lengo sawa na wewe, na watashirikiana na wewe kufikia maono haya ya pamoja. Kazi ya uanaharakati inaweza kufanywa kuwa imara zaidi kupitia miungano ambayo huunda majukwaa ili mashirika yawe na umiliki wa malengo ya pamoja. Uandalizi katika ushirikiano ni hatua muhimu ya kimkakati kusaidia kupaza sauti za wanaharakati zaidi, na unasaidia kuongeza shinikizo kwa walengwa wako, kama wale wanaofanya maamuzi.

Faida za kufanya kazi pamoja ni kama vile:

- Kushiriki habari, ujuzi, tajiriba, vifaa, fursa za ushirikiano na kadhalika.
- Sauti ya pamoja ambayo inaweza kuongea kwa nguvu ya umoja na kueneza jumbe kwa upana zaidi.
- Mitandao na miunganisho iliyokuzwa: mnaweza kufanikiwa zaidi pamoja kuliko ukiwa peke yako.
- Ufikiaji mkubwa kwa watoa maamuzi au walengwa wako muhimu.
- Kuongeza upatikanaji wa rasilimali ya watu na fedha.
- Kinga kwa wanachama ambao hawawezi kuchukua hatua peke yao, haswa wanapofanya kazi katika mazingira mabaya au magumu.
- Kupunguza marudio ya juhudi na ufanisi ulioboreshwa.
- Uaminifu ulioboreshwa, ushawishi na athari.

- Utofauti unaweza kuimarisha kampeni kwa kupanua mtazamo na kuleta uvumbuzi. Unaweza pia kusaidia ufikiaji kwa kuvutia idadi pana ya watu wenye vipaumbele na maslahi tofauti.
- Maendeleo ya kibinafsi na ya kitaalam ya watu na mashirika: msaada wa rika, kutia moyo, motisha na utambulikaji wa kitaalam.

Kufanya kazi katika muungano pia kuna changamoto kadhaa:

- Athari ya sifa mbaya kwa mashirika ya kibinafsi ikiwa kazi ya pamoja haijafanikiwa.
- Kupoteza uhuru.
- Migogoro ya maslahi.
- Kupungua kwa nyenzo.
- Inachukua muda mwingi kwa sababu inabidi kuleta kila mtu pamoja na kukuza makubaliano kama kikundi.
- Kugeuza maoni, na hivyo kudhoofisha au kupunguza kasi ya kufanya maamuzi na utekelezaji.

Licha ya uwezekano wa changamoto hizi, faida za kufanya kazi kwa muungano kwa ujumla huzidi changamoto kwani inaongeza nguvu yenu ya pamoja na inawapa sauti yenye nguvu zaidi ya uanaharakati.

Shughuli 8: Kazi ya vikundi - Faida na changamoto za kufanya kazi pamoja

Gawanya washiriki katika vikundi vinne vidogo - fanya hivi kwa njia yoyote ambayo ilikufaa katika vikao vya awali. Vikundi vyote vinapaswa kujadili maswali yafuatayo kwa pamoja:


- Je, unaweza kufikiria faida maalum za kufanya kazi kwa pamoja?
- Je, unafikiria ni changamoto zipi zinaweza kutokea kwa kufanya kazi kwa njia hii?

Shughuli 9: Hitimisho

Sasa ni wakati wa kumaliza kikao. Fanya muhtasari wa hoja kuu ambazo tumejifunza leo kuhusu hatari, kuzuia hatari, na tathmini ya hatari. Waombe washiriki waongeze kwa muhtasari au wajaze mapungufu yoyote. Shukuru kila mtu kwa kikao kizuri na ushiriki wao. Ruhusu hadi dakika 10 kumaliza kikao na kujibu maswali au maoni yoyote ya mwisho.



Picha © Russell Watkins / Department for International Development



Moduli 5: Kufuatilia maendeleo, kushiriki na kujifunza

Muhtasari wa Moduli

- Ufuatiliaji na tathmini (kwa Kiingereza M&E) ni nini, umuhimu wake ni upi kwa kazi yako na kwa kuonesha mafanikio yako?
- Jinsi wanaharakati vijana wanaweza kufuatilia na kukagua shughuli zao.
- Umuhimu wa kujifunza na kushiriki maarifa na wenzako na washirika.

Moduli 5:

Kufuatilia maendeleo, kushiriki na kujifunza

 <p>Lengo Kuelewa thamani ya kufanya tathmini na kufuatilia ushahidi wa athari za kazi yako</p>  <p>Idadi ya washiriki: Chini ya 24</p>  <p>Wakati unaohitajika: Saa 1 Dakika 40</p>	 <p>Muhtasari wa kikao</p> <ul style="list-style-type: none"> Jifunze kwa nini ufuatiliaji na tathmini ni muhimu Jua jinsi na ni aina gani ya habari unahitaji kukusanya ili kufuatilia mradi wako kwa ufanisi Jifunze jinsi ya kushiriki masomo uliyojifunza na njia za kufanya mradi huo kuwa endelevu kwa muda mrefu 	 <p>Vitu vya kuandaa mapema</p> <ul style="list-style-type: none"> Soma maelezo ya usuli na uyajue vizuri ili uwe na ujasiri wa kuyawasilisha kwa kikundi cha jumla Slaidi za uwasilishaji (iwe za kielektroniki au kwenye karatasi) Jizoeze shughuli ya kusisimua ikiwa utaifanya na kikundi 	 <p>Vifaa vinavyohitajika</p> <ul style="list-style-type: none"> Karatasi za chati, kalamu za alama au kalamu nene, utepe au kitu cha kubandikia karatasi ukutani Mawasilisho Hati Peremende au chokoleti
---	--	---	---

Shughuli	Wakati uliotengwa	Muhtasari
1	Dakika 5	Utangulizi
2	Dakika 5	Majadiliano ya wazi: Jinsi ya kupata habari unayohitaji
3	Dakika 10	Mazungumzo: Ufuatiliaji na tathmini ni nini?
4	Dakika 5	Uwasilishaji wa mkufunzi: Kufuatilia na kutathmini kazi yako
5	Dakika 10	Uwasilishaji wa mkufunzi: Kukusanya habari yako
6	Dakika 30	Kazi ya vikundi: Kutumia kiolezo cha Ufuatiliaji na Tathmini
7	Dakika 10	Majadiliano ya wazi: Kushiriki ujuzi wako
8	Dakika 5	Uwasilishaji wa mkufunzi: Kushiriki maarifa
9	Dakika 20	Kuhitimisha majadiliano na kumalizia mafunzo

5.1 Mwongozo wako wa mkufunzi

Shughuli 1: Utangulizi

Anzisha moduli ukitumia utangulizi ule ule kama ilivyoainishwa katika vikao vya awali: utangulizi wa jumla, ukumbusho wa ulinzi, na ukumbusho wa sheria za kufanya kazi. Kuna njia tofauti za kuanzisha kikao ikiwa unakisimamia moja kwa moja baada ya vikao vingine, au ikiwa ni kikao cha kusimamia kipekee.

Ikiwa ni kikao cha ufuatiliaji, basi tunapendekeza uongoze shughuli ya kusisimua kwa haraka ili kumchangamsha kila mtu. Tafadhali soma tena utangulizi mwingine na ufuate mwongozo huo huo. Una dakika 5 kwa utangulizi na kwa kuelezea mada ya kikao cha leo. Usisahau kukumbusha kikundi chako kuhusu onyo la ulinzi na unyeti na sheria za msingi ambazo mliunda pamoja.

Shughuli 2: Majadiliano ya wazi - Jinsi ya kupata habari unayohitaji

Ongoza kikao cha kuwaza haraka pamoja na kikundi kwa dakika 5 kwa kuwauliza maswali yafuatayo:

- Ni habari gani unahitaji kukusanya ili kujua ikiwa mradi wako umefanikiwa?
- Unawezaje kukusanya habari hii?
- Utashiriki vipi habari hii muhimu (haswa kuhusu mafanikio yako) na watu wengine ili kuonesha kazi yako?

Shughuli 3: Majadiliano ya wazi - Ufuatiliaji na tathmini ni nini?

Sasa unaweza kufahamisha kikundi kuhusu mada ya kikao hiki. Eleza kinahusu ufuatiliaji au kukagua kazi yako wakati wa mradi au kampeni yako, kutathmini kile umefanya mwishoni mwa mradi au kazi yako, kutathmini athari yako na kushiriki kile ulichojifunza.

Kuwa na mazungumzo mafupi na kikundi cha jumla kuhusu maswali yafuatayo:

- Je, unajua nini kuhusu ufuatiliaji na tathmini?
- Unafikiri ni kwa nini ni muhimu kufanya ufuatiliaji na tathmini?
- Waalike washiriki kujibu na kuandika maneno muhimu kwenye karatasi ya chati. Una dakika 5 kwa majadiliano.



Shughuli 4: Uwasilishaji wa mkufunzi - Kufuatilia na kutathmini kazi yako

Sasa ni zamu yako kueleza tunachomaanisha tunapozungumza kuhusu ufuatiliaji na tathmini! Una dakika 10 za kufanya uwasilishaji wako.


Ufuatiliaji na tathmini - mara nyingi huitwa M&E kwa Kiingereza (Monitoring & Evaluation) - ni mkusanyiko wa shughuli au mchakato ambao husaidia kutathmini mafanikio yako na kufikia matokeo bora kutoka kwa miradi yako au uanaharakati wako. Inakupa njia ya kufuatilia kazi yako na mabadiliko gani hufanyika kupitia kile unachofanya, kwa kipindi cha muda mfupi na mrefu. Pia hutoa njia kwako kukagua ikiwa unachofanya, shughuli unazoweka na matokeo unayopata ni mazuri na inasaidia kuboresha hali unayotaribu kabadilisha. Ikiwa sivyo, unaweza kubadilisha kile unachofanya katikati ili kuimarisha kazi yako.

Ufuatiliaji unahusu kukusanya habari mara kwa mara kutambua ikiwa mradi wako una athari nzuri au mbaya. Hii inasaidia kupunguza hatari na kuonesha mapungufu ambayo labda hukuona wakati ulipopanga kazi yako. Pia hukuruhusu kubadilisha njia au jinsi unavyofanya mambo, au hata ni shughuli gani unafanya, wakati unafanya kazi ili uweze kuboresha kazi yako, na mwishowe mafanikio yako.

Tathmini kwa ujumla ni uchanganuzi wa kina zaidi wa mradi wako kupima kiwango cha mafanikio uliyopata. Hii inaweza kufanywa katikati ya mradi, lakini kawaida hufanyika mwishoni mwa mradi kutazama kazi zote ambazo zimefanyika, nini kilienda vyema na nini kinahitaji kuboreshwa. Kukusanya ushahidi ni muhimu sana kwa kazi yako kuthibitisha kuwa unafanya mabadiliko, na kuthibitisha kuwa mabadiliko yenyewe yanawezekana. Kuonesha kuwa una athari kutasaidia kuimarisha sauti yako, uanaharakati wako, na kuwezesha watu zaidi kukusikiliza.

Kwa nini nijisumbue kufuatilia na kutathmini?

- Ufuatiliaji na tathmini kutakusaidia KUTHIBITISHA ikiwa unafanya mabadiliko na ikiwa unafanikiwa.
- Ufuatiliaji utakusaidia kuboresha kazi yako - hukuruhusu kukagua kile kinachofaulu, kile ambacho kina upungufu na hukuruhusu kubadilisha jinsi unavyofanya mambo.





AU



AU



Mfano wa Uwasilishaji: Ni wakati wa Ufuatiliaji na Tathmini!

Ufuatiliaji na tathmini ni mkusanyiko wa shughuli au mchakato ambao husaidia kutathmini matokeo yako na kupata matokeo bora kutoka kwa miradi yako au uanaharakati wako.

Ufuatiliaji unahusu kukusanya habari mara kwa mara kuhusu ikiwa mradi wako una matokeo mazuri au mbaya. Hii inasaidia kupunguza hatari na kuonesha mapungufu ambayo labda hukuona ulipokuwa ukipinga kazi yako.

Tathmini kwa ujumla ni uchanganuzi wa kina zaidi wa mradi wako kupima kiwango cha mafanikio uliyopata. Hii inaweza kufanywa katikati ya mradi, lakini kawaida hufanyika mwishoni mwa mradi kutazama kazi zote ambazo zimefanywa, nini kilienda vyema na ni nini kinahitaji kuboreshwa.

Kwa nini ufuatilie na utathmini?

- Kuelewa ikiwa shughuli na nyenzo zako zilikuwa na ufanisi.
- Kusaidia kutambua matatizo yaliyotokea na kupata suluhisho.
- Kusaidia kujua ikiwa njia ambayo shughuli ilipangwa ndiyo njia sahihi zaidi ya kutatua suala, au kutoa mwongozo kuhusu kuboresha mipango katika siku zijazo.

Kumbuka: Wanaharakati wanapaswa kuwa na uwezo wa kusema kila wakati walichofanya, kwa nini, walipata matokeo gani, na kile walichoifunza.

Shughuli 5: Uwasilishaji wa mkufunzi - Kukusanya habari yako

Habari ambayo unachagua kukusanya ili ujifunze ikiwa mradi wako umefanikiwa haihitaji kuwa habari rasmi kila wakati au kukusanywa kupitia njia rasmi. Wakati mwingine mitazamo ya kibinafsi na kuuliza watu kuhusu maoni au ufahamu wao unaweza kuwa vyanzo vya habari vya maana zaidi. Maswali muhimu ya kuulizana na wenzako pamoja na wengine wanaohusika katika mradi huo ni pamoja na:

Maswali ya ndani

- Tumejifunza nini?
- Ni nini kilienda vyema? Ni nini kinachoweza kuboreshwa?
- Ni mbinu zipi zilizofanikiwa zaidi?
- Tumewezaje kushawishi walengwa wetu?
- Tulitarajia hatari zote?

Maswali ya nje - kwa watu ambao tumejaribu kuwashawishi

- Ni nini kilifanyika vizuri kulingana na maoni yao? Na kwa nini?
- Ni nini tunaweza kuboresha? Vipi?

- Walionaje mafanikio / athari ya jumla ya kazi?

Nyenzo muhimu za habari na njia za ufuatiliaji wa kazi yako ni pamoja na:

- Utafiti rahisi
- Takwimu
- Mahojiano na wadau muhimu
- Vyombo vya habari
- Mazungumzo na vikundi maalum
- Mikutano ya kukagua mradi mara kwa mara na watu wanaohusika katika mradi huo

Vidokezo Vikuu

- Fanya ufuatiliaji na tathmini uwe rahisi. Epuka chochote kitakachotumia muda mwingi.
- Usikusanye habari nyingi zaidi. Zingatia mambo ya lazima.



AU



AU



Mfano wa Uwasilishaji: Zaidi kuhusu ufuatiliaji na tathmini

- Habari unayokusanya kwa ufuatiliaji na tathmini haihitaji kila wakati kuwa rasmi au ngumu.
- Kuuliza maswali wakati mwingine ndiyo njia bora ya kufuatilia kazi zetu.
- Ifanye iwe rahisi - chagua njia ambazo hazitumii muda mwingi.
- Usikusanye habari nyingi zaidi- haswa ikiwa huna wakati wa kuzitumia.

Maswali ya ndani (kwa watu wanaohusika katika kutekeleza mradi) ni pamoja na:

- Tumejifunza nini?
- Ni nini kilienda vyema? Ni nini kinachoweza kuboreshwa?
- Ni mbinu zipi zilizofanikiwa zaidi?
- Tumewezaje kuwashawishi walengwa wetu?
- Tulitarajia hatari zote?

Maswali ya nje - kwa watu ambao tumejaribu kuwashawishi:

- Ni nini tulichofanya vizuri kulingana na maoni yao? Na kwa nini?
- Ni nini tunaweza kuboresha? Vipii?
- Je, walionaje mafanikio / matokeo ya jumla ya kazi?

Nyenzo muhimu za habari ni pamoja na:

- Utafiti rahisi
- Takwimu
- Mahojiano na wadau muhimu
- Vyombo vya habari
- Mazungumzo na vikundi maalum
- Mikutano ya kukagua mradi mara kwa mara na watu wanaohusika katika mradi huo

Shughuli 6: Kazi ya vikundi - Kutumia Kiolezo cha Ufuatiliaji na Tathmini

Waeleze kikundi kuhusu kiolezo cha ufuatiliaji na tathmini (angalia hapa chini) na uwaeleze ni jinsi gani wanaweza kurekodi habari hii kwenye kiolezo. Itafaa ikiwa watakamilisha jedwali kulingana na mkakati waliotengeneza hapo awali katika Moduli ya 3: Kikao cha 2

Alika kikundi wawasilishe mipango yao ya ufuatiliaji na tathmini iliyokamilika na uwahimise kuzikamilisha pamoja. Kumbuka kuisitiza kwamba wanapaswa:

- Kuepuka njia inayotumia muda mwingi.
- Kukusanya habari muhimu pekee.

Mkakati wa uanaharakati uliotengeneza hapo awali ndio zana yako ya msingi ya kuandaa ukaguzi wa shughuli zako. Hatua inayofuata ni kufikiria kuhusu matokeo au athari. Tumia kiolezo cha msingi cha ufuatiliaji na tathmini kwa kujaza habari mara kwa mara na kuikagua kwa njia ya kimfumo. Tayari utakuwa umejaza safu 1 hadi 3 kama sehemu ya mkakati wako wa uanaharakati, kwa hivyo kwa mpango wako wa ufuatiliaji na tathmini, sasa utahitaji kuzingatia safu 4, 5, 6 na hatari / mawazo.

Ruhusu dakika 20 kwa vikundi kujadili na kukamilisha kiolezo kadiri wawezavyo. Kisha wana dakika 10 za kuzungumza kuhusu yale waliyojaza. Ruhusu dakika 10 kwa majadiliano kuhusu mawazo yoyote au maswali kuhusu ufuatiliaji na tathmini.

Kiolezo cha Ufuatiliaji na Tathmini

<p>Madhumuni Je, kwa pamoja mnataka kufikia nini?</p>	<p>Shughuli / Matokeo Mtafanya nini? Matokeo yenu makuu ni yapi?</p>	<p>Nyenzo / Matokeo Ni mambo yapi yanahitajika kukusaidia kufikia lengo lako?</p>	<p>Utaweza kutathmini vipi ikiwa yamefanikishwa? Ni zana, rasilimali za habari, au viashiria gani unahitaji kukusanya ili kuona ikiwa umefikia lengo lako? Utakusanya lini na vipi?</p>	<p>Je, kulikuwa na tofauti gani katika muda mfupi? Matokeo na mafanikio yako ya muda mfupi yalikuwa nini?</p>	<p>Hatari zinazoweza kutokea Je, kuna tishio, athari mbaya au changamoto zipi ambazo zinaweza kudhibiti kazi yako kuhusu suala hili? Pia fikiria kuhusu masuala ya kijinsia yanayohusika.</p>	<p>Ni mabadikio gani yalifanyika kwa kipindi kirefu zaidi? Je, kulikuwa na matokeo gani ya muda mrefu (kwa mfano, mwaka mmoja kuendelea)? Kwa muda mrefu zaidi, umeona mabadikio yoyote?</p>	<p>Je, kulikuwa na hatari au dhana zozote za awali zilizohusika? Bainisha wazi ni nani anayeongoza kwa kazi gani maalum, na jukumu lao ni lipi katika kuhakikisha imekamiliika.</p>
--	---	--	--	--	--	---	--

Shughuli 7: Majadiliano ya wazi - Kushiriki ujuzi wako

Zaidi ya kufuatilia kazi yako na kuitathmini mwishowe - pia ni vizuri kushiriki matokeo yako (mazuri au yasiyo mazuri) na watu wengine, haswa wale unaofanya kazi nao na watu ambao umejiunga nao au kushiriki katika kazi yako. Uliza kikundi kizima jinsi wanavyofikiria wanaweza kushiriki mafunzo na ujuzi wao na wengine katika mitandao yao - washirika, wenzao au wale ambao wamekuwa wakifanya kazi nao. Waulize watambue ni watu gani muhimu watashirikiana nao kujifunza, ni njia ipi bora ya kushiriki kile wanachopata, na ni kwa nini wangefanya hivi / kwa nini ni muhimu.

Tenga dakika 10 kwa majadiliano.

Shughuli 8: Uwasilishaji wa mkufunzi - Kushiriki maarifa

Tenga dakika 5 za kupitia uwasilishaji ufuatao kuhusu mapendekezo ya jinsi kikundi kinaweza kukusanya habari na kushiriki matokeo yao.

Hatua inayofuata ni kushiriki kile ulichojifunza na ujuzi pamoja na washirika na wenzako, haswa wale ambao umekuwa ukifanya kazi nao. Kushiriki masomo na tajiriba ambazo umejifunza, pamoja na kufeli na changamoto ambazo umepata, ni muhimu kwani inasaidia kila mtu kuimarisha kazi yake.

Unaweza kushiriki masomo kupitia:

- Majadiliano yasiyo rasmi (kwa mfano, kwenye mkutano wa kikundi cha vijana au shuleni).
- Mtandaoni (kupitia vikundi vya barua pepe, majarida au vikundi vya Facebook).
- Kwa upana zaidi na washiriki wengine wa *Girls Not Brides* kwa kuwasiliana na sekretarieti ya *Girls Not Brides* au mashirika yoyote ya kitaifa yanayoshughulikia masuala kama hayo, pamoja na mashirika ya kitaifa ya *Girls Not Brides*.
- Kuwasilisha kazi yako kutumia uchambuzi wa visa.



AU



AU



Uwasilishaji wa mfano

- Kubadilishana ujuzi husaidia kuimarisha kazi zetu.
 - Shiriki masomo kupitia majadiliano yasiyo rasmi (kwa mfano, kwenye mkutano wa kikundi cha vijana au shuleni) au mitandaoni (kupitia vikundi vya barua pepe, majarida au vikundi vya Facebook) na kwa upana zaidi na washiriki wengine wa *Girls Not Brides*.
-

Shughuli 9: Majadiliano ya hitimisho

Pongezi! Sasa tumefikia mwisho wa mafunzo. Umefaulu. Rejelea hoja kuu kuhusu ufuatiliaji na tathmini kwa kikundi, na kisha ufanye zoezi la mwisho la kikundi. Chagua washiriki tofauti kujibu maswali yafuatayo:

- Je, ufuatiliaji unamaanisha nini?
- Kwa nini ufuatiliaji na tathmini ni muhimu?
- Je, umejifunza nini katika kikao hiki?
- Ni njia gani moja ya kushiriki mafunzo na wengine?
- Je, utafanya nini tofauti baada ya mafunzo haya?
- Je, ni jambo gani muhimu zaidi ulijifunza?
- Je, utatumiaje mafunzo haya katika kazi yako?
- Je, tunawezaje kusaidiana katika kazi yetu ya uanaharakati?

Wape peremende kama zawadi kwa kujibu, na uwaulize washiriki tofauti maswali tofauti hadi kila mtu kwenye kikundi ajibu swali. Una dakika 15 kufanya shughuli hii.

Kwa kuwa hiki ni kikao cha mwisho kwenye mafunzo, wapongeze kikundi chako kwa kazi nzuri, na kwa yote wamefanya kufanikisha mafunzo! Kama ishara ya wema, unaweza kumtengenezea kila mmoja cheti ili kuwapongeza kwa kukamilisha mafunzo.



Hitimisho la jumla la mafunzo

Hongera!

Sasa umekamilisha mafunzo yako. Umefanya vyema na kwa bidii yako yote - na tunatumaini kuwa ulikuwa mchakato mzuri mno. La muhimu zaidi, tunatumaini kuwa vijana ambao ulikuwa ukifanya kazi nao walifurahia vikao, walijifunza kutoka kwa warsha, na sasa wanajisikia wameimarishwa katika kazi yao ya kutetea mabadiliko.

Tunapendekeza sana ufanye tathmini mwishoni mwa mafunzo yako na vijana ambao umekuwa ukifanya kazi nao. Hii ni hatua muhimu kukamilisha kwani itakupa hisia ya jinsi washiriki walithamini mafunzo au ikiwa kulikuwa na vikao vyovyote ambavyo vinahitaji kufuatiliwa. Tumeambatisha fomu ya tathmini ya mfano hapa chini ili kukusaidia kujibu maswali ambayo ni muhimu kuuliza kikundi chako. Waombe waijaze, au fomu nyingine ya mbadala, mwishoni mwa mafunzo. Wanaweza kuifanya bila kutambulisha majina yao ikiwa wangependa hivyo, lakini la muhimu zaidi ni kwamba upate kufahamu jinsi walivyohisi kuhusu mafunzo na jinsi wanavyopanga kuyatumia katika kazi yao.

Tunapendekeza pia ufuatilie kikundi hicho hicho baada ya miezi michache ili kuangalia jinsi wanavyoendelea, jinsi kazi yao inavyokwenda, na jinsi wametumia habari waliyojifunza kwenye mafunzo katika kazi zao - au ikiwa hata wameitumia. Kufuatilia hili na kuwafuatilia washiriki wenyewe ni muhimu kwani inakupa ufahamu kuhusu ni ujuzi gani wametumia au kufaidika nao zaidi, na kuona ni jinsi gani wamejumuisha ujuzi au habari yoyote mpya katika kazi yao ili kusaidia kukomesha kuozwa kwa watoto.

Tunawatakia kila la heri katika kazi yenu nzuri. Pamoja tunaweza kufikia maono yetu ya pamoja ya ulimwengu ambao kila mtoto anaweza kuchagua siku za usoni anazotaka yeye mwenyewe, ulimwengu ambao vijana wote wana sauti yenye nguvu ya kupinga udhalimu na ukosefu wa usawa. Pamoja tunaweza kukomesha kuozwa kwa watoto.

Asante!

Fomu ya tathmini: Mafunzo ya Simama, Sikika!

Jina (Kwa hiari)

Jinsia

Umri

Shirika

Nchi

Kwa ujumla, unatathmini vipi mafunzo haya ya uanaharakati wa vijana?

Tafadhali tathmini maoni yako kati ya 1 (kuumaanisha ni duni sana) na 5 (kumaanisha ni bora sana).

Tafadhali weka alama katika kila swali katika jedwali lifuatalo ili kuonesha maoni unayokubaliana nayo.

	Hapana	Kwa kiasi fulani	Sana	Kwa uhakika
<i>Ninaweza kueleza kuozwa kwa watoto ni nini, kunasababishwa na nini na kunaweza kuzuiwa vipi.</i>				
<i>Ninaelewa jinsi ya kuunda mkakati rahisi na wazi wa kazi yangu ya uanaharakati.</i>				
<i>Ninaelewa jinsi ya kujenga mtandao wa watu maalum na kushawishi walengwa wangu wa uanaharakati.</i>				
<i>Ninaelewa jinsi ya kutathmini kazi yangu na kukagua ni mabadiliko yapi yalifikiwa.</i>				

Je, ni kikao kipi kilikuwa muhimu zaidi kwako? Kwa nini?

Je, ni kikao kipi unaonelea kinahitaji kubadilishwa zaidi au kinahitaji kuboreshwa? Kwa nini?

Je, utatumia vipi yale uliyojifunza katika mafunzo kwa kazi yako / maisha yako katika siku zijazo? Taja mambo mahususi.

Je, una maoni mengine yoyote kwa wakufunzi?

Je, unahitaji msaada upi ili uweze kutumia ulichojifunza katika vikao hivi?

Girls Not Brides
ni ushirikiano wa
kimataifa wenye zaidi
ya mashirika 1000 ya
kiraia kutoka zaidi
ya nchi 95, ambazo
zimejitolea kupambana
na kuozwa kwa watoto
na zilizo na dhamira
ya kuwawezesha
wasichana kufikia
uwezo wao kamili.



The Global Partnership
to End Child Marriage

Chapisho la Agosti 2018 la
Girls Not Brides
Ghorofa ya Saba
65 Leadenhall Street London,
EC3A 2AD Uingereza

T: 0203 725 5858
F: 0207 603 7811

 www.GirlsNotBrides.org

 info@GirlsNotBrides.org

 www.facebook.com/GirlsNotBrides

Girls Not Brides ni kampuni inayodhibitiwa na
dhamana (Na. ya Usajili 8570751) na shirika
la msaada lililosajiliwa nchini Uingereza na
Wales (Na. ya Usajili 1154230)